Hii ni nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 4 Novemba, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kikao cha kwanza cha Mkutano wa Kumi na Tatu kinaanza, Katibu!

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa inayotolewa inahusu Miswada iliyopitishwa na Bunge hili katika Mkutano uliopita wa Kumi na Mbili. Bunge lilipitisha Miswada mitatu na yote imekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais na sasa ni Sheria Na.13, 14 na 15 za nchi hii. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):**

Nakala ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

### Ziara za Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Mikoani

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza:-

Je, ni lini Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu watajenga tabia ya kutembelea Mikoa mbalimbali nchini kuanzia tarehe ya kuwasilishwa kwa swali hili hapo tarehe 31 Julai, 2003 ili kuona matatizo mbalimbali ya wananchi badala ya mtindo wa sasa wa kumwachia Waziri Mkuu peke yake kufanya ziara za mara kwa mara Mikoani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, hawana tabia ya kumwachia Mheshimiwa Waziri Mkuu peke yake kufanya ziara za mara kwa mara Mikoani akiwa anafuatilia matatizo mbalimbali ya wananchi na kuhimiza maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Mheshimiwa Rais kutangaza Baraza jipya la Mawaziri mwishoni mwa mwaka 2000, Katibu wa Baraza la Mawaziri alitoa Waraka wenye kuonyesha majukumu ya kazi za Wizara mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu. Kila Waziri wa Nchi katika Ofisi hiyo anayo majukumu yake ambayo yanamfanya wakati wote awe na mambo mengi ya kufanya na hivyo kumlazimu kufanya ziara huko Mikoani kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wake. Kwa mfano, Waziri wa Nchi anayeshughulikia Habari na Siasa katika kipindi cha Januari, 2001 hadi Oktoba, 2003 amefanya ziara Mikoani zaidi ya Mikoa tisa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Singida, Ruvuma, Mwanza, Lindi, Kilimanjaro na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi anayeshughulikia Sera, yeye ametembelea Mikoa 14 ambayo ni Lindi, Mtwara, Morogoro, Mbeya, Arusha, Mwanza, Kilimanjaro, Iringa, Dodoma, Ruvuma, Dar es Salaam, Pwani, Singida na Manyara. Mheshimiwa Waziri Mkuu anapofanya ziara, Mawaziri wa Nchi hupewa taarifa ya ziara hizo na kufanya ufuatiliaji wa mambo ambayo yametolewa maelekezo na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba tutaendelea kuweka mipango ya kutembelea Mikoa ili kuona matatizo yanayokwaza jitihada mbalimbali zilizoandaliwa kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo na kuboresha hali ya maisha vijijini na mijini.

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Waziri Mkuu kama alivyotunga swali Mheshimiwa Semindu Pawa, hufanya juhudi za kutembea je, haamini kwamba hilo swali lililoulizwa haliendi sambamba kutokana na kauli ya Serikali ya Mkoa wa Kigoma ambao mpaka sasa Waziri wa Nishati na Madini hajatembelea tangu amekuwa Waziri na tatizo lile tulimwambia Waziri Mkuu anayelifahamu je, hilo linaweza kujibika kwa sasa hivi ili tuweze kupata umeme wa muda mrefu uliokosekana? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haliwezi kujibika kwa sasa hivi kwa sababu swali la msingi lilihusu Mawaziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Kicheko)*

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kama msimamizi wa Mawaziri wote ili kuhakikisha kwamba Mawaziri wanatembelea Wilaya zote za nchi hii kwa kipindi cha miaka mitano, ni utaratibu gani anaoutumia kuhakikisha kwamba Mawaziri wanatambelea Wilaya zote katika nchi vinginevyo Mawaziri hawa wanashinda kwenye Majimbo yao?

**SPIKA:** Swali limeelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Waziri baada ya kupewa Wizara yake anajipangia utaratibu wake wa kazi kwa kipindi kifupi, kipindi cha kati na kipindi cha muda mrefu. Kwa hiyo, kwa kweli ni jukumu la Waziri kuhakikisha kwamba kwa kadri inavyowezekana anatembea kila mahali kwa kuanzia na yale maeneo ambayo kwa mwelekeo wa sekta yake yana matatizo zaidi.

Kwa hiyo, nina hakika Waheshimiwa Mawaziri wanapanga utaratibu wao kutegemeana na uzito wa kazi katika Wizara zao ili waweze kutembea kila mahali na nina hakika kabla ya miaka mitano Mawaziri wote watakuwa wametembelea Wilaya zote za nchi hii. *(Kicheko)*

Na. 2

**Kuboresha Maslahi, Elimu na Vitendea Kazi kwa Waandishi wa Habari**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kuboresha maslahi, elimu na vitendea kazi kwa Waandishi na Watangazaji wa Habari ni lazima kuweka mazingira mazuri ya kuwaelimisha,

kuwaadilisha na kuwapa motisha na pale inapobidi wapewe *Overtime Allowance* wanapofanya kazi zaidi ya muda wa kawaida wa kazi:-

(a) Je, Vyombo vya Habari vya Serikali vinatekeleza hayo?

(b) Je, Vyuo vyetu Tanzania vinatoa Shahada *(Masters Degree)* ya Utangazaji na Uandishi kwa wafanyakazi wa fani hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, Mkoa wa Kaskazini Unguja, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika kuboresha maslahi, elimu na vitendea kazi kwa Waandishi wa Habari na Watangazaji wa vyombo vya habari vya Serikali ni lazima kuweka mazingira mazuri ya kuwaelimisha, kuwaadilisha na kuwapa motisha kwa mfano posho ya kazi za ziada yaani *overtime.*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka kanuni na taratibu mahsusi za kushughulikia maslahi siyo ya wanahabari tu bali pia na ya watumishi wake wote. Kwa mfano, katika kuboresha maslahi yao, Serikali imekuwa ikiongeza mishahara kila wakati hali ya uchumi wa nchi inaporuhusu. Aidha, Serikali huwapandisha vyeo watumishi wake wanaostahili kila muda wa stahili hiyo unapowadia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu na vitendea kazi, vyombo vya habari vya Serikali vimepangiwa utaratibu wa kujiweka mipango ya mafunzo na kujitengea mafungu ya fedha za matumizi kutokana na Bajeti ya Serikali ya kila mwaka ili kulipia mafunzo ya wanahabari wao na kujinunulia vitendea kazi vinavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, malipo ya kazi za ziada hutolewa kufuatana na kanuni na taratibu za fedha zilizowekwa na Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa sasa inavyo Vyuo Vikuu viwili vya binafsi vinavyotoa mafunzo ya taaluma ya Uandishi na Utangazaji wa Habari. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Tumaini kilichoko Iringa na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine kilichoko Mwanza. Hata hivyo, hakuna Chuo katika hivyo kinachotoa mafunzo hayo kwa ngazi ya Shahada ya Uzamili au Digrii ya Pili yaani *Masters* au zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Chuo Kikuu cha tatu cha taaluma ya habari kimekuja hivi karibuni wakati Chuo cha Uandishi wa Habari cha Tanzania *(TSJ)* kilipojiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tarehe 01 Julai, 2003 na kuwa Taasisi ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na uongozi wa taasisi hiyo kuteuliwa rasmi. Katika miaka

michache ijayo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitaweza kutoa Digrii ya Pili yaani *Masters* na hata za Udaktari wa Falsafa kwa fani hizo za utangazaji na Uandishi.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Chuo cha *TSJ* ni Chuo kizuri ambacho kinatoa Waandishi wa Habari na Watangazaji lakini hakijafikia hatua ya kutoa Digrii ya Kwanza wala ya Pili na hivi sasa kinakabiliwa na matatizo ya miundombinu na vitendea kazi.

Je, kuna mkakati gani wa Wizara yake kushirikiana na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu ili kukiboresha Chuo kile?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya msingi nimesema hapa kwamba *TSJ* sasa hivi hakipo badala yake kimejiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kwa hivyo kitaweza kutoa Digrii ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu. Kwa sababu kiko chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitaweza kupata msaada mkubwa kupitia Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa vipo vyombo vya habari ambavyo vinafanya kazi sambamba na vile vya Serikali kama vile *ITV, DTV* na vinginevyo na kwa kuwa zipo ziara mbalimbali zinafanywa na viongozi wetu wa Kitaifa wakati huu tunaboresha uchumi wa nchi yetu lakini hivi vyombo vingine havipati nafasi ya hawa Waandishi kutembea na wale viongozi kwenye nchi hizo ili wakirudi waandike habari nzuri zaidi. Kwa mfano, kile...

**SPIKA:** Sasa swali.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Je, Serikali itakubaliana nami kuwa sasa ni wakati mzuri wa kuandamana na hawa Waandishi wengine ili waweze kuboresha uchumi wakirudi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, napenda kumuarifu Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kwamba Serikali yetu haibagui wenye vyombo vya habari binafsi ndio maana wakati anaongea na Waandishi wa Habari, Waandishi wote wanaitwa wa redio, televisheni na magazeti pale Ikulu au kwa Waziri Mkuu.

Mfano halisi wakienda Mikoani Waandishi wa Habari wa binafsi wanashirikishwa kwa sababu madhumuni yetu ni kutaka kuona kwamba maendeleo ya nchi taarifa zake zinawafikia watu wote.

Mheshimiwa Spika, lakini la msingi ni kwamba hivi karibuni pia Rais wetu ametembelea Japan, Ujerumani na amechukua Waandishi wa Habari wa *ITV* na vyombo vingine. Kwa hiyo, hatubagui Waandishi wa Habari wa vyombo binafsi.

Na. 3

**Malipo ya Waathirika wa Matukio ya Januari 26 na 27, 2001**

**MHE. ALI SAID SALIM a**liuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliunda Tume ya Kuchunguza Matukio ya Januari 26 na 27, 2001 na kwa kuwa Tume hiyo ilifanya kazi iliyokusudiwa na kupeleka taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais na kwa kuwa katika muafaka ilikubalika kwamba wale wote walioathirika na matukio yaliyotajwa wawe wameshalipwa fidia ifikapo tarehe 31 Desemba, 2002 lakini jambo la kusikitisha ni kwamba hadi sasa watu hao hawajalipwa na hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili hiyo katika Bajeti ya mwaka 2003/2004:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kwa kufanya hivyo ni kuvunja Muafaka hasa ikizingatiwa kuwa Mheshimiwa Rais iliahidi kutekeleza Muafaka uliofikiwa mbele ya Watanzania wote na dunia kwa ujumla?

(b) Je, Serikali inaweza kutamka kwamba ni lini watu hao watalipwa fidia hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Jimbo la Ziwani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Katiba ya nchi yetu pamoja na mambo mengine inatambua kwamba utu na haki za binadamu lazima zilindwe na kuheshimiwa. Kwa kuzingatia wajibu huu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliunda Tume ya Kuchunguza Matukio ya tarehe 26 na 27 Januari, 2001. Tume hii ilipewa majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili matukio kama hayo yasirudie hapo baadaye. Aidha, Muafaka uliofikiwa kati ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na *Civic United Front (CUF)* umeiwezesha nchi hii kuendelea kuwa na mshikamano, maelewano, udugu, umoja na kuweka msingi imara wa kuimarisha umoja wa wananchi wetu. Ni jambo la kujivunia na hatuna budi kulilinda kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, kila inapobidi Serikali hulazimika kutoa kifuta machozi kwa raia wake waliopata athari fulani kama tukio la tarehe 26 na 27 Januari, 2001. Baada ya

uchunguzi kufanyika na matokeo kuwasilishwa Serikalini, imekubalika kwamba kifuta machozi sio fidia kitolewe kwa walioathirika au familia za walioathirika mapema iwezekanavyo. Taratibu zinaendelea kufanyika kutekeleza ahadi hiyo. Ni kweli miezi kadhaa imepita tangu Tume ya Mbitta iwasilishe taarifa yake kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika kipindi hiki Serikali imekuwa ikishirikiana na Jumuiya ya Madola kuwasiliana na wahisani watakaoweza kusaidia suala la kifuta machozi kwa waathirika. Hii inatokana na ukweli kwamba hali yetu ya uwezo wa kifedha sio mzuri lakini pia Jumuiya ya Madola ina ahadi yake ya kusaidia kupitia Mfuko wa Ujenzi Mpya wa Maridhiano *(Fund for Reconstruction and Reconciliation).* Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge na waathirika waendelee kuvuta subira wakati suala hili linashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Muafaka umekwishatekelezwa kwa kiwango kikubwa mpaka sasa. Kwa hakika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinastahili pongezi kwa utekelezaji huo wa kuridhisha. Hivyo hakuna suala la Serikali kukiuka Muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi sana baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali zote mbili zimekuwa zikitekeleza muafaka kwa makini na uaminifu mkubwa. Kwa hiyo, Serikali haijavunja Muafaka kwa sababu inahitajika kuwa makini katika kufanya malipo.

(b) Serikali haiwezi kutamka ni lini wahusika watalipwa kifuta machozi kwa sababu taratibu za malipo hazijakamilika. Pindi taratibu hizo zitakapokamilika wahusika watataarifiwa kwa uwazi wa kutosha kulingana na mazingira yenyewe.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri kidogo ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa imechukua muda mrefu kulipwa hicho kifuta machozi kwa waathirika je kuna matumaini yoyote ya kutekelezwa taarifa za Tume mbili ambazo zimeundwa chini ya Muafaka huu huu kwa upande wa Zanzibar Tume ya Waliovunjiwa Nyumba pamoja na Tume ya Waliofukuzwa kazi kwa sababu za kisiasa?

**SPIKA:** Samahani, hebu rudia swali lako hatujalielewa vizuri.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Kutokana na kuchukua muda mrefu kutekelezwa taarifa ya Tume ya Mbitta, je, kuna matumaini yoyote ya kutekelezwa taarifa za Tume mbili ambazo zimeundwa Zanzibar chini ya Muafaka huu, Tume ya Waliovunjiwa Nyumba pamoja na Tume ya Waliofukuzwa Kazi kutokana na sababu za kisiasa?

**SPIKA:** Sawa, litajibiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, jibu la msingi linahusu pia hayo matukio aliyoyataja ya kuvunjiwa nyumba pamoja na watumishi kule Zanzibar. Swali lililoulizwa hapa linahusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yale mengine yanahusu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, lakini napenda kumhakikishia kwamba yote yanakwenda sambamba kwa utaratibu ule ule kama ilivyojibiwa hapa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Muafaka tuliweka ratiba maalum ya utekelezaji na kwa kuwa ratiba hiyo sasa kwa kiwango kikubwa imepitwa sana, je, Serikali inaweza kutuhakikishia Wabunge kwamba pamoja na kuchelewa huko kutekelezwa yale mambo ya msingi ambayo tumekubaliana yatatekelezwa kabla ya uchaguzi wa 2005?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, hiyo ndio nia ya Serikali. *(Makofi)*

Na. 4

**Maadhimisho ya Sikukuu ya Uhuru na Muungano**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu ilipata Uhuru tarehe 9 Desemba, 1961 na kuungana na Zanzibar na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapo tarehe 26 Aprili, 1964; na kwa kuwa maadhimisho ya Sikukuu hizo mbili yamebakia tu katika ukaguzi wa gwaride la heshima la Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama kunakofanywa na Amiri Jeshi Mkuu:-

Je, isingekuwa vizuri maadhimisho ya siku hizo mbili muhimu katika nchi yetu yaani siku ya Uhuru na Muungano kila mwaka pamoja na kukagua gwaride rasmi, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akalihutubia Taifa *(Presidential Address to the Nation)* ikawa ndiyo fursa ya kuelezea maendeleo ya nchi yetu yanayotokana na uhuru na muungano wetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Damas Nakei, Mbunge wa Babati Magharibi, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1961 nchi yetu ilipopata Uhuru tumekuwa tunasherehekea sikukuu mbalimbali za Kitaifa kama matukio maalum ya kihistoria kwa Taifa letu. Lengo kubwa la kusherehekea sikukuu hizi ni kujikumbusha tulikotoka na tulipofikia.

Hivyo, viongozi wetu wa Kitaifa hususani Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu wamekuwa wanashiriki kwa kupokea maandamano ya wananchi, kukagua na kupokea heshima ya gwaride la Majeshi yetu ya ulinzi na usalama pamoja na kuhutubia Taifa kupitia vyombo vya habari.

Viongozi wa nchi yetu wamekuwa ama wakifanya moja kati ya mambo hayo matatu au yote kutegemea wanavyoona inafaa. Rais wa Awamu ya Tatu anawahutubia wananchi kila mwezi kwa njia ya televisheni na redio. Aidha, hotuba zake huchapishwa kwenye magazeti. Utaratibu huu mzuri umepongezwa na wengi na unawawezesha wananchi kufahamu mambo muhimu ya Kitaifa kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii. Mheshimiwa Rais bado anaweza kuhutubia kwenye sikukuu ya uhuru na ya Muungano akiona inafaa.

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri, napenda kuuliza swali moja la nyongeza.Je, Serikali haioni umuhimu wa gwaride kama hilo kufanyika kila Mkoa ili kuwaweka karibu wananchi walioko Mikoani ambao hawana *video* au wasiokuwa na redio na wenyewe wakajionea kwa macho yao kisha gwaride hilo likakaguliwa na Mkuu wa Mkoa kwa niaba ya Rais?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, mara nyingi tumekuwa tunafanyia kwenye viwanja vya Dar es Salaam au Zanzibar lakini ni kutokana na umuhimu wa shughuli zenyewe. Lakini pia uandaaji wa shughuli hizi ni gharama kubwa kwa sababu una *involve* hela nyingi sana maana wale Askari wote wanao-*perform* katika gwaride lile sio wa Dar es Salaam peke yake. Kwa hiyo, gharama nayo ni sehemu muhimu ya kuzingatia katika hili.

Mheshimiwa Spika, pili, uwezekano wa kwenda Mikoani upo na ndio maana mwaka huu sherehe za Uhuru na Jamhuri zitaazimishwa hapa Mkoani Dodoma kwa malengo hayo hayo.

Na. 5

**Kina Mama na Watoto kula Udongo**

**MHE. AISHA P. MAGINA** aliuliza:-

Kwa kuwa wapo wanawake hasa wale wajawazito pamoja na watoto wanakuwa na tabia ya kula udongo.

(a) Je, kwa watu wenye tabia kama hizo huwa wanasumbuliwa na ugonjwa gani?

(b) Je, ni matatizo gani yanayoweza kuwapata watu wanaokula udongo?

(c) Kama kuna ugonjwa wowote unaotokana na tabia hiyo; je, tiba yake ni nini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aisha Magina, Mbunge wa Viti Maalum *(CUF),* lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tabia ya kula udongo husababishwa na upungufu wa madini ya chuma mwilini *(Iron Deficiency).* Madini ya chuma hupungua mwilini kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo:-

(i) Upungufu wa lishe bora *(Nutritional Iron Deficiency);*

(ii) Kwa kuwa madini ya chuma kwa sehemu kubwa yanapatikana kwenye chembechembe nyekundu za damu *(Red Blood Cells),* kupoteza damu kwa njia yoyote husababisha upungufu wa madini chuma mwilini mfano malaria, minyoo, bawasili na kadhalika.

(b) Mheshimiwa Spika, watu wanaokula udongo huweza kupata minyoo kwa kuwa si kila udongo ni msafi na hivyo kuzidisha upungufu wa madini chuma mwilini.

(c) Mheshimiwa Spika, tiba ya ugonjwa huu ni kumpa mgonjwa vidonge vyenye madini ya chuma *(Ferrous Sulphate)* ambavyo huondoa hamu ya wagonjwa kula udongo. Aidha, ni muhimu kutibu ugonjwa unaosababisha upungufu wa madini ya chuma kama vile malaria, minyoo, bawasili na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, akina mama wajawazito wanaohudhuria kliniki *(Antenatal Clinic)* hupatiwa vidonge hivi vya *Ferrous Sulphate* ili kuondoa upungufu wa madini hayo ambao husababishwa na lishe duni au malaria kwa wajawazito.

**MHE. AISHA P. MAGINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna mtoto mmoja ameripotiwa na vyombo vya habari ana tabia ya kula magodoro sasa huo nao ni ugonjwa gani? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Kuna ugonjwa wa kisaikolojia au *psychiatric illness* unaoitwa *Paica* na ugonjwa huu huwafanya wagonjwa hao kula vitu ambavyo kwa kawaida haviliwi sio magodoro peke yake. Kwa hiyo, tunadhani kwamba *Paica* ndio ugonjwa aliokuwa nao huyo mtoto lakini ameshapelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa uchunguzi zaidi.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, nina swali moja la nyongeza kuhusu ulaji wa udongo.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekwepa kufafanua kwamba udongo ule una madhara ndani ya mwili wa binadamu, je, kama Mheshimiwa Naibu Waziri atathibitisha hayo kwamba udongo una madhara Serikali itachukua hatua gani ili kuzuia udongo huo na kufanya kitu mbadala ili kunusuru maisha na siha za wanawake ambao tunawategemea? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba udongo unaoliwa hususani na wanawake wajawazito unaweza kuleta madhara ya kiafya kwa sababu si kila udongo ni salama. Kwa hiyo, sikukwepa kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema bali nimesema wazi kabisa kwamba kula udongo kunaweza kusababisha minyoo ambayo inaweza kusababisha zaidi upungufu wa hayo madini ya chuma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunachosema hapa ni kwamba wanawake hawa wajawazito au watoto wanaokula udongo wakifikishwa kwenye kliniki zile watatambulika na watapewa hayo madini ya chuma *(Ferrous Sulphate)* na ile hamu ya kula udongo itatoweka. Aidha, ni vema kuzingatia lishe bora ambapo chakula kama maini yamesheheni madini haya ya chuma na vile vile mboga za majani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna sababu ya kutoa kitu mbadala badala yake ni kutibu magonjwa hayo na kumpa mtu madini chuma.

**MHE. ADELASTELA E. MKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa hao wanaokula udongo akina mama na watoto wao wamekuwa wazi kujieleza vizuri kwa Daktari lakini wapo wanaume ambao wana tatizo hili na hawawezi kujieleza vizuri kwa Daktari hao nao tutawapataje ili kuwatibu? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba sababu zinazomfanya mtu atamani kula udongo ni upungufu wa madini chuma ndani ya mwili wake. Mara nyingi tatizo hili huwapata watoto wadogo na wanawake wajawazito lakini nilisema kama mtu anapoteza damu kwa mfano wagonjwa wa bawasili *(Hemorrhoids)* wanapoteza damu kwa muda mrefu na husababisha pia upungufu wa madini chuma na hivyo hutamani kula udongo.

Kwa hiyo, hata wale ambao hawasemi kwamba wana hamu ya kula udongo lakini endapo watafika hospitali na kuonekana kwamba wamepungukiwa na madini chuma basi hupatiwa dawa hizo.

Na. 6

**Huduma za Matibabu Bure kwa Makundi Maalum**

**MHE. PETER KABISA** aliuliza:-

Kwa kuwa pamoja na Serikali kutamka mara kwa mara kwamba wazee, watoto wenye umri chini ya miaka sita na akina mama wajawazito ambao hawana uwezo wa kuchangia huduma za matibabu watapatiwa huduma hizo bure lakini baadhi ya wananchi wa Jimbo la Kinondoni ambao wapo kwenye kundi hilo maalum hawapatiwi huduma hizo bure kama ilivyokusudiwa zaidi ya kupatiwa kadi kujiandikisha kumwona daktari ambapo hutakiwa walipe gharama hizo au huambiwa dawa hakuna:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba maamuzi yake hayaheshimiwi na baadhi ya wauguzi kwenye hospitali na zahanati zake?

(b) Je, Serikali inasema nini juu ya wauguzi na wahudumu ambao wanapuuzia maamuzi ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, naomba kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa mwongozo kuhusiana na Sera ya Uchangiaji ambayo pia imeainisha makundi ya wenye stahili ya kupatiwa matibabu bila malipo ambao ni akinamama wajawazito, watoto walio chini ya umri wa miaka mitano pamoja na wazee walio na umri wa miaka sitini na zaidi ambao hawana uwezo wa kulipia matibabu hayo.Wajibu wa kusimamia utekelezaji wa jambo hili upo katika Mamlaka za Mikoa na Wilaya. Mtumishi wa afya atakayekiuka utaratibu huu, Mamlaka husika zinapaswa kumchukulia hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Kinondoni imeshaunda Bodi ya Afya ya Wilaya, hivyo ni vema Bodi hii ikatumika kuwadhibiti wakorofi wachache wanaokiuka sera hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya jumla, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sera hii ya msamaha kwa makundi maalum kwa kiwango kikubwa imekuwa ikitekelezwa vizuri katika vituo vingi vya utoaji huduma. Lakini ni kweli kwamba kuna baadhi ya watumishi wachache wamekuwa wakikiuka utaratibu huu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inazikumbusha Bodi za Afya za Mikoa, Wilaya pamoja na zile za hospitali za Rufaa na Kamati za Afya za Vituo vya kutolea huduma kwamba ni wajibu wao kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi ambao wanapuuza maamuzi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wananchi kutoa taarifa kwa Mamlaka za Wilaya na uongozi wa hospitali husika kuhusu ukiukwaji wa sera ya uchangiaji.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa vile inadhihirika kwamba mamlaka ya Mikoani na Wilaya haiwezi kuwabana hawa wahudumu kwa kuwakosesha tiba au madawa hawa wazee, akina mama wajawazito na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Je, haoni kwamba Serikali inawajibika kutia nguvu zaidi kuhakikisha kwamba matibabu haya yanapatikana bure kama ilivyoainishwa katika hiyo sera?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Serikali inawajibika kuhakikisha kwamba Bodi hizi zinafanya kazi yake ya kuhakikisha kwamba watu waliokuwa na msamaha wa kupata matibabu basi wanapatiwa msamaha huo. Kwa hiyo basi, baada ya kupokea malalamiko mengi Wizara yangu inafanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunarudi tena katika ngazi za Mikoa na Wilaya kutoa elimu kwa Bodi hii, lakini hatimaye mamlaka za nidhamu bado zipo chini ya Bodi hizo. Kwa hiyo, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu na kuhakikisha kwamba utaratibu uliopangwa na Serikali unafuatwa.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa katika baadhi ya Hospitali Teule za Wilaya huwa wanawatoza hao baadhi ya watoto kwa kisingizio kwamba wazazi wao hawakuwapeleka kwenye *clinic,* kwa hiyo, ni lazima wawatoze na wasipolipa fedha wanawarudisha majumbani lakini pia huwatoza wakisema madawa mengine wao wameyanunua. Je, mwongozo wa Serikali au ukweli hapa ukoje kuhusiana na madawa wanayopewa hizi hospitali teule?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, sera ya uchangiaji ipo kwa hospitali zote nchini ambazo ni za umma pamoja na zile hospitali teule. Kwa hiyo, si sahihi kwa hospitali teule kuendelea kuwachaji wagonjwa hawa kwa sababu dawa pamoja na ruzuku nyingi wanapata kutoka Serikalini. Kuhusu madawa hapa ninachotaka kusema ni kwamba Serikali inatoa dawa zote zinazokwenda katika hospitali hizi teule.

Aidha, Serikali imeanzisha utaratibu wa *Drug Revolving Fund* ambapo mtu anapochangia anapopewa dawa analipa nusu ya gharama yake kwa wale ambao hawana msamaha. Aidha, Serikali imeanzisha Mifuko kama Mfuko wa Bima ya Afya ambao unawaingizia hospitali zile fedha kwa madhumuni ya kuweza kupata fedha zaidi za kununulia dawa na kuepusha uhaba. Kwa hivyo, tunachosema ni kwamba bado tunazitaka Bodi za Afya za Wilaya zihakikishe kwamba hakuna hospitali inayowatoza watu ambao kisera wapo katika msamaha.

Na. 7

**Vitendea Kazi Bora kwa Askari Polisi**

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA** aliuliza:-

Kwa kuwa jukumu la kulinda usalama wa raia na mali zao ni la Jeshi la Polisi na kwa kuwa utekelezaji wa majukumu ya jeshi hilo hupitia kwenye vituo vya Polisi

vilivyoko kwenye maeneo mbalimbali ya nchi na kwa kuwa kazi yao inakuwa kubwa na ngumu sana pale wanapokuwa hawana vitendea kazi bora na vya kutosha katika shughuli zao kama vile magari, vifaa vya ofisi, karatasi za kuandikia *statements,* mashine za kutolea nakala na sehemu za kuhifadhi watuhumiwa kabla ya kuwapeleka rumande au Magereza kama ilivyo kwa vituo vingi vilivyopo Dar es Salaam na kwa kuwa ukosefu huu wa vitendea kazi wakati mwingine husababisha raia wajihudumie wenyewe kwa kutoa usafiri kwa Polisi au kujinunulia karatasi ili waweze kuandikiwa *statements:-*

(a) Je, Serikali haioni kwamba usumbufu huo unachelewesha raia kupata huduma na kudhoofisha uwezo na ufanisi wa askari hao wa kufanya kazi zao vizuri na matokeo yake hupewa lawama wasizostahili?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha kasoro hizo ili raia waweze kuhudumiwa ipasavyo na kuwaondolea Polisi lawama zisizo za lazima?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ipo haja ya kuangalia upya Bajeti ya Wizara husika ili kutoa kipaumbele kwa masuala yanayohusu usalama wa raia kwa kutenga fedha za kununulia vitendea kazi ili kuondoa usumbufu na lawama kwa jeshi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakualibana na Mheshimiwa Mbunge kuwa jukumu la kulinda raia na mali zao ni la Jeshi la Polisi lakini bila ya kuondoa wajibu wa raia na wao wenyewe kushiriki katika jukumu hilo.

Nakubaliana pia na Mheshimiwa Mbunge kuwa ukosefu wa vitendea kazi unaweza kuchelewesha raia kupata huduma na kudhoofisha uwezo wa askari Polisi kufanya kazi zao kwa ufanisi. Ni kutokana na kufahamu hivyo ndiyo maana Serikali kupitia Bunge hili Tukufu inajitahidi kadiri inavyowezekana kuongeza bajeti ya Polisi kila mwaka ili Jeshi hili liweze kuwa na vitendea kazi vya kutosha na hivyo kuweza kufanya kazi zake za kuhudumia wananchi kwa ufanisi zaidi. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2001/2002, Serikali ilitenga fedha katika Bajeti yake na kuweza kununua magari mia moja aina ya *Land Rover Defender 110* ambayo yamesaidia sana katika kuboresha kazi za kulinda raia na mali zao.

Katika mwaka wa fedha 2002/2003, kwa kutambua umuhimu wa vitendea kazi, Serikali iliongeza Bajeti ya Jeshi la Polisi kwa asilimia 30 ili iweze kununua vitendea kazi muhimu. Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2003/2004, Bajeti ya Polisi imeongezeka kutoka shilingi bilioni 55/= za mwaka 2002/2003 hadi shilingi bilioni 70/=.

Katika Bajeti hiyo zipo fedha za kutosha kwa ajili ya kununulia mitambo mipya na ya kisasa ya mawasiliano itayorahisisha kazi za Polisi. Serikali kupitia Bunge hili Tukufu itaendelea kuboresha mazingira ya kazi za Jeshi la Polisi mwaka hadi mwaka kwa nia ya kuliwezesha Jeshi la Polisi lifanye kazi kwa ufanisi zaidi kwani Watanzania wanastahili kupata huduma bora kutoka Jeshi la Polisi na bila ya usumbufu wowote.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri bado ningependa kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kuna vituo vya mahabusu ndogo ndogo Vijijini na katika vituo hivi inatokea mara kwa mara kwamba mlalamikaji akimpeleka mgomvi wake inabidi wamwombe awasaidie kumpa chakula na pia wakati mwingine asaidie nauli ili waweze kumsafirisha kumpeleka kwenye kituo kikubwa. Ningependa kufahamu je, ni kazi ya nani kuhudumia mahabusu hawa wanapokuwa Vijijini hadi kupelekwa Mahakamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna vituo pia vya Mahabusu vya kwenye vituo vikubwa vya Polisi. Katika vituo hivi nimeshuhudia kuona kwamba hawakutenganisha kati ya sehemu ya wanawake na wanaume hadi kesho yake wanapopelekwa Mahakamani, nimeshuhudia kuona kwamba wanawake inakuwa kazi hata kwa Polisi inabidi wawalinde mpaka asubuhi na kuna mahali ambapo niliona kwa macho yangu ilibidi Mkuu wa Kituo awachukue wanawake awaweke ndani ya ofisi yake ili kuwanusuru mpaka asubuhi.

Je, Serikali haioni kwamba imefikia hatua ambayo na kutokana na matatizo ya kila siku watenganishe kuwe na kisehemu cha wanawake peke yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tunavyo vituo vingi vya Polisi huko Vijijini ambapo mhalifu akikamatwa anapelekwa katika vituo hivyo na baadhi ya Vijiji mhalifu akikamatwa ambapo hakuna kituo cha Polisi anafungiwa hata katika ofisi za Serikali. Sasa pale mahali ambapo kuna kituo cha Polisi jukumu la kumhudumia yule mahabusu aliyewekwa hapo kwenye kituo hicho ni jukumu la Serikali kimsingi, lakini vituo hivi ni vingi sana, Tanzania hii ni pana sana wakati mwingine Polisi mafungu yao yanakwisha.

Kwa hiyo, nakiri kwamba wakati mwingine inatokea kwamba raia wanaombwa kusaidia na wakati mwingine hata familia yenyewe kwa sababu kituo kipo pale pale Kijijini mwanandugu mwenzao amefungiwa pale hujitolea tu kupeleka chakula pale kwenye kituo, kwa hiyo, kimsingi ni jukumu la Serikali na kwa vile sasa hivi mafungu ya Jeshi la Polisi kila mwaka Bunge hili mnaongeza basi katika sehemu ambapo mafungu yataongezwa ni katika kulisha mahabusu huko walipo, kwa hiyo tatizo hilo litakwisha jinsi bajeti ya Polisi inavyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwaweka pamoja mahabusu wanawake na wanaume kwa kweli huu siyo utaratibu, utaratibu ni kwamba na ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi tunapojenga vituo vidogo popote pale moja ya mahitaji makubwa katika kituo cha Polisi chochote ni mahabusu moja ya wanawake na nyingine ya wanaume. Sasa katika eneo hilo kama hilo lilitokea Mheshimiwa Mbunge tumesikia na tutarekebisha.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa vituo vingi vya Polisi vina uhaba mkubwa wa magari na magari ni nyenzo muhimu sana kwa askari kufuatilia matukio mbalimbali katika eneo lake na hivyo vituo vingi vinavyokosa magari pamoja na kituo cha *Mbamba Bay,* je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza magari ili Polisi waweze kutekeleza majukumu yao vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba usafiri hasa magari ni kitendea kazi muhimu kabisa katika kazi za Jeshi la Polisi na lengo letu kusema kweli kama Bunge hili mtaendelea kutupatia fedha za kutosha kila mwaka kwamba katika kila kituo cha Polisi pale mahali ambapo kuna *OCD* lengo letu tuwe na magari yasiyopungua matatu katika kila Kituo cha Polisi cha Wilaya kwa maana moja la *OCD,* moja la Mkuu wa Kituo na moja la Afisa wa Upelelezi. Mpaka sasa hali ilivyo katika Wilaya zetu nyingi, asilimia 60 ya Wilaya zetu kuna magari mawili kwa maana la *OCD* na la Mkuu wa Upelelezi na asilimia arobaini ya Wilaya zetu bado kuna gari moja tu.

Kwa hiyo, lengo kwanza tumalize zile asilimia 40 za Wilaya ambazo hazina magari, tukimaliza hapo sasa ndipo twende kwenye vituo vingine vya kati kama kile cha *Mbamba Bay.* Kwa hiyo, naomba subira tumalize kwanza hizi Wilaya baada ya hapo ndiyo tutakwenda katika vituo vingine vya kati kama vya Mbamba Bay na vingine katika Makao Makuu ya Tarafa.

Na. 8

**Kesi Zilizofanyika Pemba**

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa makosa makubwa dhidi ya jamii yamekuwa yakitendeka kwa kasi kubwa sana hapa nchini na kwa mujibu wa hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka 2003/2004, katika kitabu chake ukurasa wa 42 jedwali la 1(c) idadi ya kesi za aina hiyo kwa kipindi cha Januari-Desemba 2002 zilikuwa 10,446 zikiwemo kesi 317 kutoka Mikoa ya Tanzania Zanzibar:-

(a) Je, Serikali inaweza ikatueleza ni kesi ngapi za aina hiyo zilizofanyika katika Mikoa ya Pemba kwa kipindi hicho cha Januari-Desemba, 2002?

(b) Je, ni Mkoa gani unaoongoza kwa kesi za aina hiyo huko Tanzania Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa idadi ya kesi za makosa makubwa dhidi ya jamii zilizofanyika katika kipindi cha Januari - Desemba, 2002 zilikuwa 10,446 nchini kote, zikiwemo 317 kutoka Mikoa ya Tanzania Zanzibar.

Idadi ya kesi za makosa makubwa yaliyotendeka dhidi ya jamii katika Mikoa ya Pemba kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2002 ni 37 ambapo makosa 19 yalitendeka Mkoa wa Kaskazini Pemba na 18 yalitendeka Mkoa wa Kusini Pemba. Aidha, Mkoa unaoongoza kwa kesi za aina hiyo kwa upande wa Tanzania Zanzibar ni Mkoa wa Mjini Magharibi ambao katika kipindi hicho walikuwa na makosa makubwa 215 sawa na asilimia sitini na saba ya makosa yote yaliyotendeka katika Mikoa ya Tanzania Zanzibar.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Moja, je kutokana na makosa hayo kidogo kuna haja ya kuweka askari wengi sana kule Pemba?

Pili, je, Serikali inayo mikakati gani ya kupunguza au kutokomeza kabisa makosa ya aina hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, sina hakika kwamba kauli ya Mheshimiwa Mbunge ni sawasawa kwamba Pemba tumepeleka askari wengi sana kupita mahitaji. Kwa sababu Jeshi la Polisi hupeleka askari mahali kulingana na uzito wa kazi uliopo pale. Kwa hiyo, idadi ya askari Polisi waliopo Pemba nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge wanatosheleza kabisa na kiwango cha hali ya uhalifu uliopo katika Mkoa wa Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupunguza makosa ya jinai katika nchi yetu amesema tuna mikakati gani. Mkakati wa kwanza kabisa ni kushirikisha tu wananchi kila mahali walipo pamoja ndugu zangu Wapemba washiriki katika kulinda maeneo yao, mali zao na maisha yao.

Kwa upande wa Pemba sasa hivi baada ya muafaka tukapata ushirikiano mkubwa sana na tunaomba tuendelee kupata ushirikiano huo ndiyo maana makosa yamepungua kule Pemba, zamani makosa yalikuwa mengi hayakuwa haya 19. Vile vile kwa Tanzania Bara bado tunaomba ushirikiano wa wananchi, vikundi vya Sungusungu na Jeshi la Polisi kupitia Bunge hili tunaendelea kuwapa zana na vitendea kazi vya kutosha kufanya kazi.

Kwa mikakati hii ya pamoja ya Polisi kupewa vitendea kazi na wananchi kutoa ushirikiano tuna hakika tunaweza kupunguza wimbi hili la uhalifu unaoikumba nchi yetu pamoja na eneo la Pemba.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge pengine wageni ninaotaka kuwatambulisha hawatakaa mpaka mwisho wa maswali bora niwatambulishe sasa. Tunao ushirikiano wa

mradi wa kuimarisha huduma za Bunge unaofadhiliwa na *USAID*. Sasa ni mchanganyiko wa Balozi zaidi ya moja zilizoko Dar es Salaam, sasa nitakaowatambulisha sasa wamekuja kuzungumza na sisi juu ya mradi huo wa kuimarisha huduma za Bunge na wanatoka Ubalozi wa Uingereza ambao wapo kwenye *Gallery* sasa hivi. *(Makofi)*

Tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Na. 9

**Mradi wa Kupeleka Maji ya Ziwa Victoria, Shinyanga na Kahama**

**MHE. TEMBE K. NYABURI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeazimia kujenga bomba kubwa la kupeleka maji ya Ziwa Victoria, Shinyanga na Kahama na kwa kuwa ipo Miji iliyoko umbali wa kilomita kumi na tano kandokando ya Ziwa hilo na haina maji kama vile Bunda:-

(a) Je, Serikali na mpango gani wa kusambaza maji ya uhakika kwa Miji iliyo kandokando ya Ziwa kama ile ya Bunda, Magu, Sengerema, Geita na kadhalika?

(b) Kwa kuwa Serikali sasa imeanzisha Bodi za Maji za Miji ya Mikoa na Wilaya lakini Bodi hizo hazina fedha za kutosha je, Serikali ina mpango gani wa kuzisaidia Bodi hizo?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tembe Kerenge Nyaburi, Mbunge wa Bunda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ziwa Victoria limekuwa linatumika kama chanzo cha maji kwa ajili ya Miji iliyoko kandokando yake kwa muda mrefu hata kabla ya kuanzishwa mradi wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria kwenye Miji ya Shinyanga na Kahama. Miji iliyoko kandokando ya Ziwa imekuwa ikitumia chanzo hiki kwa muda mrefu sasa na Miji hiyo ni pamoja na ile ya Musoma, Mwanza, Bukoba, Bunda, Magu na Sengerema. Miundombinu ya usambazaji wa huduma ya maji katika Miji hii ni ya siku nyingi na kwa hiyo haikidhi mahitaji ipasavyo kwa sababu ya uchakavu au uwezo mdogo kwa kuwa Miji imepanuka kuzidi uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuendelea kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu ina mipango ya kusaidia Miji iliyoko kandokando ya Ziwa kama ifuatavyo:-

- Kukarabati mradi wa maji wa Mji wa Mwanza kwa msaada wa *EU* na Serikali ya Ujerumani kupitia shirika lake la

maendeleo la *KfW*. Hadi sasa *EU/KfW* wametenga *EURO* milioni 38 kwa ajili ya Mji wa Mwanza peke yake.

- Kufanya uchunguzi kwa ajili ya ukarabati wa miradi ya maji kwa Miji ya Musoma, Bukoba na Misungwi kwa msaada wa Serikali ya Ufaransa *(AFD)* kwa gharamaya *EURO* milioni 162,000. Mradi huo upo kwenye hatua za kuajiri Mhandisi Mshauri.

- Miradi ya Magu na Sengerema imefanyiwa ukarabati mkubwa mwaka 2001/2002 kwa msaada wa Serikali ya Sweden kupitia *HESAWA*. Hata hivyo Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kupanua mtandao wa kusambaza maji katika Miji hii miwili.

Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Serikali ilinunua mabomba kwa ajili ya kukarabati mradi wa maji wa Mjini Bunda. Mabomba yanatarajiwa kulazwa kutoka Guta hadi kwenye matanki ya kuhifadhi maji. Kazi ya kulaza mabomba inatarajiwa kufanywa na Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na Mradi wa Maendeleo ya Wilaya *(DPP)* unaofadhiliwa na Serikali ya Sweden *(SIDA)*. Mazungumzo kati ya Halmashauri ya Wilaya na uongozi wa Mradi wa Maendeleo ya Wilaya *(DPP)* yanaendelea. Ukarabati wa mradi huu unatarajiwa kugharimu shilingi milioni 94.

(b) Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Maji ambazo zimeanzishwa kwenye Miji Mikuu ya Mikoa na Wilaya zimepewa mamlaka ya kukusanya mapato na kuyatumia kwa ajili ya kuendesha shughuli za maji. Aidha, Serikali bado inazipatia ruzuku baadhi ya mamlaka za Miji Mikuu ya Mikoa na zile za Miji Mikuu ya Wilaya zote kwa ajili ya kulipia umeme, mishahara ya watumishi wake na madawa ya kutibu maji ili kujiimarisha kiuendeshaji.

Mamlaka zilizoko kwenye Miji Mikuu ya Mikoa hupata fedha kupitia Wizara yangu na zile za Miji Mikuu ya Wilaya hupata fedha hizo kupitia Halmashauri husika. Lengo la Serikali ni kuziwezesha mamlaka hizi zijitegemee katika uendeshaji wa miradi yao ya maji. Serikali pia hutoa vitendea kazi, mafunzo na ushauri kwa ajili ya kuimarisha mamlaka hizi.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Katika swali la msingi Mheshimiwa Nyaburi aliulizia kuhusu Wilaya ya Geita na Mheshimiwa Waziri inaonekana katika maelezo yake Wilaya ya Geita imesahaulika na inaonekana haipo katika mpango, je, Serikali haioni kwamba Wilaya ya Geita ipo karibu na Ziwa Victoria na ina miradi ambayo imekaa muda mrefu haifanyiwi kazi?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, tunatambua tatizo la Geita na yeye mwenyewe ni shahidi kwamba tumekuwa tunashughulikia kuchimba visima na kusaidia wananchi wa Geita. Kadri tutakavyopata

fedha zaidi tutaendelea kuisaidia Wilaya ya Geita kama tunavyofanya katika Wilaya nyingine.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Baadhi ya Bodi za Maji Mikoani hutoza bei kubwa ya maji kwa wateja kwa misingi tu ya kuweka Bajeti zao vizuri kwa matumizi ya Kimkoa na hiyo inawapa kero watumiaji wa maji. Je, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo ana mpango gani wa kuweza kurekebisha hali hii ili tusiwe na bughudha na wananchi Mkoani na Wilayani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya hakunitajia ni mamlaka gani ambayo inatoza maji hayo kwa bei kubwa, lakini nataka niamini kwamba labda anaisemea mamlaka ya Mji wa Shinyanga ningependa kuliarifu Bunge hili kwamba Mamlaka ya Shinyanga sasa inafanya kazi nzuri sana, imeongeza mapato yake kutoka milioni 18 mpaka milioni 65 katika muda wa miezi mitatu tu kwa sababu ya kazi nzuri wanayofanya ya kuongeza ajira na watu wanalipa.

Tatizo lililopo nchini ni kwamba ipo asilimia kubwa ya watu wanaotaka kufikiri kwamba maji yatatolewa bure, bure hakuna, bure alikufa mwaka juzi, maji lazima yalipiwe.

Na. 10

**Viwanda vya Kusindika Mazao ya Mifugo**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR (k.n.y. MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR)** aliuliza:-

Kwa kuwa mifugo ni muhimu sana kwa kukuza uchumi wa nchi na lishe bora na kwa kuwa viongozi waliotangulia waliona umuhimu wa kuendeleza mifugo hiyo kwa kujenga viwanda mbalimbali kama vile Kiwanda cha Kuweka Maziwa kwenye paketi, Kiwanda cha Kusindika Nyama ya Ng’ombe kwenye makopo, Kiwanda cha Kutengeneza Ngozi na kadhalika na kwa kuwa bidhaa hizo ziliuzwa ndani na nje ya nchi lakini viwanda hivyo sasa ama havifanyi kazi au vinafanya kazi kwa kiwango kidogo sana kiasi cha kufanya mazao hayo kukosa soko endelevu na la uhakika.

Je, Serikali inaweza kutueleza mipango iliyo nayo ya kufidia au kufufua soko hilo ili kuinua uchumi wa wafugaji pamoja na Taifa kwa ujumla?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mbunge wa Mikunguni, naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya sera za jumla ambayo yalilenga kurekebisha uchumi wa nchi yetu, viwanda vingi vikiwemo vya kusindika maziwa, nyama, ngozi pamoja na viwanda vingine vya bidhaa zitokanazo na mifugo vilibinafsishwa.

Kwa sasa usindikaji wa mazao ya mifugo yakiwemo maziwa, ngozi na nyama hufanywa na sekta binafsi ambapo kuna viwanda 17 vya kusindika maziwa vyenye uwezo wa kusindika lita 150,000 kwa siku. Vile vile kuna viwanda vitano vya kusindika ngozi na viwanda saba vya kusindika nyama.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mbunge wa Jimbo la Mikunguni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mipango ya kuongeza usindikaji wa mazao yatokanayo na mifugo kwa lengo la kufufua viwanda vya ndani na kupanua masoko ya bidhaa hizo ndani na nje ya nchi ili kuinua uchumi wa wafugaji. Baadhi ya mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Wizara yangu inahamasisha sekta binafsi kuwekeza na kuanzisha viwanda vidogo na vya kati vya kusindika nyama na bidhaa zitokanazo na maziwa na ngozi ili kuongeza thamani ya bidhaa hizo na hivyo kufufua soko.

(ii) Wizara yangu inajenga machinjio ya kisasa pamoja na chuo cha kukata na kusindika nyama hapa Dodoma kama mkakati wa kuongeza ubora wa nyama inayochinjwa kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi.

(iii) Wizara yangu imeanzisha Maadhimisho ya Wiki ya Maziwa ili kuhamasisha unywaji wa maziwa nchini na hivyo kuongeza soko la maziwa la ndani na lishe kwa wananchi. Unywaji wa maziwa kwa Mtanzania kwa mwaka ni wastani wa lita 30 wakati viwango vinavyopendekezwa na Shirika la Chakula Duniani *(FAO)* ni lita 200.

(iv) Wizara yangu ikishirikiana na wadau wa sekta ya Mifugo inahamasisha uanzishaji wa Bodi ya Maziwa na Bodi ya Nyama. Bodi hizi za wadau zinaratibu maendeleo ya sekta hizo na kudhibiti ubora wa mazao yatokanayo na mifugo.

(v) Serikali imeweka kodi ya asilimia 20 kwa ngozi zote ghafi zinazouzwa nje ili kupunguza mauzo ya ngozi ambazo hazijasindikwa badala ya kuongeza usindikaji wa ndani ambao utaongeza thamani ya ngozi zinazouzwa nje.

(vi) Serikali imeweka kodi ya nyongeza *(Suspended Duty)* ya asilimia 20, *VAT* asilimia 20 na kodi ya kuingiza *(Import Duty)* ya asilimia 15 kwa maziwa na mazao yake yanayoingizwa nchini ili kulinda bidhaa za maziwa zinazosindikwa hapa nchini. Aidha, Serikali imeondoa kodi ya vifungashio

*(packaging)* ili kuongeza ushindani kati ya maziwa yanayosindikwa nchini na yanayotoka nje.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na juhudi zake za kufufua soko la ndani na nje kwa kuhimiza usindikaji wa maziwa, nyama, ngozi pamoja na viwanda vingine vya bidhaa zitokanazo na mifugo. Hali hii itaongeza thamani ya bidhaa zitokanazo na mifugo na kupanua soko la bidhaa zilizosindikwa ili kuinua uchumi wa Taifa pamoja na kipato cha wafugaji nchini.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali ndogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ambayo yana matumaini kwa Watanzania, napenda kumuuliza kuwa kama kuna mkakati wa Watanzania kunywa maziwa, je, mkakati huo umefanikiwa kwa kiasi gani kwa Watanzania hivi sasa? Katika viwanda vyote vilivyoko Tanzania vinaonekana vyote viko katika Miji Mikuu je, wananchi wa vijijini wanafaidikaje na mikakati hii ya kunywa maziwa?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ingawa ni kweli viwanda vingi vya maziwa viko mijini, lakini maziwa hayo hutengenezwa na kupelekwa vijijini. Tatizo tulilonalo nchini ni kwamba ule utashi wa kunywa maziwa kiwango chetu ni kidogo. Ukienda mahali kama Uholanzi, asubuhi unakunywa chai, kuna glasi kubwa ya maziwa, mchana unapokula chakula, kuna glasi kubwa ya maziwa, usiku unapokula chakula, kuna glasi kubwa ya maziwa, Watanzania wengine bado hatujajenga utamaduni huo. Lazima tupanue soko la ndani ndipo tutakapoimarisha sekta ya mifugo.

Na. 11

**Ujenzi wa Nyumba Bora kwa Gharama Nafuu**

**MHE. ROBERT J. BUZUKA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa vijiji vya Kata za Pandagichiza, Solwa na Iselamagazi; Mwantini na Mikitolyo wamejiunga katika vikundi vya ujenzi wa nyumba bora kwa gharama nafuu.

Je, Serikali iko tayari kutoa mafunzo ya Ujenzi wa Nyumba Bora na za gharama nafuu kwa wananchi katika Kata hizo ili nao waweze kutoa elimu hiyo kwa wananchi wengine kwa lengo la kuboresha makazi yao?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Robert Jacob Buzuka, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza wananchi wa vijiji vya Kata za Pandagichiza, Solwa, Iselamagazi, Mwantini na Mwakitolyo kwa kujiunga katika vikundi vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa kushirikiana na viongozi wao.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara yangu, kupitia Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi, ni pamoja na :-

- Kufanya utafiti wa vifaa bora na ufundi wa ujenzi kwa lengo la kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba nchini;

- Kutoa ushauri, usanifu, ukadiriaji wa gharama na usimamizi wa ujenzi wa nyumba;

- Kusambaza matokeo ya utafiti na utaalamu wa ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu nchini; na

- Kuendesha mafunzo ya vitendo na semina za uhamasishaji kuhusu ujenzi wa nyumba za gharama nafuu zinazotumia maliasili ya maeneo ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikitekeleza majukumu hayo Mikoani baada ya kufanya mawasiliano na Mikoa iliyotayari kupokea huduma hizo, ukiwemo Mkoa wa Shinyanga mmojawapo.

Tarehe 31 Oktoba, 2003, Wizara ilipeleka wataalamu wake Mkoani Shinyanga kwenda kuona uwezekano wa kuweka utaratibu wa kutoa elimu ya mafunzo ya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu hususan katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini ambapo tumepata mwaliko kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo. Serikali iko tayari kutoa mafunzo ya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu katika Kata za Pandagichiza, Iselamagazi, Mwantini, Makitolyo na Solwa kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali ndogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa Serikali tayari kama alivyojibu imetekeleza wito wetu na kwamba watalaamu wako tayari kule Shinyanga. Je, Serikali inaonaje kuweka kituo cha kudumu cha utafiti wa nyumba hizo bora na za gharama nafuu katika Mkoa wa Shinyanga ikizingatiwa kwamba wakazi wa Mkoa wa Shinyanga wana utajiri mkubwa sana, lakini makazi hayawiani kwa kweli na hali halisi ilivyo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna umuhimu wa kuweka kituo katika Mkoa wa Shinyanga, lakini kitengo hiki ni miaka miwili tu ambapo kimeimarishwa, na haitakuwa

rahisi kwa wataalamu wetu walio wachache kwenda kuweka vituo katika Mikoa yote, kwa sababu tukianza katika Mkoa wa Shinyanga, kila Mkoa utahitaji. Lakini ninachosema ni kwamba sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwahamasisha wananchi wetu kuhusu ujenzi wa nyumba bora. Kwa sababu kuwa na wananchi wenye afya na ndiyo matumaini yetu ya wapiga kura.

Kwa hiyo, hili suala si la utafiti tu katika kitengo hiki cha utafiti bali sisi wenyewe tujumuike na wanasiasa na watendaji walioko katika Wilaya ili waweze kuwahamasisha wananchi ujenzi wa nyumba bora.

Na. 12

**Sheria ambazo si za Muungano**

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni nchi moja yenye Serikali mbili yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, zenye mamlaka kamili na hutaja mambo yanayohusu Muungano na yale yasiyokuwa ya Muungano; na kwa kuwa ziko Sheria zinazotungwa na kutakiwa kutumika Tanzania nzima wakati hazikutajwa katika mambo ya Muungano.

(a) Je, ni sheria ngapi kama hizo ambazo tayari zimekwishatungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

(b) Je, ni taratibu gani zinatumika katika kuzitunga sheria kama hizo kwa pande zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar?

(c) Je, kuna matatizo gani ya kiutekelezaji wa sheria kama hizo ambayo yamewahi kujitokeza?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, hakutaja sheria anazozizungumzia ni za kuanzia lini, lakini kati ya mwaka 1990 na 2003 sheria zilizotungwa na kutakiwa kutumika Tanzania nzima wakati hazikutajwa katika mambo ya Muungano ni tano.

(b) Katiba ya Nchi katika Ibara ya 64(4) imeainisha masharti ambayo sheria yoyote iliyotungwa na Bunge inatakiwa kutimiza kabla ya kutumika Tanzania Zanzibar. Taratibu zinazotumika katika kutunga Sheria kama hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mapendekezo hutolewa kwa kupitia Waraka wa Serikali kuhusu Sheria inayohusika, baada ya kuwashirikisha wadau mbalimbali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar;

(ii) Baraza la Mawaziri hujadili Waraka huo na kutoa maoni na kutoa kibali cha kuchapishwa Muswada;

(iii) Muswada huwasilishwa kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya kwanza;

(iv) Wadau mbalimbali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar hupata fursa ya kutoa maoni yao;

(v) Bunge la Jamhuri ya Muungano hujadili Muswada ambao umechangiwa pia na wadau na kuupitisha kama Sheria; na

(vi) Sheria hiyo huanza kufanya kazi baada ya kupata ridhaa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(c) Katika utekelezaji wa mambo ya utendaji wa Sheria hizi kumejitokeza matatizo kama ilivyo katika shughuli nyingine za utendaji.

Aidha, ili sheria iliyotungwa na Bunge iweze kutumika Tanzania Zanzibar lipo sharti lililowekwa na Ibara ya 132(2) ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, la kupelekwa kwa Sheria hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi kwanza.

Baadhi ya matatizo ya utekelezaji wa sheria hizi yamekwishawasilishwa kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi na yanashaghulikiwa kwa shabaha ya kuondoa kasoro hizo.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ikiwa kama itajitokeza kesi upande mmoja wa Zanzibar ambayo sheria yake haikutungwa na Serikali ya Muungano na ikabidi kwamba mshitaki au mshitakiwa anataka rufaa ya Mahakama Kuu. Je, katika kipengele hiki ni taratibu gani ambazo hutumika ndipo haki hiyo au utaratibu huo wa kufanya hivyo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano Mtanzania na kwa maana hiyo akiwepo kwa maana pana Mzanzibari wote ni Watanzania, kama anataka kukata rufaa kwa suala lolote atafanya kwa taratibu zilizopo.

Lakini kupinga uamuzi au kuhoji uamuzi uliotolewa na Mahakama Kuu ya Zanzibar kwenda kwenye Mahakama ya Rufani isipokuwa tu kwa suala moja, kesi ambazo zimetokana na maamuzi ya Mahakama ya Kadhi na sasa hivi hizo haziwezi kwenda moja kwa moja kwenye Mahakama ya Rufani.

**MHE. ISSA MOHAMMED SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ingawa mwuliza swali hakutaja kesi ambayo imeleta utatanishi katika utekelezaji.

Lakini kuna Sheria ya Uvuvi ya Bahari Kuu ambayo imeleta matatizo Zanzibar na Zanzibar wamekuwa wanatoa leseni kinyume na sheria iliyotungwa na Bunge. Je, katika sheria ambazo zitaangaliwa upya na hiyo ipo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli yapo matatizo machache katika utendaji wa Muungano, likiwemo na eneo hili la utoaji wa leseni katika shughuli za uvuvi wa Bahari Kuu yaani *Deep Sea Fishing.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, shughuli ya *Deep Sea Fishing* siyo jambo la Muungano, linashughulikiwa pia na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika sasa katika kuangalia sheria hizi ambazo zina matatizo ni kuona jinsi gani Wizara zinazohusika zinaweza zikashirikiana katika suala zima la utoaji leseni ili tuweze kuvuna raslimali iliyomo katika Bahari Kuu kwa manufaa ya wananchi wetu wote.

Na. 13

**Watuhumiwa wa Kesi mbalimbali**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi watuhumiwa wa kesi mbalimbali wanapopelekwa Mahakamani Mahakimu huwa wanajali sana maombi ya Mwendesha Mashtaka wa Polisi *(PP)* ya kutowapa dhamana watuhumiwa kuliko kuangalia hali halisi ya kesi ilivyo na kusababisha kuwaweka watuhumiwa rumande kwa kipindi kirefu, kwa mfano, kama mtuhumiwa kesi yake ikitajwa humwomba Hakimu au Jaji arudishwe tena mtuhumiwa rumande wiki mbili na muda huo ukiisha huomba tena arudishwe huko kwa madai kwamba ataharibu ushahidi, lakini baada ya muda mrefu hatimaye kesi humalizika bila ushahidi na mtuhumiwa akiwa hana kosa:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuweka mtu rumande kwa muda mrefu kwa makosa ambayo hawana uhakika nayo na hatimaye wakakosa ushahidi ni kukiuka haki za binadamu?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwadhibiti waendesha mashitaka wenye tabia kama hizo?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamisi Juma, Mbunge wa Micheweni, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo mafupi ya jumla kama ifuatavyo:-

Kwa utaratibu wa sheria, wakati wowote Polisi inapopata taarifa ya uhalifu inafanya uchunguzi wa kumkamata mtuhumiwa na kama wataridhika kwamba upo ushahidi wa msingi wa kumhusisha na uhalifu uliotokea ndipo Polisi humfikisha Mahakamani, wakati upelelezi unaendelea. Upelelezi unapokamilika ndipo inaweza kuonekana kama upo ushahidi wa kutosha kuendelea na shitaka dhidi ya mtuhumiwa au la. Hata hivyo, mtuhumiwa husika kama atakuwa amewekwa rumande basi ana haki ya kuomba dhamana ambayo itafikiriwa na Mahakama kwa kuzingatia sheria ya utaratibu wa uendeshaji wa Mashtaka ya Jinai.

Hakimu au Jaji, kama mtoa haki, ana wajibu wa kusikiliza hoja za mtuhumiwa anayeomba dhamana na hoja za Mwendesha Mashitaka. Kwa upande mwingine Mwendesha Mashitaka anayo haki ya kupinga kutolewa dhamana kwa mtuhumiwa kwa kutoa sababu za msingi za kupinga ombi hilo.

Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamisi Juma, kama ifuatavyo:-

(a) Kwa vile baadhi ya watuhumiwa wanapelekwa Mahakamani wakati upelelezi unaendelea, inakuwa vigumu kwa Waendesha Mashtaka kuthibitisha kama shauri lina ushahidi wa kutosha au la; hata hivyo wakati huo Polisi wanakuwa na ushahidi wa awali wa kiwango cha kuwafanya waridhike kwamba mtuhumiwa ana wajibu wa kujibu shtaka linalomkabili. Kwa sababu hiyo na kwa kuzingatia maelezo niliyokwishayatoa hapo awali, hatua hii haiwezi kuchukuliwa kuwa ni ukiukwaji wa Haki za Binadamu.

(b) Serikali inaweza kuwadhibiti Waendesha Mashtaka kama itathibitika wamekiuka taratibu zao za kazi. Aidha, kama mtuhumiwa akiona amewekwa rumande bila uhalali wowote wa kisheria anaweza kutuma malalamiko yake kwa Mkurugenzi wa Mashitaka ambaye kama ataridhika ni ya msingi basi ataagiza mashitaka yanayomkabili yafutwe na hivyo kumfanya mtuhumiwa awe huru.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza. Je, kuna sababu zipi za msingi zinazomsababisha Hakimu atoe ruksa kwa mtuhumiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge hujakamilisha swali lako.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Je, kuna sababu zipi za msingi zinazomsababisha Hakimu aweze kutoa dhamana kwa mtuhumiwa?

**SPIKA:** Sababu za msingi za kutoa dhamana.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, Hakimu ama Jaji anaweza kutoa dhamana. Kwanza, ana uhakika kwamba mtuhumiwa atakuja katika shauri atakapoitwa. La pili, ni kwamba Hakimu ama Jaji aridhike kwamba akimwachia mtuhumiwa hatarudia kosa lile wakati atakapokuwa nje. La tatu, ni kwamba Hakimu au Jaji ajiridhishe kwamba mtuhumiwa ataingilia shughuli za upelelezi wakati atakapokuwa nje. Hakimu au Jaji ajiridhishe kwamba kutokana na ukubwa wa kesi yenyewe ama adhabu kwamba akipatikana huyu na tuhuma ya kuadhibiwa, kama adhabu ni kubwa basi apime kwamba huyu mtuhumiwa anaweza kutoroka au ku- *jump the bail* haya ndiyo masharti yenyewe. *(Kicheko)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa suala la watu kukaa rumande siyo wanawasumbua hao watu wenyewe, lakini pia ni mzigo kwa Serikali wa kuwalisha. Je, Serikali haioni umefika wakati wa kuweka muda maalum wa watu kukaa rumande hasa kwa makosa ya kawaida kuliko kila siku kutohukumiwa wakawa wanarudishwa ndani na matokeo yake ikawa ni mzigo kwa wao wenyewe na kwa Serikali?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba kwa nyakati nyingine hivi vyombo vyetu vinavyohusika na utoaji haki, havizingatii sheria au taratibu mbalimbali.

Kwanza, niseme kwamba dhamana *is the right, is not a privilege, it is a right.* Kwa hiyo, watuhumiwa hawa wote kwa kweli inabidi wapate hiyo dhamana aidha kutoka kwa Polisi ama kwenye Mahakama. Kama watakuwa wako rumande na Polisi wanasema kwamba upelelezi unaendelea, unaendelea, Hakimu anao uwezo baada ya siku 60 kumtoa mtuhumiwa katika rumande. Lakini unakuta wakati mwingine masharti haya hayafuatwi kwa masuala ambayo ni *available.* Kwa hiyo, nakubaliana na wewe.

Na. 14

**Kiwanda cha *MWATEX***

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati Kiwanda cha *MWATEX* kilipokuwa kinazalisha kabla ya kubinafsishwa baadhi ya Vyama vya Ushirika kama vile *NCU (1984) LTD, SHIRECU (1984) LTD* vilikuwa na hisa katika Kiwanda hicho; na kwa kuwa baadhi ya Vyama kama vile *SHIRECU, NYANZA, BCU, BUHA, MARA CO OPERATIVE, SIRECU* pia

vilikuwa na hisa kwenye Kampuni ya *Pamba Engineering LTD (PEL)* kabla ya kuuzwa kwa Kampuni hiyo:-

(a) Je, vile Vyama vilivyokuwa na hisa *MWATEX* vinaendelea kumiliki hisa zao hata baada ya Kiwanda kubinafsishwa?

(b) Je, Vyama vilivyokuwa na hisa kwenye *Pamba Engineering LTD (PEL)* vinaendelea kumiliki hisa zao huko?

(c) Kama Vyama hivyo havikumilikishwa hisa, je, vimelipwa hisa zake na ni kiasi gani cha fedha?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Ni kweli kwamba baadhi ya Vyama vikuu vya Ushirika kikiwemo *SHIRECU* na *NYANZA,* vilikuwa vinamiliki hisa katika kiwanda cha *MWATEX* na Kampuni ya *Pamba Engineering Ltd* kabla havijabinafsishwa. Kumbukumbu za Vyama hivyo zinazoonyesha kuwa *SHIRECU* ilikuwa inamiliki hisa zenye thamani ya shilingi 3,166,000/= na *NYANZA* ilimiliki hisa zenye thamani ya shilingi 3,793,000 katika Kiwanda cha *MWATEX.*

Aidha, *SHIRECU* ilimiliki hisa zenye thamani ya shilingi 6,250,000/= na *NYANZA* ilimiliki hisa zenye thamani ya shilingi 30,000,000/= katika Kiwanda cha *Pamba Engineering.*

Hivi sasa Viwanda vya *MWATEX* na *Pamba Engineering* vimeuzwa na *LART* kwa utaratibu wa ufilisi ambapo kwa mujibu wa sheria, ufilisi unapokamilika ulipaji wa Dhima yaani *Liabilities* ya Kampuni iliyofilisika huanza kwa kulipa madai ya sheria yaani *Statutory Creditors,* halafu hufuatia wadai wenye dhamana yaani *Secured Creditors* na wadai wengine na mwisho kabisa humalizia wenye hisa yaani *shareholders.*

Ninaamini kwamba Mheshimiwa Mbunge, pamoja na viongozi wote wa Vyama vya Ushirika wanaufahamu vizuri utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi sasa ufilisi wa Kampuni za *MWATEX* na *Pamba Engineering* bado haujafika mwisho na kwa hali hiyo hatma ya hisa za *SHIRECU,*

*NYANZA* na wanahisa wengine itafahamika mara ufilisi utakapokuwa umekamilika na mikutano ya wanahisa wote kuitishwa ili wafahamishwe hatma ya hisa zao.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema kwamba shughuli ya mfilisi bado inaendelea ni lini hasa itakamilika shughuli hiyo ili Vyama vya Ushirika viweze kupata haki yake?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwamba Kampuni hizi za *MWATEX* pamoja na *Mwanza Engineering* zinafanyiwa ufilisi kwa utaratibu wa *LART* na kazi ambayo imeshafanyika sasa hivi ni kuuza mali za vyombo hivi.

Kwa hiyo, sasa taratibu zingine zinazofuata ni kukamilisha mahesabu na kuweza kujua sasa wadai wanaweza wakalipwa kwa utaratibu gani. Kwa hiyo, kusema ni muda gani ni mpaka hapo hesabu zitakapokuwa zimekamilika za kuandaa utaratibu wa malipo ya wahusika wote.

Na. 15

**Ushirika wa Mifugo na Masoko ya Mazao ya Mifugo**

**MHE. LEKULE M. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa tangu Wizara ya Ushirika na Masoko iundwe imekuwa ikijishughulisha sana na masoko ya mazao ya kilimo tu na kuacha masoko kwa mazao yanayotokana na mifugo:-

(a) Je, Mazao ya Nyama, Maziwa, Ngozi, Siagi na kadhalika hayauziki na Wizara ya Ushirika na Masoko?

(b) Je, isingekuwa busara kwa Serikali kuanzisha Ushirika wa Wafugaji kama wanavyoelimisha na kusaidia Ushirika wa wakulima wa kahawa, pamba, korosho, mkonge na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba tangu Wizara ya Ushirika na Masoko ilipoundwa imekuwa ikijishughulisha sana na masoko ya mzao ya kilimo tu na kuacha masoko ya mazao yatokanayo na mifugo. Ukweli ni kwamba, Wizara imekuwa ikishughulikia masoko ya

mazao yote bila kubagua. Aidha, ili kuwezeha mazao yoyote yanayozalishwa kuingia katika soko, Wizara yangu inafanya mambo yafuatayo:-

- Kutoa taarifa za bei, viwango vya ubora na madaraja ya mazao kwa ajili ya kuwawezesha wafugaji na wakulima kuingia katika soko.

- Kuwaunganisha wazalishaji wadogo kupitia Vyama vyao vya Ushirika na taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo ya kufanyia biashara; na

- Kusimmamia sera na kanuni za ushindani wa haki katika soko.

Mheshimiwa Spika, kama nilieleza katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2003/2004, Sekta ya mifugo na mazao yake bado inategemea kwa kiasi kikubwa soko la ndani kutokana na mifugo yetu pamoja na mazao yake kutokidhi viwango vya kimataifa. Aidha, magonjwa ya mifugo katika Ukanda huu yanazuia usafirishaji na uuzaji kwa wingi mifugo na bidhaa zake katika masoko ya Kimataifa.

Hata hivyo kuwekuwepo na ongezeko la uzalishaji na mazao ya nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku kwa asilimia 2.6 mwaka 2002/2003 ikilinganishwa na msimu wa 2001/2002. Uzalishaji na mauzo ya mayai uliongezeka kwa asilimia 21.5 na uzalishaji na mauzo ya maziwa katika soko la ndani uliongezeka kutoka lita milioni 900 hadi lita milioni 980. Hivyo hivyo kwa zao la ngozi, mwaka 2002/2003 kulikuwa na ongezeko la asilimia 17 la mauzo ya ngozi nje ya nchi ikilinganishwa na kipindi cha 2001/2002.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inahimiza sana uanzishaji wa Vyama vya Ushrika wa aina mbalimbali ukiwemo Ushirika wa wafugaji pote nchini. Azma hii imeelezwa kina katka hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2003/2004 kuhusu hatua mbalimbali zilizochukuliwa, pamoja na malengo tuliyojiwekea katika kuhakikisha kwamba wananchi wanajiunga pamoja na kuanzisha Vyama vya Ushirika kama njia bora ya kuondokana na umaskini. Takwimu zilizomo katika Jedwali Na. 1 ya kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu ni kielelezo kamili cha ukuaji wa sekta ya Ushirika kwa ujumla hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ushirika wa ufugaji, mwaka 2002 vilikuwepo Vyama vya Ushirika vya Wafugaji vipatavyo 70, ambapo hadi Mei, 2003, idadi hiyo iliongezeka na kufikia 95. Mikoa inayoongoza kwa wingi wa Vyama vya Wafugaji ni Kagera wenye vyama 27, Mbeya vyama 22, Shinyanga vyama 15, Arusha vyama 11, Tanga vyama 9 na Kilimanjaro vyama 5. Vyama vya Mkoa wa Tanga vimeonyeshwa kustawi zaidi na kufanikiwa katika kuuza maziwa na mazao yatokanayo na maziwa yenye ubora wa hali ya juu. Wizara yangu imekwishatoa maelekezo kwa Chuo cha Ushirika Moshi kuendesha mafunzo ya uendeshaji bora wa Vyama vya Wafugaji ili viweze kuwa na manufaa ziadi kwa wafugaji. Ninapenda kutumia fursa hii kutoa mwito kwa wafugaji wote kuiga mfano, wa Vyama vya Wafugaji vya Mkoa wa Tanga.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirika Masoko amesema kwamba anashughulikia suala la masoko. Je, ni masoko mangapi yanayoshughulikiwa na Wizara ya Ushirika na Masoko katika Wilaya ya Monduli?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama Naibu Waziri alivyosema ni kweli Serikali inashughulika na masuala ya masoko ya mifugo. Tatizo ni kwamba utaratibu haufuatwi, watu wamezoea *panya routes.*

Katika Wilaya ya Monduli kwa mfano, katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, tumefungua soko kubwa sana pale Londigo kwa ajili ya kuuza mifugo nchi ya Kenya, lakini tatizo ni kwamba wananchi hawapendi kwenda kwenye soko, badala yake wanapita njia za pembeni wanapeleka mifugo yao Kenya. Kwa hiyo, naomba tushirikiane na Mheshimiwa Mbunge kusaidia masoko haya yaliyoanzishwa pamoja na lile la Longido yaweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Zamani kulikuwa na Bodi ya Maziwa na hivi karibuni tumeambiwa Bodi hiyo imeundwa upya. Je, shughuli zake ni nini na ina uhusiano gani na Wizara ya Ushirika na Masoko?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO (k.n.y. WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO):** Mheshimiwa Spika, sheria anayoizungumza tunakusudia kuileta katika Bunge la mwezi Januari na maelezo yote yatapatikana wakati huo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Tunaendelea na mambo mengine, lakini kabla ya hapo nina matangazo mawili.

Tangazo la kwanza ni kwamba, wale Waheshimiwa Wabunge wenzetu watatu walioadhibiwa katika Bunge lililopita kwa kusimamishwa shughuli za ndani ya Bunge hili adhabu yao wameimaliza na sasa wamerejea Bungeni, tunawakaribisha. Nao ni Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou. *(Makofi)*

Tangazo la pili ni kwamba, Mheshimiwa Ritta Mlaki, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, anawaomba Wabunge wa Mikoa inayolima Korosho ambayo ni Mtwara, Lindi, Pwani na sehemu ya Dar es Salaam, wakutane naye saa 5.00 katika chumba namba 227, ghorofa ya pili ya vyumba vyetu vya Kamati.

Kabla ya kuendelea na *Order Paper,* kama nilivyowataarifu jana kwamba sasa kwa kuwa tuko katika kipindi cha Mfungo wa Ramadhani ni lazima tubadilishe saa zetu za vikao kwa kutengua kanuni. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, atoe hoja ya kutengua Kanuni inayohusika.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI YA MUDA WA KUINGIA BUNGENI KIPINDI CHA MCHANA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 120, naomba Bunge lako Tukufu likubali kutengua kanuni ili muda wa kuingia Bungeni kipindi cha mchana uwe ni saa 10.00 jioni badala ya saa 11.00 jioni na kumaliza saa 12.00 jioni badala ya saa 1.45 usiku ili kuwawezesha wenzetu waliofunga waweze kuwahi kuswali na kufuturu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ya Kutengua Kanuni ya Muda wa Kuingia Bungeni Kipindi cha Mchana Ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, ni *procedural motion* inaitwa, haina mjadala.

Waheshimiwa Wabunge, samahani kulikuwa na tangazo lingine kumbe nilikuwa sijaliona.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu wakutane leo tarehe 4 Novemba, 2003 saa 5.00 asubuhi katika ukumbi namba 75 ghorofa ya pili, ili kushughulikia Muswada ule wa *Merchant Shipping* ambao Kamati ilipelekewa na Spika.

Tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Utoaji wa Huduma za Afya ya Mifugo wa Mwaka 2003 *(The Veterinary Bill, 2003)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *Veterinary Act* wa mwaka 2003 sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma za mifugo na usimamizi wa maadili ya taaluma ya Madaktari hudhibitiwa na sheria ya *Veterinary Surgeons Ordinance Cap. 376* ya mwaka 1956 ambayo ilifanyiwa marekebisho madogo sana mwaka 1963. Sheria hii

inawalenga Madaktari wa Mifugo wenye ajira ya Serikali na kwa kiasi kikubwa imetumiwa vizuri sana wakati wa ukoloni hadi katikati ya miaka ya 1990.

Mheshimiwa Spika, katikati ya miaka ya 1980 hadi sasa Serikali imefanya mageuzi ya sera za kiujumla za kiuchumi na za kihuduma za jamii. Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997 inaelekeza Sekta Binafsi kutoa huduma za mifugo, kuagiza na kusambaza madawa na pembejeo nyingine za mifugo. Kufuatia mabadiliko haya ya kisera kumekuwepo na ongezeko kubwa la watoa huduma za mifugo katika Sekta Binafsi ambao hawasimamiwi na sheria iliyopo. Kwa sasa kati ya Madaktari 450 waliosajiliwa mwaka 2002 asilimia 55 wameajiriwa Serikalini na katika Mashirika ya Umma, wakati asilimia 45 wamejiajiri wenyewe.

Aidha, kuna wataalam mbalimbali wanaotoa huduma za mifugo wapatao 2,500 wenye Stashahada na Astashahada, lakini hawasajiliwi kulingana na sheria ya sasa na wengi wao wako katika Sekta Binafsi. Kabla ya mwaka 1994 Serikali ilikuwa ikichukua huduma zote za mifugo na watoaji huduma hao binafsi hawakuwepo. Sheria hii inakusudia kuimarisha udhibiti wa maadili katika utoaji na usimamiaji wa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 Wizara yangu iliitisha mkutano mkubwa wa wadau wa Sekta ya Mifugo ambao Mheshimiwa Rais, Benjamin William Mkapa, aliufungua na kuwa Mwenyekiti wake. Katika mkutano huo wadau walibainisha matatizo makuu saba yanayoikabili Sekta hii, mojawapo ikiwa ni magonjwa ya mifugo.

Katika mkutano huo wadau waliweka dira ya Sekta ya Mifugo na ninukuu: "Ifikapo mwaka 2025 kuwe na Sekta Shirikishi ya Mifugo yenye ufugaji endelevu, yenye mifugo bora yenye uzalishaji mzuri, inayoendeshwa kibiashara na yenye kuboresha hali ya maisha, ajira na uzalishaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda, yenye kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa na kuhifadhi mazingira." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, dira hii itaweza kufikiwa kama huduma za mifugo zitaimarishwa kwa kuongeza na kuboresha usimamizi wa wataalam wanaotoa huduma hizo za mifugo. Chini ya sheria hii kutakuwepo na chombo yaani *Veterinary Council of Tanzania* kitakachosimamia maadili ya wataalam hao.

Wizara inategemea kwamba huduma bora za afya ya mifugo zitapunguza matukio ya magonjwa ya mifugo na hivyo kuongeza uzalishaji wa mifugo bora na mazao yake kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi yetu. Kabla ya kutoa mpangilio wa mtiririko wa Muswada huu, naomba nichukue fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Eliachim Simpasa kwa msaada wao mkubwa walionipatia katika Muswada huu. *(Makofi)*

Pili, namshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge na wataalam wake ambao wametusaidia sana kuimarisha Muswada huu na Maafisa wa Wizara yangu ambao walikesha kuhakikisha Muswada huu unatoka kama ulivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha udhibiti wa magonjwa, sheria itaweka utaratibu wa lazima ikiwa ni pamoja na taratibu za usafirishaji wa mifugo na mazao yake na vyombo vya usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba nitoe kwa muhtasari wa mpangilio na maeneo muhimu ya Muswada huu.

Muswada huu umegawanyika katika sehemu kubwa saba kama ifuatavyo: -

Sehemu ya Kwanza ina Kifungu cha 1 - 2:-

(i) Kinaelezea jina la Muswada na kwamba utekelezaji wa sheria utaanza siku Waziri atakapotangaza kwenye gazeti la Serikali.

(ii) Kinatoa ufafanuzi *(interpretation)* pamoja na marekebisho katika kifungu hicho.

Sehemu ya Pili ina Kifungu cha 3 - 14:-

(i) Kifungu cha 3 - 4, kinaelezea kuundwa kwa Baraza, muundo wake na hadhi yake kisheria, pamoja na marekebisho katika kifungu cha 3 ibara ndogo ya (ii).

(ii) Kifungu cha 5, kinaelezea majukumu na madaraka ya Baraza.

(iii) Kifungu cha 6, kinaelezea uundwaji wa Kamati mbalimbali za Baraza pamoja na marekebisho katika kipengele kidogo cha pili.

(iv) Kifungu cha 7, kinaelezea uundwaji wa Sekretarieti ya Baraza.

(v) Vifungu vya 8 na 9, vinaelezea kuchaguliwa kwa Msajili na Naibu Msajili pamoja na majukumu yao.

(vi) Kifungu cha 10, kinaelezea kuchaguliwa kwa Wasajili wasaidizi katika ngazi ya Wilaya na majukumu yao.

(vii) Kifungu cha 11, kinaelezea kuchaguliwa kwa wakaguzi, majukumu na uwezo wao wa kisheria.

(viii) Kifungu cha 12, kinaelezea vyanzo mbalimbali vya mapato ya Baraza, mamlaka ya kukopa na kuwekeza, pia taratibu zote za fedha, matumizi ya maendeleo pamoja na marekebisho katika kifungu cha 12 (i).

(ix) Kifungu cha 13, kinaelezea maslahi ya Wajumbe wa Baraza, Kamati, Sekretarieti na Watumishi wote wa Baraza.

(x) Kifungu cha 14, kinaelezea jinsi sheria itakavyolinda Wajumbe, Wanakamati na Watumishi wa Baraza.

Sehemu ya Tatu ina Vifungu vya 15 - 27:-

(i) Kifungu cha 15 - 18, kinaelezea usajili wa Madakatari wa Mifugo na Madaktari bingwa ikielezea sifa za usajili, utaratibu utakaotumika na aina ya vyeti vitakavyotolewa.

(ii) Kifungu cha 20 - 21, kwanza kinaelezea utaratibu wa usajili wa Madakatari waliofuzu nchi za nje na wale ambao si Watanzania. Pili, utaratibu wa usajili wa muda mfupi yaani temporally registration.

(iii) Kifungu cha 22 na 23, kinaelezea utunzaji wa *register* ya Madaktari na Madaktari bingwa na taratibu za kuhakikisha kuwepo kwa jina katika register kila mwaka *(retention)* pamoja na marekebisho katika kipengele cha nne.

(iv) Kifungu cha 24, kinaelezea taratibu za kutangaza orodha ya Madaktari wa Mifugo katika gazeti la Serikali.

(v) Vifungu vya 25 - 27, vinaelezea taratibu za kufuta au kusitisha usajili na kusajili upya pamoja na marekebisho katika kifungu cha 25(i).

Sehemu ya Nne ina Vifungu 28 - 31:-

(i) Vifungu hivi vinaelezea usajili wa Wataalam wa Mifugo wenye stashahada *(Para-veterinarians)* na astashahada *(Para-veterinary assistants),* sifa za usajili na utaratibu utakaotumika na aina ya vyeti vitakavyotolewa.

(ii) Vifungu vya 33 - 37, vinaelezea utunzaji wa orodha ya majina ya wataalam hao, utaratibu utakaotumika kufuta au kusitisha usajili na utangazaji wa orodha ya wataalam waliosajiliwa katika gazeti la Serikali.

Sehemu ya Tano ina Vifungu 38 - 41:-

(i) Kifungu cha 38, kinaelezea taratibu za usajili wa sehemu au vituo cha huduma za afya ya mifugo.

(ii) Kifungu cha 39, kinaelezea taratibu za usajili wa vituo vya kutoa huduma za afya ya mifugo.

(iii) Vifungu vya 40 - 41, vinaelezea utunzaji wa rejista za vituo vya huduma ya afya za mifugo na taratibu za kufuta usajili wa vituo hivyo.

Sehemu ya Sita ina Vifungu 42 - 46:-

(i) Kifungu cha 42, kinaelezea mambo ya ujumla kuhusu maadili ya watoa huduma za afya ya mifugo.

(ii) Kifungu cha 43, kinamkataza mtu asiyeruhusiwa kisheria kutoa huduma.

(iii) Kifungu cha 44, kinampa Waziri mamlaka ya kuunda kanuni zinazoruhusu baadhi ya huduma za afya kwa mifugo kutolewa bila kufuata masharti ya sheria hii.

(iv) Kifungu cha 45, kinaelezea utaratibu wa kushughulikia malalamiko chini ya sheria hii.

(v) Kifungu cha 46 kinaelezea uwezo wa Baraza kutoa maamuzi yanayohusu malalamiko na kina marekebisho katika kifungu cha 3 (i) ukurasa wa 30 na aya ya 11 ukurasa wa 31.

Sehemu ya Saba ina Vifungu 47 - 52:-

(i) Kifungu 47, kinaelezea taratibu za mlalamikaji kukata rufaa.

(ii) Kifungu cha 48 - 50, kinaelezea makosa na adhabu chini ya sheria itakayopendekezwa.

(iii) Kifungu cha 51 kinafuta sheria ya Madaktari wa Mifugo *(Veterinary Surgeons Ordinance Cap. 376)* ya mwaka 1958. Kinatoa kipindi cha mpito kwa yale yaliyokuwa kwenye sheria ya zamani yaweze kuendelea kwenye sheria hii mpya.

(vi) Kifungu cha 52 kinampa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni *(regulations)* na taratibu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema na kama nilivyoonyesha kwenye hotuba yangu, maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi juu ya Muswada huu tumeyapokea, tumeyazingatia kama yalivyoonyeshwa katika marekebisho tuliyoambatanisha katika *Order Paper* ya leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya nakushukuru sana kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, naomba kuwasilisha taarifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taarifa inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 70 (ii) Toleo la mwaka 2003. Kabla sijawasilisha maoni naomba kwanza niwataje Wajumbe ambao wamehusika na kuchambua Muswada huu.

Wa kwanza ni Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh na Mheshimiwa John Singo.

Wengine ni Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Philip Magani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilichambua Muswada wa *Veterinary Bill, 2003* tarehe 27 Oktoba, 2003. Kabla ya kuchambua Muswada huu Kamati ilikutana na wadau mbalimbali kwa lengo la kupokea maoni ya kitaalam kutoka kwa wadau wahusika. Kamati ilifaidika sana kukutana na wadau pamoja na wataalam kutoka Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na kupata maelezo ya kitaalam.

Mheshimiwa Spika, sote tunajua kuwa huduma inayotolewa kwa mifugo yetu sasa hairidhishi na sheria iliyopo ililenga zaidi kwa huduma ya mifugo inayotolewa na Madaktari wa Serikali tu, lakini sasa huduma nyingi za mifugo yetu zinafanywa na watu binafsi ambao hawakutajwa kwenye sheria iliyopo sasa.

Aidha, kumekuwa na malalamiko mengi ya utumiaji holela wa madawa ya mifugo ambayo yanasababisha maradhi mengi kwa mifugo. Kamati imekubaliana na Muswada huu kuwa umeletwa wakati muafaka kabisa kwa sababu sasa umepanua wigo wa Sekta ya *Veterinary* na kuwahusisha watoa huduma wengi tofauti na sheria ya zamani.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yalijadiliwa katika Muswada huo na Mheshimiwa Waziri kama mtaalam wa masuala ya mifugo. Hakusita kukubaliana na mapendekezo ya Kamati ambayo yalitokana na kushirikiana na wadau, wataalam pamoja na wanakamati kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, labda tu nigusie maeneo machache tuliyopitia na kuyatolea maoni. Katika ibara ya 12 kifungu cha (1) (b), Muswada umeeleza mapato ya Baraza kwa ajili ya kuendesha shughuli zake kwa ufanisi, Kamati iliona kuwa vyanzo hivyo vinavyopendekezwa na Muswada huu havikidhi mahitaji ya Baraza, hivyo Serikali iwasiliane na Wizara ya Afya ili waone uwezekano wa kupewa sehemu ya mapato yanayotokana na sheria ya *Medicine Board* ambayo inatoa asilimia 2 ya dawa zinazoingizwa hapa nchini kwani baadhi ya dawa hizo zipo pia vile vile za mifugo.

Aidha, Muswada huo uweke ushuru au kodi kwa wale wote wanaoingiza kutoka nchi za nje nyama za makopo na maziwa ili fedha za kutosha zipatikane kwa ajili ya kuendeshea Baraza hili.

Mheshimiwa Spika, pia tuliangalia kwa karibu sana Ibara ya 20 - 21 ambazo zinaelezea kuwa Madaktari wa Tanzania waliosomea nje na wageni kutoka nje kabla ya kuanza kuendesha huduma za mifugo ni lazima wafanyiwe mitihani na kufaulu. Hili tuliona ni jambo la busara sana, lakini tulijiuliza nini sababu hasa ya kufanya hivyo kwa sababu vyuo vingi vinatambuliwa Kimataifa. Ni kwa nini Mtanzania aliyesomea Chuo Kikuu cha Makerere afanyiwe mtihani kabla ya kuanza kazi ya huduma ya mifugo?

Nashukuru Waziri alikubali, hivyo basi mitihani itafanywa na wale tu waliosomea kwenye vyuo ambavyo havitambuliwi Kimataifa au pale panapotokea mashaka. Lakini jambo tulilolisisitiza zaidi ni kwamba wageni wanaoomba leseni za kuendesha huduma hii basi wapewe leseni za muda kwanza hata kama watafanya mitihani na kufaulu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasi ya kiteknolojia inayoendelea na kubadilika mara kwa mara, Kamati ilikubaliana kuwa katika Muswada kiwekwe kipengele cha kuwa, Madaktari wa Mifugo ni lazima wapate mafunzo kila baada ya miaka mitano kwa sababu sekta ya *veterinary* ina mabadiliko makubwa ya mara kwa mara. Bila kupata mafunzo Madaktari hao watapitwa na wakati. Aidha, katika ibara ya 6(ii) tulipendekeza kuwa kuna ulazima wa kuongezwa Kamati ya Mafunzo *(Training Committee).* Mheshimiwa Waziri alikubaliana na hoja hii na akaweka kwenye Muswada huu kifungu ambacho kitaruhusu kuongezwa kwa Kamati zote kama itakavyoonekana kuna ulazima wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu pia tulijadili kwa kina na kupendekeza kuwa Muswada huu upanue wigo wake ili kuweka wazi nani atakuwa ameyatibu magonjwa ya samaki na ndege, kwani hapa haionyeshi magonjwa haya yanatibiwa na nani, ni *veterinary* au waganga wa kawaida. Kamati ilipata bahati katika kuimarisha hilo ya kwenda kutembelea shamba la ndege na wanyamapori lijulikanalo kama *Tegeta Avi Fauna Farm Limited* ambalo linaendeshwa na Mtanzania mwenzetu anayeitwa Willy Kusaga ambaye anajihusisha na usafirishaji wa ndege na wanyamapori na vile vile anawafuga. Kamati iliona umuhimu wa Muswada huu kweli kupanua wigo wake vile vile kuhusisha ndege na samaki.

Mheshimiwa Spika, Muswada umeweka wazi kwamba kama Serikali ikiamua kuharibu mifugo ambao wameathirika, basi wafugaji hao watalipwa fidia, lakini Muswada haukuweka wazi kwa vipi mfugaji aliyepoteza mifugo yake kutokana na *professional misconduct* au madhara yanayotokana na Daktari wa Mifugo kudhuru mifugo ya wafugaji, aidha kwa kumshauri mfugaji kutumia dawa vibaya au kwa namna yoyote ile. Muswada umeweka tu utaratibu wa hatua zitakazochukuliwa kwa Daktari ikiwa ni pamoja na kufutiwa usajili wake au leseni yake.

Hii tulikubaliana kuwa ni adhabu kubwa kwake yeye Daktari kufutiwa leseni, lakini kwa mfugaji hasara yake bado iko pale pale, itafidiwa na nani? Ni kwa nini

Muswada usiweke kipengele cha mfugaji kufidiwa na Daktari au na chombo chochote kile kuliko kutegemea kumpeleka Mahakamani kwa kutumia sheria nyingine za kawaida mfugaji ndiyo afanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Muswada huu, Kamati yangu ilikubaliana na Mheshimiwa Waziri na mapendekezo ya Muswada huu na kwa hivyo iliupitisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI ABASS JECHA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi ya kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kwa mujibu wa Kanuni, kifungu 70 (ii) kuhusu Muswada wa *Veterinary Act, 2003* kama ambavyo umewasilishwa mbele ya Bunge hili na Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Aidha, napenda pia kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kwa namna ambavyo wameandaa na kuwasilisha mapendekezo yao ambayo yamelenga katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika naomba nichukue nafasi hii adhimu nimpongeze kwa niaba ya Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya *SADC* inayoitwa *Southern African Developing Organisation Public Accounts Committee* na uteuzi wake huo si pekee kwamba ni heshima kwake tu, bali pia kwa Bunge letu na kwa Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona madhumuni makubwa ya sheria hii ni kuboresha huduma za mifugo nchini, hasa kwa kuzingatia mabadiliko ya Sera ya Kilimo na Mifugo mwaka 1997 kuipa nafasi Sekta Binafsi kushiriki kikamilifu katika kutoa huduma na hivyo kuongeza uzalishaji wa mifugo nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hayo, sheria hii inafuta ile sheria ya zamani ya 1956 ambayo ilifanyiwa marekebisho madogo mwaka 1963 ambayo kwa ujumla wake kwa sasa haikidhi haja kutokana na mabadiliko ya sera kama nilivyotangulia kusema hapo awali. Kufuatana na mabadiliko hayo na kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amependekeza, kumekuwepo hapa nchini ongezeko kubwa la watoa huduma za mifugo na hasa katika Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko hayo na kwa sababu sheria ya zamani haielekezi kudhibiti Sekta Binafsi, Kambi ya Upinzani inaona sheria hii sasa itaimarisha udhibiti wa maadili katika usimamiaji na utoaji wa huduma za mifugo hapa nchini. Aidha, sheria hii mpya inatambua kuwepo kwa Chombo maalum *(Veterinary Council of Tanzania)* ambacho kitasimamia na kudhibiti hayo maadili ya wataalam

wanaotoa huduma za mifugo nchini ili kuboresha viwango vya utoaji huduma na kuongeza pato la mfugaji.

Mheshimiwa Spika, kupitishwa kwa sheria hii, Kambi ya Upinzani inaona kwamba kutaimarisha huduma za afya ya mifugo, kupunguza matukio ya magonjwa na hatimaye kuongeza uzalishaji wa mifugo bora na mazao yake na kukuza soko la ndani na nje la bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inauona Muswada huu kuwa ni mzuri, umetayarishwa kitaalam na hasa kwa kuwa maudhui yake yanalenga katika kukuza kipato cha mfugaji na hatimaye pato na uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini kupitisha sheria iliyo nzuri na bora ni jambo moja na utekelezaji wa sheria yenyewe ni jambo lingine. Pamoja na uzuri wa sheria hii tunaishauri Serikali mambo yafuatayo: -

- Serikali iandae mkakati maalum wa kutoa *in-service training* kwa watendaji na hasa wale wa vijijini ambao wengi wao hawajapata mafunzo kwa muda mrefu na kwa kuzingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika karne hii ya leo.

- Serikali iandae utaratibu ulio madhubuti kabisa utakaoweza kuifuatilia mienendo ya watendaji katika kutoa huduma kuona kwamba maadili yanachungwa ipasavyo.

- Kwa kuwa sheria hii inampa Mheshimiwa Waziri uwezo wa kutengeneza kanuni na taratibu mbalimbali, Kambi ya Upinzani inamshauri Mheshimiwa Waziri afanye hima kutengeneza kanuni hizo zitakazowezesha kutoa ufafanuzi wa kutosha ili kurahisisha utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaunga mkono Muswada huu na tunaliomba Bunge lako Tukufu kuupitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kwanza kuchangia Muswada huu.

Pili, nampongeza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na wataalam wake kwa kuweza kuleta Muswada kwa wakati muafaka. Vile vile, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ambayo imepitia na kuchambua Muswada huu vizuri.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni muhimu sana hasa kwa kuunda hili Baraza la wataalam ambalo kwa kipindi kirefu sana tangu mwaka 1958 lilipoundwa na baadaye lilififia, lakini sasa hivi kuna mabadiliko makubwa sana katika hii Sekta ya Mifugo hasa ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tulifika wakati hawa wataalam wetu hawakuweza kufanya kazi kwa sababu ya ukosefu wa raslimali na kupoteza dira. Ninaamini Baraza hili linaweza likafanya kazi na kuwasaidia hasa hawa *professionals* wote, *veterinarians* ambao wanaweza wakakaa sasa na kudhibitiwa. Hili Baraza tunalitakia kazi njema.

Mheshimiwa Spika, karibu wataalam wengi wameunda mabaraza yao ya namna hii, lakini wanakuwa na haya kubwa sana ya kusimamiana. Sheria zao ni nzuri sana kwa jinsi walivyoziweka, lakini utendaji kazi wake siyo mzuri. Nadhani kwa vile wanaoneana haya wanashindwa kabisa namna ya kusukumana.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza tunayo katika *section* nyingi unakuta walimu, madaktari wa binadamu na kadhalika. Lakini hatuoni namna wanavyobanana, ila tunaona marupurupu mengi yanapelekwa katika mabaraza. *Funds* za kupata watapata lakini namna ya kubanana ndiyo tatizo letu, wako.

Kwa hiyo, naomba sana kwa hili Baraza wakifanya kazi tutapata matunda mpaka kule kwa wafugaji. Sasa hivi *industry* ya mifugo ni muhimu na ndiyo wakati sasa hivi wa kupanua masoko. Hapa hatujaona mfugaji analindwa. Nashukuru Kamati ya Kilimo na Ardhi, wameweka hili kwa sababu hapa mfugaji halindwi hata kama wakiua ng'ombe wake wote hakuna mahali anapokwenda. Naishukuru Wizara imekubali kuweka hicho kipengele. Maana yake nilikuwa nasoma pale kazi utamtufukuzaje huyu? Wakasema kwamba akiharibu kazi, kazi gani? Hawataji kitu gani cha kuharibu. Wameweka tu kijumla kwamba akiharibu kazi basi atafukuzwa. Lakini kwa nini useme ukiharibu kazi, ukiua ng'ombe wa mtu bila sababu na kujitia kwamba ugonjwa ndiyo huu, wewe unachomachoma sindano ng'ombe wanakufa unaacha, lazima nikuulize kwamba ni dawa gani na ugonjwa gani ambao umeua?

Vile vile nashukuru sana madaktari sasa hivi wengi wamefungua maduka ya madawa na kadhalika. Hatuna uhakiki wa madawa ambayo tunayojua sasa hivi ni hili baraza ambalo tunategemea kwamba litafanya kazi nzuri kupitia baraza hili. Sijaona kabisa mtiririko wake wa hili baraza kwamba katika ngazi ya Wilaya, baraza hili likoje ni vizuri Waziri utuelimishe hapo kwa sababu kuna *registration* ya hizi *facilities* kwa hiyo, ni muhimu katika ngazi ya Wilaya itakuwaje, katika ngazi ya Mkoa itakuwaje na huyu mlalamikaji awe anaomba hizi huduma za mifugo, watapitia ngazi vizuri. Nimeona kwamba kuna watu tu pale Wilayani lakini baraza itakuwaje?

Halafu katika kutunga kanuni ya Waziri utuwekee kipengele kidogo kama ikiwezekana hata wafungaji nao wakawa na baraza lao ili ziende sambamba kidogo na hawa na malalamiko wawe kama wadau kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika suala hili nilitaka nisisitize kwamba baraza hili tunawatakia kila heri kufanya kazi, tunawatakia vile vile madaktari ufanyaji kazi mzuri, waunde chombo chao na wakisimamie na kazi hizi ambazo zimewekwa hapa zifanye kazi kwa sababu sasa hivi tuko katika ushindani mkubwa, kama tunavyoelewa kwamba sasa hivi katika Muswada mwingine unaofuata ni mzito kama huu.

Lakini sasa hivi wafugaji tunahitaji kwenda katika masoko mazuri na hatuna mategemeo makubwa kama hawa madaktari hawatafanya kazi nzuri, tuna mategemeo makubwa kwamba watatuvusha mifugo nayo iingie katika soko la dunia ni hawa madaktari na hiki chombo ndiyo vitakavyotuvusha sisi. Kwa hiyo, wafugaji wote wana matumaini makubwa sana na baraza hili, kwamba hiki chombo kitazaa matunda makubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii nizungumzie Muswada huu wa sheria unaohusu Huduma Bora za Mifugo ili kuongeza ubora wa mifugo yetu nchini. Muswada huu ingawa inazungumzia mifugo nataka kutoa taarifa tu kwamba si wafugaji peke yake watakaofaidika na Muswada ni pamoja na Wakulima wa Morogoro Vijijini. Naomba rejeeni mkutano tulioufanya na Mkuu wa Mkoa mwezi wa jana ambapo wadau wote wakulima na wafugaji tulikaa pale katika Manispaa ya Morogoro ili kujadili matatizo makuu yanayowakumba wakulima na wafugaji Mkoani.

Wafugaji maoni waliyotoa ni kuhusu uhafifu wa dawa, ubora wa dawa, mambo ya malisho na kukosa maji ya uhakika. Sasa Muswada huu ambao tunaujadili unajibu baadhi ya hoja chache ambazo zilikuwa zimeelekezwa katika mkutano ule ambaye mimi nilikuwa mzungumzaji mkuu katika sehemu ile na Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Stephen Mashishanga, kama tulitabiri kama kuna Muswada wa aina hii unakuja kwa kuwa utupa mapema huu tulikubaliana nao kwa hiyo niliwaambia kwamba hoja hizo zitajibiwa katika Muswada huu kwa ajili ya kuboresha na kutekeleza azimio la mkutano wa wadau wa Arusha ambao mimi nilikuwa mshiriki pamoja na kwamba sina hata ng’ombe mmoja, nina kuku tu na mbuzi mmoja tu pale nyumbani. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini *at least* Muswada huu unajibu hoja kwamba mimi ni mfugaji nusu lakini kwa hakuna nusu mfugaji na hakuna ng’ombe wa ghorofa kwa hiyo, nilikuwa najua kwamba mimi nilikuwa ni mdau na mdau wa Watanzania kwa sababu wafugaji na wakulima ni kitu kimoja, tunawatetea hapa kwa ajili ya masuala haya.

Sasa mambo ya Kimuswada *technicality* nilisoma kwenye *amendment* ya Muswada wenyewe nimeona kuna kitu kinaitwa *The Bill Act, 2003* lakini kwenye *Order Paper* imeandikwa *The Veterinary Bill, 2003* nadhani haya ni maneno tu *(wording)* kwa sababu ni matajiri wa maneno kwa hiyo, nadhani hiki ni kitu kimoja tu. Sasa *technicality* za Muswada kwa sababu mimi si Mwanasheria ni Babasheria natunga sheria kwa kuwa maneno ya ki- *technicality* siyajui.

Baada ya kusema hayo juu ya utangulizi naomba niseme kwamba Muswada huu sasa kwa kuwa umeanza ni moja ya utekelezaji wa maazimio ya kule Arusha ya mwaka 2001, ambayo nilihudhuria basi uzingatie yale maazimio 7 ambayo tuliyatoa ili kuboresha mifugo nchini.

Lingine la msingi ni kwamba elimu kwa wafugaji wenyewe. Najua hawa watalaam ambao wanatajwa humu ma-*Veterinary* wana elimu. Lakini elimu kwa wafugaji kwamba wasiwasumbue watalaam ambao tunawaunda hapa pamoja na baraza kwamba watulie mahali pamoja. Kama mko Morogoro basi tutaorodhesha mifugo yote kule Morogoro na kuwapangia maeneo ya kukaa kwa mfano kule Magera Kamati zimekaa tumepanga kuwapanga Kiegea na watapata huduma zote kule, kule Kidugalo tumepanga kule Ekenywa ambako tayari tumepata shilingi 3,000,000/= ambazo Mheshimiwa Edward Lowassa, ulitoa mwaka jana na zinaanza kufanya kazi. *(Kicheko)*

Natoa wito kwamba naomba Lambo lile liishe kabla sijarudi. Maeneo kama Lugaga na maeneo mengine kwa kweli mifugo kwa taarifa ya tathmini ya miaka 20 ya Chama cha Mapinduzi katika ukurasa 57 tumesema naomba ninukuu inasema kwamba: "Kwa upande mifugo uzalishaji wake haukubadilika sana hata ukizingatia Tanzania ina mifugo ipatayo 12.5 milioni kwa mujibu wa sensa ya mifugo ya 1984. Lakini mifugo bora miongoni ya hiyo ni 230,000 tu."

Hii ni aibu kubwa sana kwa Taifa ambalo lina mifugo kiasi hiki lakini wachache ndiyo bora. Ina maana kwamba hawa wote ni wagonjwa au wamekonda. Ingekuwa tunaye ng'ombe wa ghorofa tungeunganisha hawa wazima kutengeneza na hawa wengine ili waonekane angalau wana afya kidogo. Lakini hakuna ng'ombe wa ghorofa, yupo ng'ombe ambaye kila mmoja anatembea kwa wakati wake, roho yake, nyama yake, maziwa yake na maeneo mengine. *(Kicheko)*

Sasa ndiyo maana tumeamua kutengeneza huu Muswada ili kuweza kudhibiti masuala ya uingizaji wa madawa kwa sababu tumepitisha biashara hii huria kabla ya Muswada huu haujaja. Kwa hiyo, yako madawa ambayo pengine yamefutwa duniani kwa mujibu wa *WHO* lakini yanaweza kuletwa Tanzania na *National Environment Management of Council* imegundua baadhi ya madawa ya aina hiyo.

Sasa madawa kama ya kuulia wadudu yanapomwagwa kwenye majani halafu wafugaji wanakwenda kulisha maeneo hayo. Muswada umekaa kimya maeneo kama hayo vile vile. Sasa ni sheria ipi inazingatiwa ni hii au sheria ile ya madawa kuulia wadudu au *food drugs, cosmetic* pale vile vile tuwasiliane na Wizara ya Afya ili tujue kifunga gani kinachomruhusu mfugaji ng'ombe zake wanapokufa, kwa mfano wanakufa ng'ombe kwamba umeua uchumi wake, sasa anachukua hatua gani za kufanya hiyo?

Lingine ni elimu kwa mfano kuna viwango kwanza kiwango cha ng'ombe mwenyewe kama siyo bora basi nyama yake si bora vile vile. Kwa hiyo, utakuta kwamba kama ng'ombe si bora basi Watanzania wanakula nyama ambayo haiko katika *standard* ambayo si bora.

Kwa hiyo, Muswada huu utazingatia kwamba Watanzania wataanza kula nyama bora ili kwa kuanza kuwapima ng'ombe wenyewe na kupima nyama kabla haijawekwa kwenye ma-*butcher.* Kwa hiyo, ma-*veterinary* wasishughulikia ng'ombe wazima peke

yake, washughulikie vile vile ng'ombe ambao wamechinjwa, kushughulikia nyama kupimwa ili Watanzania wasije wakaambukizwa magonjwa hayo.

Mheshimiwa Spika, tabia nyingine kwa mfano ya matangazo ya *veterinary* katika Wilaya na Mikoa. Unakuta kwa mfano wanatangaza kwa mfano mbwa wachanjwe kesho, wasipochanjwa tukiwakuta hawajachanjwa tutawaua. Sasa lengo la daktari siyo kuua mbwa, lengo la daktari ni kutibu. Sasa kwa sababu mbwa hana akili ya kwenda kwenye *clinic* mwenyewe, ni yule mmiliki ndiye apewe adhabu, asipewe adhabu mbwa mwenyewe ambaye hajui. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, Waziri utakapotunga Kanuni katika kifungu kilichotajwa katika Muswada huu basi wale maafisa ambao wanakimbilia kuua tu kwa sheria sasa hivi wakimbilie kwenda kuwatibu mbwa hao na baadhi ya mifugo mingine ili kuwa na taratibu hizo.

Mheshimiwa Spika, vile vile mizoga ambayo inatupwa katika miji mbalimbali huokotwa na kwenda kuuzwa katika maeneo fulani fulani. Ilitokea Dar es Salaam na ilitangazwa na ilifanywa msako mkali.

Napenda kutoa pongezi kwa viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa hatua zilizochukuliwa mwezi Septemba, 2002 na mwanzoni mwa mwaka huu kwa hatua ambayo mizoga ya kule Ruvu na Pugu ambayo ilikuwa imechukuliwa kwenda kuuzwa katika masoko ya nyama ya Dar es Salaam. Wananchi wa Dar es Salaam walikuwa wanalishwa nyama ambazo si za *standard* ambayo inatakiwa.

Lingine ni kwamba kuna tabia kwa baadhi ya wafugaji kuweka alama ng'ombe, wanawachanja bila ridhaa yao. Utakuta ng'ombe anawekwa hereni kwa ajili ya alama. Kwa hiyo, zile nazo zingetajwa kwa sababu ile ni *effect* kwa magonjwa mengine yanaingia kwa ku-*penetrate* kupitia kwenye ngozi ili kuingia kwenye *blood stream.* Kwa hiyo, hiyo nayo vile vile ielezwe kabisa kama alama wanataka wafunge shingoni na kuwapa majina tu wale ng'ombe kama wanataka kuwapa majina yao. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, halafu afya ni kitu muhimu sana kwa hiyo, izingatiwe kote kuangalia maduka ya madawa ambayo wanauza dawa za ng'ombe na wale waganga wanaokwenda kuwaona wafugaji kule kule kuwauzia madawa kwa kufunga kwenye vifungashio visivyo sahihi. Wanapimiwa kwa vijiko kwa bei kwa hiyo, hii nadhani itakuwa imesimamisha tabia hii. Kuna baadhi ya wafugaji wanauziwa dawa maeneo kama vile Mvuha, kama sehemu za Ngerengere wanauziwa madawa kwa kufungiwa kwenye magazeti kwa ajili ya kuogeshea ng'ombe.

Kwa hiyo, unakuta pengine zile zimepitwa na wakati hakuna *expiring date,* wala *quality control,* wala jina la dawa yenyewe, ila wanaambiwa jinsi ya kufanya. Kwa hiyo, mifugo mingi imepata matatizo, hasa *deep concentration* ambayo unakuta wengine hawajui utaratibu wa *concentration.*

La mwisho, ni kutoa elimu kwa wafugaji kwamba matumizi bora, wakiwa Magela wabaki Magela pale pale wasitoke Magela wakati tunafanya utaratibu wao wa kuwasaidia sasa baada ya muda wa miezi miwili wanakwenda Mkulazi, baada ya miezi mitatu wanahamia Mikese, wabaki maeneo na Wakuu wa Wilaya wamepata maelekezo na Mkuu wa Mkoa kwamba wanapokaa kwenye vituo tuwaletee huduma bora maeneo haya, wasihamehame. Tunaomba wawe wafugaji wasiwe wachungaji. Sheria hii inazungumzia wafugaji. Atakayependa kufuga hukaa eneo moja, tutawasaidia kuwapatia Malambo na huduma muhimu maeneo hayo. Lakini ukihama Lambo halifuati huko uliko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja kwamba huo ni Muswada ambao unatekeleza Azimio la Arusha ambalo mimi nilikuwa mjumbe wa Kamati ya wadau pamoja na kwamba sina ng'ombe. Ahsante nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita mtoa hoja nimthibitishie Mheshimiwa Semindu Pawa, kwamba *Order Paper* haijakosewa, hii ndiyo inakuja Bungeni, *Bill* ikishakupitishwa na Bunge ikienda kwa Rais ikakubaliwa ndiyo inakuwa *Act* yaani Sheria kamili. Kwa hiyo, *Order Paper* inavyoonyesha *Bill* ni sawa sawa kabisa. Sasa namwita mtoa hoja ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuhitimisha hoja yangu ambayo imeungwa mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Kwa sababu imeungwa mkono asilimia mia kwa mia, sikusudii kupoteza muda wako kurejea maeneo ambayo yameshaelezwa katika sheria. Lakini naomba nifanye yafuatayo:-

Kwanza kuwashukuru sana waliochangia Muswada huu ambao ni Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Semindu Pawa na Mheshimiwa George Lubeleje, aliyeniletea maelezo yake kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Muswada umeungwa mkono, lakini naomba nifafanue maeneo machache sana.

Kwanza nitoe mfano katika Wilaya moja hapa nchini naihifadhi jina kwa faida ya Mheshimiwa Mbunge, asidhani nampiga vijembe, kulikuwa kumetokea ugonjwa, ulipotokea ugonjwa wale wafugaji wakaenda nchi jirani, yule mwenye boma akaenda akachukua dawa, dawa aliyochukua ni dawa ya kinga ambayo inatakiwa ibebwe kwenye chombo maalum kwenye *fridge* na utaratibu wa kumdunda ng'ombe yule kinga upo. Yeye akachukua akijua dawa ile ni ya kwenda kutibu mgonjwa.

Kwa hiyo, ameingia amemdunga asubuhi, amemdunga na jioni. Katika muda wa siku tatu, ng'ombe zaidi ya 100 walikufa. Walipoitwa watalaam wakamwuliza mzee hizi

dawa umetoa wapi? Akasema nimetoa nchi jirani. Hii dawa ni ya nini? Akasema si ya kutibu huu ugonjwa. Mzee mbona umepewa dawa ya chanjo? Ulibebaje? Ahaa! Waliniwekea kwenye kibakuli nikabeba.

Mheshimiwa Spika, sasa matukio kama haya ndiyo yanatufanya tuje na sheria ya kuwa na watalaam wanaoweza kufanya kazi hizi za kitaalam. Tunatunga sheria kwa madhumni ya kuwatawala wale madaktari wa mifugo ya wenyewe wasifanye vitendo vya ovyo, lakini waweze kuwasaidia wafugaji.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba huko duniani kuliko endelea mtu chakula anakula lazima ajithibitishie kwamba chakula kile ni kisafi hakina madhara kwa mwili wa binadamu. Duniani siku hizi wameanzisha utaratibu wa *tracebility* kwa mifugo mpaka tunajaribu kuanza kwenye *SADC Region* kwamba ng'ombe anapokuwa mchanga wanamvalisha ka- *chivy* hivi *computer,* wanapokwenda kumchinja wana- *retrieve* kale ka-*chivy* katakuambia alizaliwa tarehe ngapi, katika shamba la namna gani na ametembelea wapi. Kwa hiyo, ng'ombe anaweza akaliwa London lakini wakajua ametoka Mabuki, Tanzania. Sasa wakiona ametoka Mabuki, Tanzania wanaangalia mbona ana ugonjwa basi, kama ana magonjwa mara moja wanakuwa wanasema hatukubali tena nyama ya kutoka nchi ile kwa sababu kwa utaratibu huu tumegundua mifugo yao ina matatizo. Kwa hiyo, lazima masuala lazima yafanywe kisayansi na sisi ili tuweze kuingie katika soko la dunia lazima tujiimarishe kuelekea huko.

Nakubaliana na Mheshimiwa Eliachim Simpasa, nakubaliana kama tulivyokubaliana kwenye Kamati kwamba Baraza linahitaji mapato. Lakini kama tulivyokubaliana tutawasiliana na Wizara ya Afya kwa sababu kuna ile *Pharmacy Board* na *Medical Board* ambako wanakusanya *two percent* tuone jinsi tunavyoweza kugawana. Madawa yanayochajiwa ni ya mifugo pamoja na yale ya binadamu.

Pia nakubaliana na Mheshimiwa Mwadini suala la mafunzo ni suala la muhimu si kwa sekta ya mifugo tu mimi nadhani kila mahali, kila mtu hata mimi kama Mbunge nahitaji kila siku kujielimisha ili kukidhi mahitaji ya dunia ya sasa.

Vile vile nakubaliana na wewe na Mheshimiwa Benedict Losurutia, watalaam wabanane nakubaliane wabanane katika *professional* yao ndiyo maana ya kuunda baraza na baraza kiwilaya tutalieleza katika kanuni atakazotunga Waziri utaratibu wake utakuwa vipi. Juu ya mfugaji, mfugaji analindwa katika sheria itakayoelezwa muda mfupi ujao, mle mfugaji analindwa na anapewa *compensation.* Daktari pia anaadhibiwa akifanya kosa ambalo ni *unprofessional* anafutwa katika *registry.* Akifutwa maana yake *the man is jobless.* Nadhani hakuna adhabu kubwa dunia kama ukishakuwa huna kazi huwezi kufanya kazi yoyote na una akili yako una miguu miwili na mikoni miwili nadhani ni adhabu kubwa sana. Nadhani ukishaondolewa hiyo inakuwa ni balaa kubwa.

Madawa yanayoletwa nchini umelisemea Mheshimiwa Semindu Pawa, amelisemea Mheshimiwa Benedict Losurutia, lakini iko sheria inayotawala hii ya wenzetu ile *Drugs and Cosmetic Act,* wako wenzetu pia wa *TRI* ambao wana mchango katika hili tutashirikiana wote kuangalia kwamba hili halitokei. Nakubali hili eneo ni

nyeti ambalo linataka usimamizi wa karibu lakini naahidi kwamba Serikalini tutashirikiana wote kuhakikisha hilo linafanyika.

Pia Mheshimiwa Semindu Pawa, nakubaliana na mengi uliyosema lakini nakubaliana zaidi na hili la elimu kwa wafugaji ni muhimu sana, nilikuwa naomba tusaidiane kuwaelimisha wafugaji wetu suala la elimu mpaka waelewe mambo haya, mpaka waelewe kwamba sera hizi madhumuni yake ni kuwasaidia.

Ukienda sasa hivi Morogoro kumejaa misitu na vyanzo vya maji ambavyo ni imara, leo vingi vimevamiwa sana kama tukiruhusu ufugaji ule ukaendelea kwa utaratibu ule hapatakuwa na mahali pa kufuga wala pa kulima. Ndiyo tunasema tunataka wananchi hawa wakae katika maeneo yao waangalie ubora wa mifugo yao, lakini ubora pia wa ardhi yao na wajue kwamba wakimaliza kutumia eneo ambalo wako hakuna mtu mwingine ambaye amewatengea eneo kule, ajue akimaliza eneo hili hawezi kuhama abaki pale pale kwenye eneo lake. Kwa hiyo, tunaendelea kusisitiza kwamba elimu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine dogo ni hili la Watanzania na wenyewe kujua haki zao na Watanzania kujiletea utamaduni wa kudai mahitaji yanayopaswa kwa mfano, ng’ombe au mbuzi akichinjwa ni lazima mkaguzi wa *veterinary* amkague ampige muhuri utaona muhuri pale. Una haki unapokwenda kwenye *butcher* udai huyu ng’ombe amekaguliwa?

Sasa kinachonisisitiza ni kwamba Watanzania hatudai ndiyo maana watu wanalishwa kibudu. Nitatoa mfano pale Dar es Salaam ugonjwa wa kimeta. Ugonjwa wa kimeta umetokeaje? Mtu amechinja ng’ombe mzuri kweli nyumbani kwake, amekaribisha majirani wake wote wamenunua ng’ombe, lakini baada ya muda wamegundua ng’ombe yule alikuwa na kimeta kwa sababu hakupimwa na watu wamekula nyama ile.

Lakini nasema Watanzania na sisi tujijengee utamaduni wa kudai haki zetu unapokwenda kwenye *butcher* u-*check* ng’ombe huyu alikaguliwa? Amepigwa muhuri? Kwa sababu kama amepigwa muhuri ukapata kimeta kwa sheria hii tutashughulika na yule daktari. Lakini ukipata kimeta kwa sababu mwenyewe umejitakia utashindwa kudai haki zake, unaipa nchi hasara tu. Lakini nasema ni vizuri tukaendelea tukaelimishana.

Tunakubali pongezi zako Mheshimiwa George Lubeleje, kwamba tumeimarisha *Mpwapwa Lite.* Lakini niseme mbele ya Bunge na Bunge lijue na Taifa lijue kwamba sasa vyuo hivi vinakwenda kwa utaratibu wa kuangalia wananchi wenyewe wanataka mafunzo ya aina gani. Wengi wa wanafunzi waliopo, asilimia kubwa ni wale ambao wanajigharamia wao wenyewe anajua kwamba nikisomea jambo hili linasoko katika *industry.*

Mheshimiwa Spika, *Lite* imejaa Morogoro vile vile imejaa nimeambiwa na Tengeru imejaa baada ya wananchi kujua kwamba naweza kugharamia naweza kugharamia masomo ya namna

hii kwa sababu nina hakika ya kupata kazi nina uhakika wa kupata cheti na naweza kufanya kazi zangu vizuri. Nakushukuru kwa mchango wako.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema hoja imekubalika nawashukuru sana kwa dhati Waheshimiwa Wabunge kwa kupitisha Muswada huu lakini kazi kubwa inayofuata ni kusaidia kuendelea kuelimisha ili wananchi wetu wafahamu maana ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hoja ni kwamba Muswada huu sasa usomwe Mara ya Pili.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**SPIKA:** Shughuli za Kamati ya Bunge Zima zinaanza.

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha10
Kifungu cha 11

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 36

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 46

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 47
Kifungu cha 48
Kifungu cha 49
Kifungu cha 50
Kifungu cha 51
Kifungu cha 52

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali

*(Jedwali la Muswada lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Utoaji wa Huduma za Afya ya Mifugo wa mwaka 2003 *(The Veterinary Bill, 2003)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa baada ya Kamati ya Bunge Zima kupitia Muswada wa Sheria

ya Taaluma ya Mifugo kifungu kwa kifungu pamoja na mabadiliko yake na kuupitisha kama ulivyo, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *The Veterinary Bill* sasa ukulibaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Magonjwa ya Wanyama wa Mwaka 2003 *(The Animal Diseases Bill, 2003)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Magonjwa ya Wanyama yaani *Animal Diseases Bill, 2003* sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokuwa katika Muswada uliotangulia Muswada huu tumesaidiwa sana na Kamati ya Kilimo na Ardhi chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Eliachim Simpasa. Napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru sana kwa kazi yao nzuri. *(Makofi)*

Vile vile tumesaidiwa sana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalam wao, naomba kutumia nafasi hii kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mwisho, niwashukuru wataalam wa Wizara ambao na wenyewe wamefanya kazi kubwa toka maandalizi hadi leo Muswada huu ukafika hapa mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, hatua za kudhibiti na kuzuia kuenea kwa magonjwa ya wanyama zinasimamiwa na Sheria za Magonjwa ya Wanyama, yaani *Animal Disease Ordinance, Cap 156* iliyowekwa na Wakoloni mwaka 1940 na kufanyiwa marekebisho madogo mwaka 1960. Kuwepo kwa magonjwa ya mifugo kumesababisha Taifa kushindwa kufanya biashara ya nje ya mifugo na mazao yake kwani sheria iliyopo imepitwa na wakati na haiwezi tena kukidhi matakwa ya Kitaifa na ya Kimataifa katika kudhibiti magonjwa ya wanyama.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuanzishwa mfumo wa uchumi wa soko huru, Serikali imeiachia Sekta Binafsi shughuli za uzalishaji na biashara ya mifugo na mazao yake. Sekta Binafsi inashughulikia pia na uagizaji na usambazaji wa madawa ya kinga na tiba. Serikali imebaki na jukumu la kuandaa sera, kusimamia sheria na kudhibiti magonjwa ya milipuko. Kuwepo na kuenea kwa magonjwa ya mifugo ni kikwazo kikubwa katika kueneza sekta hii muhimu ambayo inachangia katika uchumi wa Taifa na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alitoa Waraka Na.1 wa mwaka 2002 kuhusu hatua za kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo nchini kama hatua ya kunusuru kuendelea kuenea kwa magonjwa hayo. Waraka huo umeagiza pamoja na mambo mengine haya yafuatayo:-

- Asasi zote za mifugo ziwe na mipango shirikishi ya kudhibiti magonjwa ya mifugo katika Bajeti zake.

- Kila Halmashauri ya Wilaya ifungue mfuko wa kuendeleza Sekta ya Mifugo kwa kutenga asilimia isiyopungua 15 ya mapato yake yatokanayo na mifugo na kutoa taarifa za mapato na matumizi ya mfuko huo kwenye Vikao vya Halmashauri.

- Kila Halmashauri ya Wilaya iwe na mipango ya kuelimisha Sekta Binafsi juu ya wajibu wao wa kusambaza madawa na kutoa matibabu ya mifugo

- Halmashauri za Wilaya zitunge sheria ndogo za kuimarisha usimamizi wa minada na usafirishaji wa mifugo. Kuanzia sasa utaratibu wa kuswaga mifugo kwenye maeneo yenye reli, barabara za lami au njia za maji, uachwe mara moja na Wakuu wa Wilaya wasaidie kufanikisha hilo. *(Makofi)*

- Halmashauri za Wilaya zihakikishe kwamba taarifa za magonjwa ya mifugo zinatumwa kwenye Vituo vya Kuchunguza Mifugo yaani *Veterinary and Investigation Centers* kabla ya tarehe 5 ya kila mwezi na ndani ya saa 24 baada ya kupata taarifa ya tukio la ugonjwa. Halmashauri zote za Wilaya nchini ziwe na mipango ya kufufua majosho na kujenga mengine mapya kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000.

- Wafugaji wahimizwe kukaa kwa utaratibu wa kudumu kwenye maeneo walipo na walinganishe idadi ya mifugo yao na uwezo wa malisho uliopo ili ufugaji uendeshwe kwa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Waraka huu yatarahisisha sana utekelezaji wa sheria tunayoipendekeza. Sheria iliyopo haina vifungu vinavyotosheleza kudhibiti ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa majukumu yaliyotajwa na matakwa ya vigezo vya Kitaifa na Kimataifa katika biashara ya mifugo na mazao yake hasa katika kudhibiti kuenea kwa magonjwa ya mifugo. Sheria ya sasa pia ina upungufu katika kuanzisha na kuendesha Vituo vya kutotoa vifaranga na Vituo vya Uhamilishaji yaani *Artificial Insemination Centers.* Aidha, sheria ya sasa haina kipengele kinachozuia kuingia nchini mifugo na mazao yake.

Mheshimiwa Spika, chini ya sheria tunayoipendekeza kutakuwa na utaratibu na viwango vitakavyotumika katika kuanzisha na kuendesha Vituo vya kutotolea vifaranga *(hatcheries)* na Vituo vya Kuzalisha Mbegu Bora za Mifugo kwani Vituo hivi vinaweza kuchangia katika kueneza magonjwa.

Aidha, kutakuwa na kipengele kitakachosimamia usafirishaji nje ya nchi au uingizaji nchini wanyama na mazao yao ikiwa ni pamoja na mazao yenye viini vilivyohasiwa yaani *genetically modified organisms* iwapo wanyama na mazao hayo yatakuwa yamesababisha au yanaweza kusababisha kuzuka na kusambaa kwa magonjwa ya wanyama na binadamu. Udhibiti wa magonjwa hayo ni miongoni mwa shughuli muhimu zinazofanywa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo ya Wizara kwamba sheria mpya itaondoa mapungufu yaliyokuwepo kwenye sheria ya zamani na kufanya iwe ni kichocheo halisi cha ukuaji wa Sekta ya Mifugo nchini katika misingi ya uchumi wa soko. Hii ni pamoja na kusisitiza udhibiti wa lazima wa magonjwa kabla na baada ya ugonjwa kutokea kwa kuzingatia mabadiliko ya kiteknolojia. Ili kurahisisha udhibiti wa magonjwa, maeneo ya nchi yatatenganishwa yaani *classified* na kuainishwa kufuatana na hali ya magonjwa ya wanyama katika sehemu zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, kutakuwa na utaratibu wa kutoa fidia kwa wafugaji ambao mifugo yao itaangamizwa ili kutokomeza magonjwa fulani fulani kadri itakavyoonekana inafaa. *(Makofi)*

Aidha, kutokana na kufanana kwa mifumo ya uzalishaji hapa nchini na nchi jirani, kwa mfano ufugaji wa kuhamahama, kuwepo kwa magonjwa yasiyo na mipaka, biashara huru ya mifugo na mazao yake, Wizara imezingatia kanuni na sheria mbalimbali ili sheria hii mpya iweze kukidhi mahitaji ya Kitaifa, Kimataifa na matakwa ya mifumo ya biashara chini ya *World Trade Organization* kwa kuzingatia mkataba wa *Sanitary and FISTO-Sanitary Agreement.* Utekelezaji wa Mkataba huu kwa upande wa Sekta ya Mifugo husimamiwa na *International Office of Epizootics* yaani *OIE* iliyopo Ufaransa ambayo nchi yetu ni Mjumbe kuanzia mwaka 1965. *(Makofi)*

Jumuiya nyingine kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* nazo zinaainisha sheria na taratibu za kudhibiti magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti ubora na udhibiti wa magonjwa ya mifugo, sheria itaweka utaratibu wa lazima ikiwa ni pamoja na taratibu za usafirishaji wa mifugo na mazao yake na vyombo vya usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nitoe kwa muhtasari mpangilio na maeneo muhimu ya Muswada huu. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tisa kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza, kifungu cha 1 - 2 kinaelezea jina la Muswada na kwamba utekelezaji wa sheria utaanza siku Waziri atakapotangaza kwenye Gazeti la Serikali. Kifungu cha pili kinatoa ufafanuzi yaani *interpretation* pamoja na marekebisho katika kifungu Na.2.

Sehemu ya pili, yaani vifungu 3 - 6. Cha tatu kinaelezea uteuzi wa Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, majukumu ya mamlaka yake kisheria pamoja na marekebisho kwenye kipengele cha (f). Kifungu cha nne, kinaelezea uteuzi wa Wakaguzi na mamlaka yao kisheria. Cha tano kinaelezea uteuzi wa watumishi wengine watakaopewa majukumu tofauti chini ya sheria hii. Cha sita kinaelezea juu ya kinga kwa madhara au hasara zinazoweza kutokea katika utekelezaji wa Muswada huu.

Sehemu ya tatu, vifungu 7 - 20. Cha saba kinaelezea hatua mbalimbali za kuzuia magonjwa ya wanyama. Cha nane, kinaelezea taratibu za kuzuia wanyama kuhama kutoka au kuingia sehemu yenye ugonjwa. Cha tisa, kinaelezea maeneo ya kuchunga. Vifungu vya 10 - 11, vinaelezea jinsi ya kutenga, kuzuia uhamaji na kuweka alama wanyama wagonjwa ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa pamoja na marekebisho katika kifungu cha 10(2) na 10(3). Vifungu vya 12 hadi 13 vinaelezea kuhusu kuwepo kwa eneo kati ya eneo lenye ugonjwa na lisilo na ugonjwa yaani *Buffer Zone* na kuzuia wanyama kuzuia au kutoka kwenye eneo hilo. Vifungu vya 14 mpaka 17 vinaelezea jukumu la kutoa taarifa ya kuwepo ugonjwa au kifo pamoja na taratibu za kuweka karantini katika eneo lenye ugonjwa pamoja na marekebisho ya kifungu cha 15(5) na kifungu cha 17. Vifungu vya 18 mpaka 19 vinaelezea kuhusu kuchinjwa au kuteketezwa wanyama wagonjwa ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa pamoja na marekebisho kwenye kifungu cha 18. Kifungu cha ishirini kinaelezea utaratibu wa lazima wa kutambua na kufuatilia mifugo yote nchini.

Sehemu ya nne, vifungu vya 21 hadi 25. Cha 21 mpaka 23 vinaelezea kuhusu kuorodheshwa magonjwa ya wanyama wasiofugwa, vibali vya mashamba ya wanyama hao na utangazaji matukio ya magonjwa yanayohusu wanyama hao pamoja na marekebisho kwenye kifungu cha 22(1)(2). Vifungu vya 24 na 25 vinaelezea utangazaji wa karantini kwenye eneo lenye ugonjwa na taratibuza kuteketeza wanyama wagonjwa ili kuzuia kuenea kwa magonjwa pamoja na marekebisho kwenye kifungu cha 25(4).

Sehemu ya tano, vifungu vya 26 hadi 39. Sehemu ya tano pamoja na marekebisho kwenye kichwa cha habari, vifungu vya 26 mpaka 30 vinaelezea mamlaka ya Wakaguzi na Madaktari wa Mifugo kufanya ukaguzi na uchunguzi kuhusu magonjwa ya wanyama. Vya 31 hadi 34 vinaelezea taratibu za kushughulikia mizoga ya wanyama na marekebisho kwenye kifungu cha 33(3). Vya 35 hadi 37 vinaelekeza taratibu za kusimamia usafirishaji wa wanyama kwa lengo la kupata taarifa za milipuko ya magonjwa ya wanyama pamoja na marekebisho kwenye kifungu Na.36(2), cha 38 kinaelekeza taratibu za Wakaguzi wa Madaktari wa Mifugo kusimamia utekelezaji wa sheria kwenye Vituo vya kutotoa vifaranga na Vituo vya uhamilishaji. Cha 39 kinaelezea uwezo wa kutoa tamko kuhusu maeneo yasiyokuwa na magonjwa pamoja na marekebisho kwenye kifungu Na.39.

Sehemu ya sita, vifungu 40 hadi 42 vinaelezea kuhusu utoaji wa fidia, mazingira yanayomwezesha mtu kulipwa fidia au kutolipwa na uwezo wa Waziri kuzuia utoaji wa fidia hizo pamoja na marekebisho kwenye kifungu 42(2).

Sehemu ya saba, vifungu 43 hadi 50. 43 mpaka 45 vinaelezea kuhusu udhibiti wa lazima wa magonjwa ya wanyama ikiwa ni pamoja na kudhibiti uhamaji na usafirishaji wa wanyama, uangalizi wa maeneo ya mipakani *(entry point)* na maeneo ya ukaguzi wa wanyama *(checkpoint)* pamoja na marekebisho kwenye kifungu cha 45(1) mpaka (3). Vifungu 47 mpaka 49 vinaelezea matumizi ya mamlaka ya Waziri katika kuanzisha mfumo au utaratibu wa kudhibiti magonjwa, kuanzishwa kwa maeneo maalum yasiyo na magonjwa *(Disease Free Zones)* na kufanya utafiti kwa wanyama waliogundulika kuwa na ugonjwa. Kifungu cha 50 kinaelezea udhibiti wa dawa za kuua wadudu na kemikali nyinginezo zitakazotumika kudhibiti magonjwa ya mifugo pamoja na marekebisho kwenye kifungu cha 50(1) na (2) kwenye mabano.

Sehemu ya nane, vifungu 51 mpaka 60. Kifungu cha 51 na 52 vinaelezea udhibiti wa maziwa na mazao yake, nyama na mazao yake ili kuzuia kuenea kwa magonjwa. Kifungu cha 53 kinaelezea udhibiti wa uchinjaji ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa machinjio *(design and layout)* ukaguzi wa wanyama kabla *(anti-mortem)* na baada ya kuchinjwa yaani *postmortem.* Kifungu cha 54 kinaelezea udhibiti wa uingizaji wa wanyama na mazao yake *(importation)* pamoja na marekebisho kifungu cha 54(1) na 54(3). Vifungu vya 55 mpaka 60 vinaelezea udhibiti wa magonjwa ya wanyama katika vituo vya uhamilishaji, matumizi na uuzaji wa viinitete *(embryos)* na mayai, matumizi na uuzaji wa wanyama na mazao yenye viini vilivyohasiwa, *(genetically modified organisms)* na udhibiti wa magonjwa ya nyuki na ya samaki pamoja na marekebisho kwenye kifungu cha 55(1).

Sehemu ya tisa, vifungu vya 61 mpaka 65. Kifungu cha 61 kinaelezea taratibu za kupeleleza na kukamata watuhumiwa. Cha 62 kinaelezea makosa na adhabu. Kifungu cha 63 kinaelezea Ushahidi unaoweza ukatumika Mahakamani. Kifungu cha 64 kinaelezea kufutwa kwa sheria ya magonjwa ya wanyama iliyopo na kifungu cha 65 kinatoa Mamlaka kwa Waziri kutengeneza kanuni na taratibu mbalimbali chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile tulipokea maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi na nimeyaeleza katika Waraka wangu na yamegawanywa leo asubuhi pamoja na *Order Paper.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninashukuru kwa kunisikiliza na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH (k.n.y. MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI NA KILIMO):** Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, kuhusu Muswada wa *The Animal Diseases Bill, 2003.*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge ibara ya 70(2), toleo la mwaka 2003, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi naomba kuwasilisha maoni ya Kamati.

Kamati ilichambua Muswada wa *The Animal Diseases Bill, 2003* tarehe 28 Oktoba, 2003. Kabla ya kuchambua Muswada huu Kamati ilikutana na wadau mbalimbali kwa lengo la kupokea maoni ya kitaalam kutoka kwa wadau husika. Kamati ilinufaika sana kukutana na wadau pamoja na wataalam kutoka Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kupata maelezo ya kitaalam.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha maoni hayo naomba kwanza niwataje Wajumbe wa Kamati hii ambao walifanikisha uchambuzi wa Muswada huu kama ifuatavyo:-

Kwanza Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge, ndiye Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Alhaj Shaweji, ndiye Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii ambaye ndiye mimi, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha na Mheshimiwa Philip Magani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umeletwa na Serikali kwa sababu ya kasi kubwa ya kusambaa kwa magonjwa ya wanyama hali ambayo inakuwa ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya mifugo hapa nchini. Mheshimiwa Waziri alivyosema, Muswada huu umelenga kufuta sheria ya magonjwa ya wanyama yaani *The Animal Diseases Control Ordinance Cap 156.* Sheria iliyotungwa mwaka 1960 ambayo haikuzingatia Sekta Binafsi na ambayo haina nguvu ya kudhibiti Sekta Binafsi. Hivyo Muswada huu umeletwa kwa wakati wake kwani sheria iliyopo kwa kweli imepitwa na wakati. Hivyo Muswada huu ni muhimu sana katika kuendeleza Sekta ya Mifugo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu Kamati yetu ilijadili mambo mengi lakini nitayataja mambo machache. Kamati ilikubaliana kuwa kati ya kazi za Mkurugenzi yaani katika Ibara ya 3(2) iongezwe pia kazi ya kutoa taarifa ya mwaka yaani *Annual Report Internationally.* Ni muhimu kazi hii iwekwe kwenye sheria.

Aidha, utaratibu wa kutoa ripoti Wizarani lazima uwekwe wazi kwa sababu watoa huduma katika Sekta ya Mifugo sasa ni wengi, hivyo kunahitajika mikakati kamambe katika ukusanyaji wa takwimu za kufikishwa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilimkumbusha Mheshimiwa Waziri kuwa ashughulikie mapema taarifa ya kuandaa kanuni katika kutekeleza Muswada huu kwani

kanuni zilizopo nazo zimepitwa na wakati. Aidha, Wajumbe walipendekeza utaratibu wa kutoa karantini uwekwe wazi katika kanuni ili kama Daktari wa mifugo ataweka karantini kinyume cha utaratibu uliowekwa na kusababisha hasara kwa baadhi ya wafugaji basi utaratibu wa kumchukulia hatua aliyeweka kanuni hiyo nao uwe wazi.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa usafirishaji wa mifugo katika minada yetu unasababisha kusambaa kwa magonjwa ya mifugo, hivyo kanuni pia ziwekwe wazi katika kudhibiti usafirishaji wa mifugo minadani.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilipokea mchango wa maandishi kutoka kwa Mkurugenzi wa *TPRI* Arusha kama mdau ambapo alipendekeza kuwa ibara ya 50(1) isomeke kuwa: *"The Director shall upon consultation with TPRI Act, ensure effective safe use and handling of pesticides for the control of Sectors of Vertenary porters."*

Baada ya maelezo ya kina kutoka kwa Waziri, Kamati ilikubaliana na Waziri kuwa suala la kudhibiti madawa hayo yabakie mikononi mwa Wizara kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI ABASS JECHA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nichukue fursa hii tena nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi kuzungumzia machache kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa kanuni ya 70(2) kuhusu Muswada wa *Animal Diseases Bill,* 2003 kama ulivyowasilishwa mbele ya Bunge lako na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuipongeza Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa mazingatio yao juu ya Muswada huu na namna ambavyo wamewasilisha hoja yao. Ni dhahiri kwama maelekezo na ushauri uliotolewa una nia ya kuongeza ufanisi katika sheria yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inauona Muswada huu kuwa ni mkombozi halisi wa wafugaji hapa nchini kwa kuwa moja katika sababu kubwa za uzalishaji hafifu katika mazao ya mifugo ni kutokana na kutodhibitiwa ipasavyo kwa magonjwa ya mifugo.

Aidha, kutokana na mabadiliko ya sera ya kilimo na mifugo, mwaka 1997, imeimarishwa Sekta Binafsi katika uzalishaji wa biashara ya mifugo na mazao yake, Kambi ya Upinzani imeona ni muafaka sasa kupitishwa kwa sheria hii ili hatimaye tuwe na mpango madhubuti wa kudhibiti magonjwa ya mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, matayarisho ya Muswada huu yamezingatia Waraka Na.1 wa Mheshimiwa Rais aliotoa 2002 kuhusu hatua ya kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo nchini jambo ambalo Kambi ya Upinzani inaona Waraka huu sasa utatekelezwa kwa mujibu wa sheria hii. Kadhalika, Kambi ya Upinzani inaona kupitishwa kwa sheria hii na kufuta ile ya zamani, *Animal Diseases Ordinance Cap 156* ya 1940 ambayo ilifanyiwa

marekebisho madogo 1960 kunaipa uhalali na nguvu mfumo wa uchumi wa soko huria ambapo Sekta Binafsi inashughulikia uzalishaji wa biashara ya mifugo, uagizaji na usambazaji wa madawa ya kinga na tiba.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kudhibiti viwango katika Vituo vya kutotolea vifaranga na Vituo vya kuzalisha mbegu bora za mifugo kutasaidia sana kupatikana mifugo iliyo bora lakini pia na udhibiti wa ueneaji wa magonjwa ya mifugo kupitia vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliowekwa katika sheria hii wa usafirishaji wa mifugo na mazao yake na vyombo vinavyohusika na usafirishaji ni jambo la msingi na la muhimu kabisa, siyo tu kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo bali pia kulinda soko la mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imeona kwamba Muswada huu umezingatia sheria na kanuni mbalimbali za Kimataifa zinazohusiana na biashara za Kimataifa, udhibiti wa magonjwa ya mifugo na kadhalika. Jambo hili lina umuhimu wake katika kukuza soko la nje kwa bidhaa zetu za mifugo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa kwa baadhi ya wafugaji kwamba baadhi ya madawa yanayouzwa katika maduka ya watu binafsi yamepita muda wake wa matumizi. Aidha, baadhi ya madawa huuzwa ghali sana, kwa hiyo Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kwamba hatua madhubuti zichukuliwe kuandaa utaratibu ambao utawadhibiti ipasavyo wauza madawa wadanganyifu. Aidha, utaratibu uandaliwe utakaowezesha wanaoagiza madawa na kuuza kwa wafugaji waweze kuuza madawa hayo kwa bei ambazo mfugaji atazimudu.

Mheshimiwa Spika, kadhalika kanuni zitakapotungwa zieleze bayana kuwaelekeza waagizaji madawa kutoka nje ya nchi wawe wanaagiza madawa yenye ubora wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba mikakati madhubuti iwekwe kudhibiti usafirishaji wa mifugo, si tu kwa kupunguza kuenea kwa magonjwa pekee bali pia kuwapunguzia wanyama hao usumbufu na maumivu yasiyo ya lazima. Suala la fidia kwa mfugaji kutokana na uzembe wa kiutendaji ambao utasababisha kifo au kujeruhiwa kwa mnyama, Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali kueleza bayana atakayehusika kulipa fidia hiyo. Aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba fidia zinalipwa kwa uadilifu na mapema iwezekanavyo ili kumwondolea usumbufu mfugaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaunga mkono Muswada huu na inaliomba Bunge lako Tukufu kuupitisha. Naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaingia kwenye mjadala wa jumla, ninao wasemaji wanane. Naanza na Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, atafuatia Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella na Mheshimiwa Njelu Kasaka ajiandae.

**MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Pili, nitoe pongezi kwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na safu yake nzima ya Watendaji kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba kimsingi sina tatizo na Muswada huu unaojaribu kuweka utaratibu na sheria za kuzuia kudhibiti na kuratibu uenezaji wa magonjwa ya mifugo. Kimsingi sina tatizo nalo. Isipokuwa naomba tu ieleweke kwamba katika nchi hii tuna aina mbili za wafugaji. Tuna ufugaji wa kisasa na tuna ufugaji wa kiasili. Kwa ufugaji wa kisasa nadhani sheria hii inawafaa sana wale ambao wanafanya ufugaji kwa utaratibu huo. Lakini kwa wafugaji wa asili, wengine wanawaita wachungaji, mimi sikubaliani na jina hilo, napenda kuwaita wafugaji wa asili.

Kwa kweli naona sheria hii ina matatizo makubwa mawili. Tatizo la kwanza mimi naona sheria hii inatazama mifugo kama zao tu la biashara na sio vinginevyo na mimi nachelea kukubaliana na hilo. Mifugo kwa wafugaji sio zao tu la biashara, ni zaidi ya zao la biashara. Ni sehemu ya maisha na utamaduni wao na sheria hii haigusii mambo hayo. *(Makofi)*

Naomba kutoa mfano mdogo kwenye miaka ya 1950 mzungu mmoja aliuawa mnadani, sehemu za Loliondo, aliuawa kwa sababu alimlazimisha mzee mmoja wa Kimasai kumwuza ng'ombe ambaye yeye hakutaka kumwuza na hakutaka kumwuuza kwa sababu alikuwa na pembe kubwa, alikuwa na rangi nzuri, alikuwa anavutia kumtazama, alifahamu tabia yake na kadhalika. Kwa hiyo, hakuwa tayari kumwuuza.

Lakini kwa macho ya yule mzungu jina lake nalihifadhi, aliona kwamba huyo akiuzwa ndiyo atakuwa na bei nzuri. Wakabishana pale, yule mzee akaamka, akamchoma mkuki akafa na yeye akachukuliwa akahukumiwa na hatimaye akanyongwa. Ninachojaribu kuelezea hapa kuna mitazamo tofauti. Kwa mitazamo ya sheria hii ng'ombe ni zao tu la biashara na siyo zaidi na kwa wafugaji sehemu kubwa ya ufugaji wa asilia ng'ombe na mifugo hiyo siyo zao tu la biashara ni zaidi na sheria hii haijaribu kutazama hilo.

Kwa hiyo, mimi naona ni upungufu mmoja mkubwa wa sheria hii. Ningefurahi sana kama kabla ya kuleta sheria ya namna hii Bungeni, tungejaribu kufanya jitihada za kuwafundisha na kuwaelimisha hao wafugaji wa asili ambao ndiyo sehemu kubwa ya wafugaji wetu, kujaribu kubadilisha mawazo na mitazamo yao. Sasa tukileta na kupitisha sheria kabla ya kubadilisha mitazamo yao tutakumbana na tatizo kama yule mzungu alilokumbana nalo.

Mfano wa kwanza, mimi naona sheria hii ina ugumu wa kiutekelezaji. Ni vigumu sana kuitekeleza hii sheria. Nasema hivyo kwa sababu wote tunaafikiri kwamba sehemu kubwa ya wafugaji wa asilia wa nchi hii wanaishi vijijini. Maeneo ambapo hamna usafiri wa magari, usafiri mkubwa ni usafiri wa kutumia miguu. Sasa ukijaribu kutekeleza sheria hii nitoe tu mifano michache, kuna yale magonjwa ambayo yanahitaji kutolewa taarifa. Kwa muda wa saa 24, Mheshimiwa Edward Lowassa anafahamu, kutoka kijiji

cha Pinyinyi Wilayani Ngorongoro kwenda Loliondo kutoa taarifa, hamna usafiri wa gari, kwa mguu utatembea siku mbili mpaka tatu. Je, utaweza kutoa hiyo taarifa kwa masaa 24 au 48? Haiwezekani hata kidogo.

Mfano wa pili, ni hili tatizo la kuweka *barriers.* Umesema ng'ombe au mifugo wasichungwe mita 200 kutoka barabarani. Ni vizuri kueleza hivyo lakini kiutendaji na kiutekelezaji sijui kama inawezekana. Kwa sababu baadhi ya wafugaji wetu huko kijijini kutoka kwenye maboma yao, makazi yao kwenda maeneo ya malisho ni lazima uvuke barabara kwa kwenda na uvuke barabara wakati wa kurudi. Sasa wanapofanya hivyo si watawekwa hatiani mbele ya sheria hii kwamba wamechunga mifugo kwenye maeneo ya barabara mita 200? Bado naona sheria hii ni vigumu sana kiutekelezaji kuifuatilia.

Mfano wa tatu, haya masuala ya *Buffer Zones.* Nafikiri kimsingi ni jambo zuri lakini bado naona kiutendaji na kiutekelezaji kuna tatizo. Kwa sababu dawa za chanjo wote tunafahamu kwamba haziji kwa wakati zinapotakikana, kama tungeweza kupata dawa za chanjo kwa muda unaotakikana, tungeweza kusema kwamba hili lingetekelezeka. Lakini uzoefu unaonyesha kwamba dawa hizo haziji kwa wakati kwa hiyo itakuwa vile vile vigumu kutekeleza kipengele cha sheria hii na mfano wa nne, *compulsory identification.* Mimi ningependa hili lifafanuliwe, kwa sababu kila jamii, kila mtu ana utaratibu wa kuweka ng'ombe au mifugo yake alama ili aweze kuwafahamu na wasipotee. Wengine ama wanakata, kuchanja masikio, wengine wanachoma moto, na wengine wanatumia alama mbalimbali. Sasa kwa *compulsory identification* bado ni dhana ile ile kwamba huyu ng'ombe, huyu mnyama ni zao la biashara na siyo vinginevyo. Kama unavyofungasha kwa robota za kahawa na kupiga muhuri na hawa ng'ombe hali kadhalika, hii mifugo vile vile tuwaweke na kuwapiga *identification marks* kwa utaratibu huu.

Lakini bado mimi ninasisitiza elimu ni lazima itolewe vinginevyo itakuwa vigumu sana kutekeleza sheria hii kwa sababu mtazamo wa sheria hii tunatofautiana sana na mitazamo ya wananchi wafugaji walio vijijini.

Kwa wafugaji wengi wa asili, mifugo yao siyo lazima hata umweke alama, unamfahamu kwa rangi, unamfahamu kwa jina, unamfahamu kwa ukubwa. Kwa hiyo, siyo suala tu kupiga muhuri kama marobota ya kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kusisitiza tu kwamba ninaona matatizo haya mawili katika utekelezaji wa sheria hii. Moja ni ule wa mtazamo na pili kiutekelezaji kwa sehemu kubwa ya wananchi wetu vijijini maeneo ambapo hapana usafiri, kutakuwa na ugumu wa kutoa taarifa hizo kwa kipindi cha saa 24 au 48.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu ambao nafikiria kwamba umekuja kwa wakati muafaka na ninaunga mkono moja kwa moja kabla sijatoa mchango wangu. *(Makofi)*

Muswada huu kitu muhimu ambacho kimefanyika ni kuangalia hali ya mazingira katika dunia ya leo na kujaribu pia kuyaingiza katika Muswada huu, na hili ni suala la muhimu la kutafsiri utandawazi ambao hatuwezi kuukwepa hasa unapokuja kwenye *genetrical engineering* na unapokuja kwenye masuala mengine ambayo sasa biashara inavuka mipaka ya dunia yetu. Na kama tutataka kuwa washindani katika biashara ya dunia katika eneo hili ambalo kwa muda mrefu tumelipuuza nadhani ni muhimu tuwe na Muswada kama huu.

Lakini pia ningependa niungane mkono na mzungumzaji aliyekaa ya kwamba Muswada huu unahitaji elimu ya kutosha. Kwa hiyo, labda pendekezo langu kwa Waziri ni kwamba ajitahidi katika Bajeti ijayo awe ameongeza Bajeti yake ya *extension* kwa ajili ya wafugaji. Kwa sababu ukiangalia wafugaji katika taifa hili wako katika maeneo mengi na idadi yao ni kubwa na Muswada muhimu kama huu kama utatekelezwa kama sheria bila wao kuwa wameelimishwa vya kutosha kuna mambo yanayoweza kutokea.

Moja wanaweza Sheria hii ikatumika kuwakandamiza. Kwa mfano, katika kipengele cha *compensation* katika kulipwa. Wanaweza, tumeona upande wa madini, watu hata hawajalipwa pesa zao za madini. Kwa hiyo, inawezekana watu, mifugo ikateketezwa na bado pesa zikapelekwa wasiweze kulipwa.

Kwa hiyo, nafikiri ya kwamba Waziri alifikirie sana hili kwa makini. Elimu itolewe na itolewe vijijini, siyo kwa watendaji wa Mikoa na Wilaya kwa sababu semina nyingi zinaishia kwa watendaji, Mikoani, Wilayani na hazifikii wananchi na wafugaji wako vijijini, wako katika Mikoa ya Arusha, Mikoa ya Mwanza, Mikoa ya Shinyanga, Mikoa ya Mara, Mbeya na mahali pengine na mahali pote hapa wafugaji ni watu ambao mara nyingi hujaona hata kwenye semina.

Mimi sijaona hata semina za wafugaji hasa wanaofuga ng'ombe wakaitwa. Kwa sababu hata kwetu kule Ukerewe tunao wafugaji ambao ni wa mfano, sijaona hata siku moja wameitwa kwenye semina. Lakini ziko semina nyingi sana zinazohusiana na ufugaji. Hilo moja. Kwa hiyo, elimu itolewe Waziri alete kwenye Bajeti tuone kwamba kuna njia mahsusi ya kuwafikia hawa wafugaji na hii elimu itolewe kwa wafugaji wote.

La pili katika suala la elimu, ni lile la magonjwa. Sheria hii itakapokuwa imepita, inataka magonjwa yaainishwe, yaorodheshwe. Haya nayo inahitaji kufikishwa mpaka kwa wafugaji wenyewe ili waweze kujua ni aina gani ya magonjwa na kuwe na vijigazeti vya kanda vinavyotolewa ili waweze kupata kila wakati kufahamu ni magonjwa gani ambayo yameingia katika maeneo yao.

Nadhani ni haki ya wafugaji kupata taarifa hizi ili wakaweze kujiandaa. Lakini kuna nyingine ambayo nafikiria inahusu pia elimu kwa sisi wote. Magonjwa mengine kama *tuberculosis* (magonjwa ya kifua kikuu). Ng'ombe kupitia kwenye maziwa watu wengi wanaweza kupata magonjwa ya kifua kikuu na hii inahitaji kuoainishwa kati ya Wizara hizi mbili kwa sababu sasa hivi Wizara ya Afya, kwa kushirikiana na mikakati ya kiulimwengu ambayo ipo ya kuondoa *malaria, tuberculosis* nadhani wangeweza

kushirikiana kuona pia kwamba wakati wenzao wa Afya wanakazana kuondoa ugonjwa wa kifua kikuu isije kupitia kwenye ng'ombe tena wakawa wanapata maambukizi haya. Ni kweli kwamba ugonjwa wa kifua kikuu unaenea kwa kasi sasa hivi kutokana na virusi na udhaifu unaosababishwa na virusi vya ukimwi lakini inawezekana kabisa bado kuna sehemu kubwa ambayo inaenea kutokana na utumiaji wa maziwa ambayo hayakudhibitiwa hasa maziwa haya ambayo yananunuliwa kutoka kwa wafugaji wanaofuga ng'ombe wawili au watatu kwa biashara ya kukimu familia.

Napenda sasa nitoe mchango mwingine kuhusu uwezo wa Serikali za Mitaa. Inavyoelekea katika Muswada huu ni kwamba mategemeo makubwa ya Wizara hii itakuwa ni Serikali za Mitaa. Lakini mimi ninayo maswali ya kuuliza. Je, Wizara hii kweli imeangalia uwezo wa Serikali za Mitaa katika pesa walizonazo, wataalam walioko kwenye Serikali za Mitaa kuweza kuhimili na kumudu kazi kubwa ambayo imeonyeshwa katika Muswada huu?

Mimi nina mashaka kabisa. Huko tuliko vijijini wataalam ambao wanaweza kuhimili kazi itakayokuwa imeletwa na kupitishwa kwa Muswada huu mimi naona hawapo, pesa hizo hazipo.

Lakini hili eneo la mifugo ni eneo kubwa ambalo tusingeliachia tu *Local Government* tungefanya kama tulivyofanya Elimu. Elimu tungeachia *Local Government* peke yake nadhani tungechukua muda mrefu kabla hatujaweza kuboresha elimu. Lakini kuna kipengele ambacho ni cha *Local Government* lakini kuna vipengele ambavyo ni vya wazi wazi ambavyo vinahudumiwa na Serikali Kuu. Kwa hiyo, wakati haujafika kabisa wa kutegemea *Local Government.*

Mimi ningependa hata kwa mfano majosho, tutumie mfano, tuliotumia kwenye Elimu. Kwa nini Wizara inayohusika isihakikishe kwamba ina utaratibu unaofahamika wa kutengeneza majosho na kuna sehemu ambayo imeainishwa kutoka Serikali Kuu na *Local Government* na Vijiji kama tulivyofanya katika ujenzi wa madarasa, ili tuweze kutoa huduma kwa ajili ya mifugo eneo ambalo nadhani kwa uchumi wetu ina mchango mkubwa. Mara nyingi wale ambao hawatoki, watu wengine hawaelewi umuhimu wa mifugo. Nchi hii, kama wafugaji hata hawa wachungaji, wangekuwa hawakutimiza wajibu wao, tungekuwa na upungufu mkubwa wa nyama na katika nchi hii hatujaingiza nyama ku-*import* kutoka nchi za nje, tunatumia hapa ndipo tunapojitegemea.

Kwa hiyo, mimi sioni tatizo kwa nini tusiweze kuweka nguvu kubwa katika eneo ambalo tumeshashinda. Hapa tumeshinda tumeweza kujitegemea kula nyama zetu, kula nyama za ng'ombe ambazo zinafungwa na wafugaji wetu kwa hiyo, ni lazima tuweke nguvu zaidi katika eneo hili ambalo tumeshinda. Katika kilimo cha nafaka bado kuna wakati ambao tunaingiza nafaka zinazotoka nje. Lakini hili ni eneo ambalo kwa kweli tumepata ushindi.

Ningependa sasa nizungumzie kwa kutumia mfano tu, katika suala la kudhibiti na kutengeneza *disease free zone.* Mimi nafikiria *disease free zone* yaani eneo ambalo linaonekana halina magonjwa halitatokana tu na kungoja mpaka itangazwe. Linapaswa

kuundwa, kuungiwa mazingira ya kwamba tunaweza kwenda hatua kwa hatua tunasema eneo hili sasa tumeliundia mazingira ya kulifanya *disease free zone.* Ni eneo ambalo halina magonjwa na mimi ningependa kushauri ya kwamba kama Waziri ataliona vizuri atumie Wilaya ya Ukerewe kama mfano. *(Makofi)*

Wilaya hii ina mazingira ambayo unaweza kabisa ukaondoa magonjwa ya mifugo. Kwa sababu ya kuwa ni visiwa na ni kwamba unaweza kudhibiti uingizaji wa mifugo. Kwa hiyo, ningemwomba tu Mheshimiwa Waziri akalifikiria hilo basi aongeze nguvu kidogo tu ili tuweze kuwa mfano katika kusema ya kwamba unapokuwa unahitaji kuwa na *disease free zone* hatua hizi zinaweza zikatumika na pili ningependa Mheshimiwa Waziri pia afikirie namna ya kutumia ujuzi wa asili wa mifugo.

Kwa sababu mpaka sasa tunazungumza juu ya dawa kuletwa. Lakini hatujafika mahali ambapo tukasema je, katika jamii ya Kimasai ambao wamefuga miaka nenda rudi, hawajui dawa za kienyeji ambazo tungeweza kuziendeleza katika kutibu magonjwa ya mifugo ili tufike mahali tuondoe utegemezi wa madawa haya ambayo tunaletewa kutoka nje na tukaweka kituo maalum.

Nataka kusema kwamba sasa hivi yamekuwepo makubaliano na tuliridhia mkataba huo katika Bunge hili la *Traditional Medicines.* Mimi nadhani tunaweza tukatekeleza sasa kwa kuanzia kwenye mifugo ya kwamba kuna watu ambao wana ujuzi huo mfano mmoja ni Wamasai lakini ningependa kusema katika Wilaya ya Ukerewe tunacho kisiwa cha Ukara ambacho kwa miaka mingi kimekuwa kikitumia *zero grazing* na wana zao za kuzuia kuenea kwa magonjwa na wana wanyama wazuri tu na ningemkaribisha tu Mheshimiwa Waziri akipata nafasi aje awatembelee wakala aone namna nyingine ya ufugaji, mimi nauwita wa kisasa pamoja na kwamba ni wa asili. *Zero grazing* ambao wanaweza kutoa mifugo mizuri na wanawatunza kuliko hata wanavyoangalia vitu vingine katika maisha yao na ninakubaliana ya kwamba ufugaji una sehemu ya utamaduni.

Kwa sababu wao wanahusisha mifugo na chakula kingine. Mifugo inawapa mbolea na wanaweza kupata chakula kingine. Baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono tena Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi na mimi nitoe machache kuhusiana na Muswada huu.

Kwanza kabisa naunga mkono Muswada na naipongeza Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla kuja na Muswada mzuri kama huu ambao unaangalia Sekta ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya Mifugo kwa kipindi kirefu imekuwa katika mazingira ambayo kidogo si mazuri kiasi kwamba mchango wa Sekta hiyo katika uchumi wa nchi na hata katika kuboresha maisha ya wananchi na kuondoa umaskini umekuwa bado ni mdogo kwa sababu Sekta yenyewe haijaangaliwa ipasavyo. Nadhani kwa Muswada huu pamoja na Miswada mingine ambayo imeletwa na Serikali kusema Sekta hii itachangia katika eneo hilo.

Moja ya mambo muhimu Mheshimiwa Spika, ambayo yanaweza kuchangia vizuri katika kuzuia mambo ya magonjwa ni upatikanaji wa maji. Kwa sasa hivi unapozungumza katika Sekta ya Mifugo haya mambo ya maradhi na magonjwa pamoja na usafirishaji wa mifugo, kwa kiwango kikubwa unachangiwa na kukosekana kwa maji katika maeneo mengi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iliangalie suala hili kwa umakini sana katika sehemu mbili.

Kwanza, hawa wafugaji wanahama hama kufuata maji. Kwa maana hiyo, wanapohama ndipo wanaposafirisha mifugo na mifugo kama kuna maradhi basi maradhi hayo yanaenezwa katika sehemu mbalimbali kutokana na kusafiri kwa mifugo kutoka eneo moja kwenda eneo lingine.

Sehemu ya pili ya suala hilo ni maji wanayokunywa mifugo wenyewe. Maji mengi ni machafu na ni tope. Unakuta maji wanayokunywa mengine yamebadilika na rangi yamekuwa rangi ya kijani. Lakini ng'ombe wanapelekwa pale kwenda kunywa hayo maji. Halafu unategemea ng'ombe wawe na afya nzuri, wasiwe na maradhi. Itawezekana wapi.

Ni jambo la fikiri, Serikali tunapozungumza juu ya kuendeleza sekta ya mifugo tunazungumza juu ya kudhibiti maradhi, basi tuanzie katika vyanzo vinavyosababisha maradhi hayo. Mojawapo ni hili suala la kuwapa ng'ombe maji machafu wanakunywa na wakati mwingine ni tope tupu. *(Makofi)*

Suala lingine linaloambatana na hilo, zamani kulikuwa na njia za mifugo, kwamba watu wanaweza kusafirisha ng'ombe kutoka eneo fulani kwenda lingine kwa kupitia njia maalum ambazo zilikuwa zimeandaliwa na Wizara ya Kilimo na Chakula. Leo njia hizo katika sehemu nyingi hazipo, kulikuwa na mradi ule wa kuendeleza masoko na njia za mifugo, sehemu kubwa ilikuwa ni upande wa Kaskazini, sielewi kwa kiasi gani umefanikiwa lakini katika maeneo mengi ya Kusini mwa Tanzania njia za mifugo hazipo.

Ng'ombe wanasafirishwa kwenye barabara na wanapita kwenye majumba ya watu kwenye vijiji vya watu na wanapita mpaka kwenye mashamba na kiasi kwamba wanaanza kugombana kati ya wafugaji na wenye mashamba hayo. Sasa nilikuwa nafikiria kwamba hili suala la njia za mifugo limeishia wapi na limefikia wapi. Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba hizi njia za mifugo zipo.

Kwa sasa hivi baadhi ya njia za mifugo ambazo nilikuwa nazifahamu zamani watu wamejenga nyumba kwenye njia za mifugo. Katika maeneo ambayo walikuwa wanaita *holding grounds* watu wameshayachukua wamejenga makazi yao humo. Sasa Serikali inachukua hatua gani katika kurekebisha hayo mambo ili tuweze kuwa na uhakika kwamba katika utekelezaji wa sheria hakutakuwa na migogoro na utekelezaji ambapo utakuwa ni nzuri ili uweze kuleta mafanikio tunayokusudia kuyapata.

Kuna suala lingine hapa ambalo tutalikuta Mheshimiwa Spika, ni usimamizi na usimamizi wa haya tunayoyapanga hapa, tunayoyatungia sheria hapa, utategemea sana

kuwepo kwa miundombinu nyingine ambayo itawafanya wale wasimamizi waweze kupata urahisi wa kusimamia. Vinginevyo wasimamizi watakaokabidhiwa kazi hizo watashindwa kutokana na mazingira magumu ya kufanyia kazi.

Katika suala hilo hilo Mheshimiwa Spika, kuna suala la majosho. Mheshimiwa Waziri wa Maji na Mifugo alipokuwa anawasilisha bajeti yake mwaka huu hapa Bungeni alitaja, alitoa idadi kubwa sana ya majosho. Lakini mengi ya majosho hayo yalikuwa hayafanyi kazi ni machache tu ndiyo yaliyokuwa yanafanya kazi na hili eneo amesema litakuwa ni la sekta ya binafsi.

Sasa mimi nilitaka nijiulize tunapofika mahali, suala la mifugo ni la muhimu na linachangia sekta binafsi na sekta binafsi haijajitokeza. Tunafanya nini? Tunaacha tu kwamba hiyo sekta basi iendelee kuharibika hivyo kwa sababu sekta binafsi haijajitokeza? Sisi tumeamua kujitoa, au tunabuni mbinu nyingine itakayosaidia kuleta huduma hizo hizo hadi hapo watakapojitokeza watu binafsi na kuchukua maeneo hayo. Haiwezekani tukasema kwamba maadam hii ni eneo la sekta binafsi hata kama hawapo basi tuache mifugo iendelee kukaa katika hali ya mazingira machafu, mazingira ya magonjwa mbalimbali ambayo mengine yanaweza kutibiwa kwa urahisi kwa kuwepo kwa majosho na mpaka sasa hivi biashara ya mifugo kwa Tanzania pamoja na kwamba ni nchi ya tatu katika Afrika kuwa na mifugo mingi hatujafanikiwa kuwa na biashara nzuri kupeleka nyama nje kutokana na maradhi mbalimbali.

Moja ya matatizo yetu ni kukosekana kwa majosho. Je, Serikali inachukua mikakati gani, inaandaa nini kuona kwamba hilo pengo kati ya kujitoa kwa Serikali na mikakati ya hawa watu binafsi kabla hawajajiingiza nini kinafanyika kuhakikisha kwamba mifugo iko katika hali nzuri. Hili tungependa labda Mheshimiwa Waziri atusaidie katika kufafanua baadhi ya mambo kama hayo.

Suala lingine ni lile linalosababisha na migogoro kati ya wafugaji na wakulima, Chunya kwa mfano. Tumekuwa na migogoro mikubwa sana katika bonde la Songwe, bonde la Ziwa Rukwa ndani ya Wilaya ya Chunya kati ya Wafugaji na wakulima. Tafrani yenyewe inatokana na maji. Wafugaji wanafuata maji na wakulima wakati wa kiangazi wanakwenda kulima bustani zao kwenye maeneo ya maji. Kwa hiyo, mifugo inapokwenda kunywa maji wanakula na mazao yaliyopandwa na wakulima. Sasa Serikali ilitoa maelekezo ambayo tuliyazingatia kwamba Serikali za Wilaya zijaribu kutenganisha kati ya wafugaji na wakulima. Serikali ya Wilaya wakishirikiana na Mkoa wa Mbeya wakafanya juhudi wakawatenganisha kati ya wafugaji na wakulima. Lakini suala kubwa ilikuwa ni kwamba maji yapatikane katika maeneo yale ambapo mifugo inapelekwa.

Waziri wa Mifugo alikuja Chunya mwaka jana tukamweleza tatizo hilo akaliona na tukamkabidhi mapendekezo yetu na tukamwelekeza hata maeneo ambayo tulikuwa tunafikiri kujenga majosho akasema hili suala tukumbushane tukiwa kwenye Bajeti inayokuja. Tukakubaliana, baadaye nilipomkumbusha akasema anaweka kwenye Bajeti. Ilipokuja bajeti ile programu ile haimo ndani ya Bajeti.

Sasa kwa hiyo, tunajikuta sisi tunarudi pale pale, kuna wafugaji wanataka kurudi kwenye maeneo ya mabonde ambapo wakulima hawapo na tutawazuiaje katika mazingira kama hayo.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri utusaidie Halmashauri za Wilaya zinafanya kazi yake wakati mwingine muone mnapozielekeza zinafanya kazi ambayo Serikali imesema. Lakini tunafika mahali tunakwama. Kwa sababu ile *response* ya pili haipo. Sasa sisi tufanyeje. Sasa leo huu ugomvi umeanza tena. Ugomvi umeanza tena leo hii kwenye kipindi cha Majira Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, kwanza alikwenda Chunya, akaagiza kwamba wafugaji watoke tena katika maeneo hayo. Lakini hawawezi kwenda kule kwa sababu hakuna maji. Pili, ametoa leo agizo lingine kwamba atawakamata wanaopitisha ng’ombe wao barabarani. Lakini kwa sababu hakuna njia za mifugo, watapita wapi? Kwa hiyo, tutakuwa tunarudi pale pale kwamba lazima kazi zifanywe na Serikali kwa umakini zaidi katika suala la kuangalia mifugo, tunapambana na maradhi lakini kuna vianzo vya maradhi vinavyosababisha migogoro mbalimbali tuvishughulikie kwanza ili tuweze kupata mafanikio katika hili jambo ambalo tunalikusudia.

Sasa tunakuja kwenye suala la usimamizi. Je, Mheshimiwa Waziri haya mambo yote ambayo umeyazungumza kwenye huu Muswada nzuri sana, mambo mengi tumeyazungumza. Mmejiandaa vipi kuhakikisha kwamba kweli mnayasimamia. Kwa sababu baadhi ya haya mambo mliyoyaandika hapa, yapo hata sasa hivi. Hii sheria ambayo itakuwa *repealed* ilikuwa inayataja haya mambo kwamba yatasimamiwa. Lakini hayajasimamiwa, katika baadhi ya vijiji vingi Mabwana Mifugo hawapo. Ng’ombe wanachinjwa. Lakini upungufu wa Mabwana Mifugo sehemu za vijiji ni mkubwa ambao tunao. Na hili nalo lazima liangaliwe kwa sababu haya ni mambo ambayo na Mheshimiwa Mathew Ole-Timan hapa alikuwa anazungumza kwamba kutoa ripoti mbali kabisa kutoka kijijini kwenda kwa miguu akatoe ripoti itakuwa ni vigumu.

Inabidi hapa Bwana Mifugo wawe katika maeneo jirani ili taarifa ziweze kufikishwa kule. Lakini bado katika Wilaya kama Chunya ambayo ni kubwa sana kutoka baadhi ya Vijiji kwenda Wilayani ni kilomita 150 mpaka 200. Kwa hiyo, hata kama mkulima atampelekea Bwana Mifugo taarifa ili Bwana Mifugo aifikishe kwenye Wilaya itachukua zaidi ya wiki moja au zaidi kabla hajaifikisha hiyo taarifa kwenye Wilaya. Kule kuna tatizo kubwa ambalo inabidi ninyi mulifikirie ikiwa ni pamoja labda kuwapa usafiri hawa Mabwana Mifugo ambao wanakaa mbali sana kutoka Halmashauri za Wilaya au Makao Makuu ya Wilaya. Kwa hiyo, tunauhakika kwamba atakapopata taarifa hizo basi aweze kusafiri kwa urahisi kufika kwenye eneo la Wilaya akatoe hizo taarifa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nadhani katika eneo la usimamizi litabidi nalo mlifanyie kazi kabisa. Vinginevyo mambo mengi mazuri ambayo yamo katika Muswada huu hayataweza kutekelezwa na kwa lugha nyingine hayatatekelekeza.Tunazo sheria nyingi ambazo hazitekelezeki au hazitekelezwi kikamilifu. Ninakumbuka katika Bunge hili hili tulipitisha sheria Mheshimiwa Spika, tukasema madreva wa magari wasiendeshe pembeni mwa barabara yaani nje kidogo ambako wanapita watembea kwa miguu,

tukapitisha sheria hapa. Leo Dar es Salaam kuna madaladala yanapita kila upande wa barabara. *(Kicheko)*

Nikamwuliza *Attorney General* labda unaliona hili? Akasema wala siyo hilo tu, Sheria nyingi tu zinavunjwa. Basi ndiyo hali hiyo. Kwa hiyo, kama hali ndiyo hiyo, tutatunga sheria hizi tunaweza tukafika mahala tukawa hatuna hata njia za kuzisimamia na kuzitekeleza. Kwa hiyo, naomba sana kwamba usimamizi na mkakati mzima uandaliwe ili sheria hii ambayo ni mzuri ambayo mimi mwenyewe naiunga mkono basi iweze kutekelezwa kikamilifu na sisi huko Chunya hili suala la mifugo wakati wa kutekeleza wafugaji na wakulima na itakuwa ni njia mojawapo ya ku-*control* matumizi mabaya kwenye barabara na pia kuondoa magonjwa mbalimbali basi lishughulikiwe siyo kwamba hali tuliyopewa mwaka jana halafu baadaye ikaishia hewani.

Mheshimiwa Spika na mimi naunga mkono hoja hii ipitishwe, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Muswada huu. Kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka. Kwa sababu Muswada huu kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kwamba, Muswada huu ni wa toka mwaka 1940 na ukarekebishwa mwaka 1960. Kimsingi ni kwamba kwa kweli umepitwa na wakati.

Napongeza kwa sababu mengi ambayo yako kwenye Muswada ni mambo ambayo yanajaribu kudhibiti hali halisi ya magonjwa ya mifugo katika nchi yetu. Kwa kweli nampongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Wataalam wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Muswada huu wote umejielekeza katika masuala ya msingi hasa udhibiti wa magonjwa mbalimbali ya mifugo, ambayo ndiyo tatizo sugu ambalo tunalo, hakuna asiyetambua umuhimu wa mifugo katika nchi yetu au wanyama katika nchi yetu. Lakini nakumbuka wakati tunajadili Muswada huu, Mheshimiwa Waziri, alitueleza mambo mazito sana kwamba, moja ya tatizo la Tanzania ni kwamba, tuna mifugo zaidi ya milioni 15 lakini hatufaidiki kwa Pato la Taifa kutokana na mifugo yetu. Kuna nchi kama Botswana ambayo ina ng'ombe milioni tano lakini wanapata Pato la Taifa kutokana na ng'ombe. Sasa Muswada huu kwa kweli umelenga katika kuboresha kuona ya kwamba na sisi Watanzania tunaofuga tunaboreka na kupata pato na pia kupata Pato la Taifa. Kwa hiyo, napenda kuupongeza sana Muswada huu na sina sababu ya kutokuunga mkono. Kwa hiyo, napenda kuunga mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri katika mambo ya msingi ambayo nimeyaona katika Muswada huu. La kwanza ambalo naomba nitoe ushauri ni kwamba, Mheshimiwa Waziri wakati anaelezea alizungumzia suala zito kwamba kuna Waraka Na. 1 ambao ulitolewa na Mheshimiwa Rais mwaka 2000 lakini wakati anaeleza haya na Sheria hii, Waraka ulianza na Sheria hii sasa ikaboreshwa lakini utekelezaji wake kwa kweli ni mgumu sana, sijui atafanyaje?

Mheshimiwa Spika, yapo masuala ambayo itabidi Mheshimiwa Waziri, awe imara ili aweze kufanikiwa kwa sababu kwa mfano, haya yote ya Waraka Na. 1 namwomba Mheshimiwa Waziri, anieleze ni Wilaya ipi ambayo imetekeleza haya, ni Wilaya ipi ambayo imetekeleza yote ambayo Mheshimiwa Rais, ameyaeleza kwa sababu yapo masuala ambayo yametolewa Waraka lakini utekelezaji wake haupo? Leo tunatunga Sheria, sasa Sheria na Waraka, sawa Sheria ni nzito Waraka siyo mzito lakini ni yale yale ambayo tumesema katika Waraka itabidi sasa Waraka huu ufutike hata kama haufutiki lakini yameingizwe kwenye Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nayasema hayo kwa kweli kwa sababu yapo masuala mengi sana ambayo yanatakiwa yatekelezwe na Halmashauri zetu lakini hakuna hata moja ambalo limetekelezwa. Je, sasa tunatunga Sheria hii kwa faida ipi? Ni mifano mingi, nakumbuka nilichangia, wanasema kila Halmashauri ya Wilaya ifungue Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo kwa kutenga asilimia isiyopungua 15 ya mapato yote yanayotokana na mifugo na kutoa taarifa za mapato na matumizi ya Mfuko huo kwenye Vikao vya Halmashauri. Je, inatendeka? Hakuna. Kila Halmashauri ya Wilaya iwe na mipango ya kuimarisha Sekta Binafsi juu ya wajibu wao wa kusambaza madawa na kutoa matibabu ya mifugo, wanafanya? Hakuna. Yaani ukisoma yote yale ni kwamba, hakuna hata kimoja ambacho kinatekelezwa. Leo tumeunda hii Sheria nzuri lakini je utekelezaji wake utakuwa wa namna gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri pamoja na kutunga Sheria lakini utekelezaji lazima uwe unatekelezeka. Nalisema hili, nilimwambia Mheshimiwa Waziri, kwa mfano, inasema kila Halmashauri itunge Sheria ndogo ndogo za kuimarisha usimamizi wa minada na usambazaji wa mifugo, kuanzia sasa utaratibu wa kuswaga mifugo kwenye maeneo yenye reli, barabara za lami au njia za maji, uachwe mara moja na Wakuu wa Wilaya wasaidie ufanikishaji wa suala hili; je, inafanyika? Hakuna. Hili ni tatizo na nilimwambia Mheshimiwa Waziri, kwa mfano, Mkoa wa Tanga mnada wa Jumatatu wa Korogwe ni wa Tanzania nzima, mpaka ndugu zangu wa Kiteto wanapeleka ng'ombe pale. Lakini ni jambo la kushangaza ni kwamba, ng'ombe wanaswagwa, hawapakiwi kama Waraka unavyosema, ni kwamba, ng'ombe 300 au 400 wanaswagwa, nyama yote wanayokula Zanzibar inatoka Tanga kwenye mnada wa Korogwe, ndiyo inatoka pale, wanapeleka Tanga ndiyo wanasafirisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukweli wenyewe ni kwamba, wananchi wanalalamika sana kwa sababu hatuwezi kudhibiti magonjwa kwa njia hii. Nadhani Waraka huu uliwekwa kwa madhumuni hayo hayo ili kuweza kupunguza magonjwa. Kwa hiyo, nilikuwa najaribu kusisitiza ya kwamba, Halmashauri zetu kama wenzangu Waheshimiwa Wabunge walivyozungumza, kwa kweli watimize wajibu wao. Kuna *gap* kubwa sana kati ya Wizara na Halmashauri kwa Watendaji, hawa Watendaji wa Idara ya Mifugo na Wizara huko katika Halmashauri ni vitu viwili tofauti, ni vizuri Serikali ikaliona hili kwamba, utendaji ni tofauti kabisa, utendaji wa Halmashauri zetu wale wataalam na maagizo yanayopata wanawajibika kwa nani? Hili ni tatizo ambalo lipo ambalo Wizara wangeliona na wakalifanyia kazi. Huyu Afisa Mifugo hayuko *answerable* kwa *DED* ila yuko *answerable* kwa Waziri, hiki kitendawili kiko namna gani? Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, huyu bwana yuko Wizara ya Kilimo na

Chakula kule aliko, sasa unaona pia matatizo yako hapo. Sasa ni vizuri Wizara wakakaa wakaona namna gani utendaji unaweza kufanikisha suala hili zima.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo naomba nilichangie ni kwamba, kuna usemi unaosema kinga ni bora kuliko tiba. Nadhani huu Muswada pia katika baadhi ya vipengele umeeleza wazi, kinga inaweza ikapunguza sana masuala ya kutibu mifugo kama *seriously* tunakuwa na masuala ambayo yako wazi, kwa mfano, majosho ambayo wenzetu wamezungumza. Josho ingekuwa ni kama vile tunavyosema, ukifungua Kijiji lazima kuwe na zahanati au kuwe na shule. Kwa hiyo, Serikali isisitize majosho kwamba, haiwezekani kuwe na mifugo halafu hakuna majosho, kama tunaamua kweli suala la mifugo basi tuseme ni kama vile shule au ni kama vile zahanati, josho lazima liwepo kwenye Kijiji ili wafugaji wale waogeshe mifugo yao kwa sababu ni kinga, kama ng'ombe anaogeshwa magonjwa yatapungua lakini hii kuzungumza nadharia tu kwamba, Halmashauri zifufue majosho, itafufua lini? Lazima kuwe na mkakati wa Kiserikali ambao utahakikisha ya kwamba, kweli majosho yanakuwepo katika maeneo ya mifugo ambapo ni rahisi kuweza kutekelezeka lakini hili si suala la kusema tu, ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni chanjo. Chanjo zisifanywe wakati wa dharura, inapotokea milipuko ndiyo watu wanakumbuka kuchanja matokeo yake ng'ombe wanachanjwa wanakufa, kwa mfano, unakuta ugonjwa wa kichaa cha mbwa umetokea ndiyo watu wanahangaika na sindano kuchanja, kuwe na utaratibu wa kupitia kuchanja wanyama hawa mara kwa mara kwa miezi fulani, hiyo itatusaidia kuliko wakati mambo yametokea ndiyo unaona kila mtu yuko *busy* kuhakikisha ya kwamba, wanaanza kuchanja, kuchanja iwe ni sehemu ya programu ambayo inaandaliwa kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Njelu Kasaka na mimi napenda kulisisitiza ni kwamba, katika kifungu kimoja kimetamka kuhusiana na maeneo ya uchungaji. Maeneo ya uchungaji katika kila Kijiji yajulikane, yaani iwe ni kila Kijiji kiwe kinajua kuondoa ugomvi huu ambao unatokea mara kwa mara, wajue kabisa Kijiji hiki maeneo haya ni ya kuchunguia na maeneo haya ni ya kulima ili kuondoa ugomvi ambao huwa unatokea mara kwa mara kwa masuala ya wananchi ili kuweka hali sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa nilichangie, ni suala ambalo linahusiana na dawa za mifugo, kwa kweli dawa ni ghali sana. Nilikuwa naomba tu Serikali ilione hilo kwamba, dawa za wanyama ni ghali mno, ni vizuri tukatafuta mbinu za kupunguza gharama za namna ya kuwasaidia wafugaji angalau wapate kama ruzuku ili waweze kupata msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikutaka nichangie mengi, kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati, ni hayo ambayo nilikuwa nayo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Muswada huu ambao ni muhimu sana wa kudhibiti magonjwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nakumbuka mwaka juzi kulikuwa na mkutano mkubwa sana wa wadau pale Arusha. Bahati nzuri nilipata nafasi ya kualikwa katika mkutano huo wa wafugaji. Lengo la Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo lilikuwa ni kuboresha ufugaji wetu wa Tanzania. Katika mkutano ule tulizungumzia jinsi gani ya kuboresha mifugo yetu na tulikuwa na Maazimio kwamba, katika kuboresha mifugo, ni lazima mifugo wapate maji, kulikuwa na Azimio la kuchimba mabwawa katika maeneo kame, tulikuwa na Azimio vile vile la kuhakikisha ya kwamba, vituo vya tiba katika Vijiji kwa sababu katika Vijiji vyetu kuna vituo vya tiba, viimarishwe kwani vituo vingi kwa kweli havifanyi kazi halafu vile vile kuhusu tiba na chanjo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengine, ni nchi ambayo ina mifugo mingi sana, tuna ng'ombe zaidi ya milioni kumi na saba na laki tano lakini inachangia kidogo sana pato la nchi yetu, ni asilimia 18 tu ukilinganisha na nchi ndogo ya Botswana, ambao wanachangia asilimia 40 kwa ng'ombe milioni mbili.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii kuna Idara tatu, kuna Idara ya Utafiti wa Mifugo, Idara ya Afya ya Mifugo na Idara ya Uzalishaji. Katika Idara ya Utafiti wa Mifugo, kuna Vituo vya Utafiti. Sasa lengo la kuwa na Vituo vya Utafiti ni kusaidia ule utafiti usaidie kuboresha mifugo yetu hasa katika maeneo yale ambayo kuna Vituo vya Utafiti. Mimi napenda nizipongeze Halmashauri za Wilaya zote katika Kanda ya Kati kwamba, tulikubaliana kuchangia, kila Halmashauri ya Wilaya ichangie shilingi milioni tatu ili kusaidia utafiti na wanafanywa hivyo. Kwa hiyo, tuimarishe vituo hivi ili utafiti uweze kufika kwa walengwa ili waweze kuboresha mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Idara ya Afya ya Mifugo. Sasa Idara ya Afya ya Mifugo hapa ndiyo wapo wataalam wa mifugo na wataalam wengi wa mifugo wapo Wilayani na Idara hii ndiyo inahusika zaidi na tiba na chanjo. Yapo magonjwa ya kuambukiza ambayo yanatoka kwenye mifugo kwenda kwa binadamu, kwa mfano, ugonjwa wa *anthrax*. *Anthrax* kama alivyotoa mfano Mheshimiwa Waziri, ni magonjwa ambayo yanaweza kutibika na kuzuilika kama mifugo itapatiwa chanjo. Lakini wananchi wengi Vijijini wanakula nyama bila kukaguliwa kwa sababu hatuna wataalam wa kutosha katika Vijiji, zamani kila Kijiji kilikuwa na mtaalam lakini sasa hivi wananchi wanachinja tu mifugo wanakula. Katika utaratibu wa ukaguzi wa mifugo, ni lazima tufanye *anti-mortem inspection* na *post-mortem*. Sasa *anti-mortem* ni ngumu na ya kitaalam sana, siyo kila mtu anaweza akakagua nyama, ni ya utaalam sana. *Anti-mortem inspection* inafanywa kabla mnyama hajachinjwa kuona kama ana dalili zozote zile za magonjwa kwa mfano, kama ana *poorness* au *emaciation* ili asiweze kuchinjwa. *Post-*

*mortem* mara nyingi ni kuangalia kama labda kuna *tuberculosis* au kifua kikuu kwa wanyama, ugonjwa kutoka kwa mnyama na kwenda kwa binadamu.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kushauri kwamba, Wizara ihakikishe kila Kijiji kinakuwa na hawa *Meat Inspectors*, sikubaliani kabisa kwamba, *Clinical Officers* nao wakague nyama. Kulikuwa na hoja mahali fulani nilikuta wanazungumza ya kwamba, *Clinical Officers* eti wanasomea, *meat inspection* inakuwa ni *one of the subject,* lakini siyo *Authorized Officers* wa *Meat Inspection*, wapo *Authorized Officers* ambao wanakagua nyama, Maafisa Mifugo, pamoja na Mabwana Afya wenyewe, lakini tusije kufanya makosa, *Clinical Officers* wawe *Authorized Officer*, tutakuwa tumefanya makosa.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nizungumzie vile vile katika Vituo vya Uchunguzi wa Maradhi ya Mifugo, Vituo hivi ni muhimu sana. Sasa madawa yetu mengi tunaagiza nje, naomba kutoa ushauri kwamba, madawa ambayo tunaagiza nje, yanaweza kuwa *expired,* lakini bahati mbaya unaweza kuuziwa *expired drugs* au zinakuwa na *side effect* kwa wanyama. Sasa nashauri, kwa kuwa Idara ya Mifugo ina wataalam wengi sana, muanze kufanya utafiti sasa kama inawezekana basi madawa haya yaanze kutengenezwa hapa nchini, madawa ya chanjo, pamoja na madawa ya tiba, itasaidia sana. Tusitegemee zaidi kuagiza nje tu kwa mfano, madawa ya binadamu tunatengeneza hapa nchini, kwa hiyo madawa ya mifugo tuanze kutengeneza hapa nchini ili kuepuka kuagiza madawa ambayo yame-*expire* na vile vile mengine ambayo yanaweza kuwa na *side effect* na kuleta madhara kwa wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, sikutegemea kupata nafasi, nilikuwa najiandaa kuondoka lakini sasa nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nami napenda kuungana na wenzangu, kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na timu yake, hasa kwa utafiti wa kutafuta namna ya kuimarisha mifugo yetu katika nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hapa kwa kweli ni afadhali tu niseme wasiwasi wangu, nikiwa kama mfugaji na mwakilishi wa wafugaji, jambo hili nalifahamu sana na naomba Serikali kwanza itusikilize. Kwa kweli itusikilize kwa sababu tunasema kwa niaba ya wananchi na Muswada huu ni mgumu sana kwa wafugaji. Kwanza, napenda kusema ya kwamba, kwetu wafugaji na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika maeneo ya wafugaji, hili ni tatizo kwetu kwani linawezekana likatuumiza mwaka 2005. Kuna wengine wanaosema ya kwamba, ni ukombozi lakini kwangu nasema siyo ukombozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu kwanza, haikuandaliwa kabisa, wafugaji walengwa wanaona haya ni matatizo makubwa sana kwa sababu haikuandaliwa ingetoka kwao, wangeulizwa au wangeshirikishwa. Kuna mambo mengine yanayogusa, ni mambo ambayo yako kwenye mila, kwa mfano, alama za mifugo. Alama za mifugo ni jambo ambalo lilikuwepo tangu zamani, ni alama za koo kwa mfano, ukoo wangu mimi kuanzia Wamasai walioko N'garo mpaka Kiteto, tunawafahamu ng'ombe wa kwa ukoo kwa alama hizo, nikienda N'garo na sijawahi kufika nikiwaona ng'ombe nafahamu kwamba, hawa ng'ombe ni wa ukoo wangu. Kadhalika Mheshimiwa Benedict Losurutia, hapa walioko Kenya mpaka Kiteto wanatumia hizo alama. Sasa unasema tu kwamba, hizi alama zisitumike, hilo ni jambo ambalo hata kama ni zuri kwa sababu ni suala la biashara kama alivyosema Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, lakini kwao wanaliona kwamba hilo siyo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la kuwapakia mifugo kwenye magari. Hili halikuandaliwa kwa sababu tuna minada siku hizi katika kila Kijiji, lakini hayo magari unayosema ya kwamba tuwapakie mifugo kutoka mnada A kwenda mnada B yako wapi? Kwa mfano, kuna Mnada Engaruka kwenye Jimbo la Mheshimiwa Waziri, kuna mnada mwingine Gilayi kwenye Jimbo langu na pia kuna mnada mwingine Engarenaibo kwenye Jimbo langu vile vile, ng'ombe wanatoka mnada wa Engaruka - Gilayi - Engarenaibo - Longido, magari hayo ya kusafirisha mifugo yako wapi? Sasa unatengeneza uzuri wa Muswada lakini itawaumiza wananchi wengine na huu Muswada unawatengenezea baadhi ya watendaji kuwanyanyasa wananchi, rushwa yaani wafugaji wakamatwe tu ovyo. Hilo ningeomba liangaliwe kabisa kwa sababu ni tatizo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuhama hama, wananchi hawahami tu kwa sababu wanapenda kuhama hama, wanahama kwa ajili ya matatizo, matatizo yale ndiyo yangeangaliwa kwanza. Wananchi wa Longido wamehama wako Gilayi na kila mahali mpaka kwa Mheshimiwa Elisa Mollel, wapo kwa ajili ya kutafuta maji. Wafugaji kutoka Kisongo wamehamia Manyara na ni kwa ajili ya tatizo la maji, utawazuia namna gani kama hakuna maji?

Mheshimiwa Spika, kuhusu malisho wakati wa ukame, mwaka jana mvua ilikuwa ni haba, imeonyesha katika baadhi ya maeneo na wanafuata baadhi ya hayo maeneo yaliyopata mvua, wanahamia, sasa ukisema kwamba wasihame ni tatizo. Kwa hiyo, huu ni Muswada mzuri lakini ungeandaliwa vizuri na tungezingatia kwanza matatizo yaliyopo katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda tuangalie tena suala la barabara, yaani mifugo iwe mbali na barabara. Ukiangalia barabara ya Arusha - Namanga, yote inapita kwenye malisho ya mifugo, kila mahali kuna mifugo, haiwezekani hata siku moja ukasema ya kwamba, ng'ombe wawe mbali na barabara hiyo kwa sababu inapita katikati ya malisho, maboma yako pande zote, wanavuka kutafuta maji upande mwingine vile vile malisho wanafuata upande mwingine. Kwa hiyo, katika hili bado tuangalie kwa sababu ni tatizo kubwa sana kwa kupokea na kusema kwamba ipite, nasema ipite lakini tuangalie matatizo yaliyopo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu walisema elimu itolewe kwa wafugaji. Napenda kusema ya kwamba, hilo ni muhimu sana na hilo ndiyo lingezingatiwa kabla ya Muswada huu kuletwa Bungeni, hilo ndiyo lingezingatiwa kabisa kwa sababu hilo ni muhimu. Kwa kweli tutapata malalamiko makubwa sana kutokana na Muswada huu kutoandaliwa hata kama ni mzuri.

Haukuandaliwa kwa sababu madawa ya mifugo tunayoyazungumzia tunayapata kwenye maduka ya wafanyabiashara, lakini Wizara au Serikali haijui kwamba hayo madawa ya magonjwa ya milipuko yako katika maduka hayo?

Kwa mfano, nikitoa mfano wa ugonjwa wa miguu na midomo, huu ni ugonjwa uliopo kila mwaka lakini hakuna dawa katika maduka ya wafanyabiashara, hata huo ugonjwa ukiingia kwenye mifugo hakuna dawa na Serikali inatambua hilo na wenzetu Kenya kila mwaka wanachanja chanjo ya kuzuia ugonjwa huo lakini Serikali yetu haichanji na wananchi wako tayari kabisa kulipia ndiyo maana wakati mwingine Serikali ya Kenya haitaki mifugo yetu kwenda upande wao kwa sababu mifugo yetu haina kinga, ingekuwa mnachanja kila mwaka ingekuwa afadhali, sasa wafugaji wengine wanakwenda kutafuta dawa huko Kenya ya ugonjwa huu, tunataka sana lakini Serikali haitutafutii, haituwezeshi. Kwa hiyo, mimi napenda kusema kwamba, hata haya magonjwa yaliyopo yanasababishwa na Serikali kutozingatia mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba, tunatoa mifano ya Botswana na Tanzania kwamba, Tanzania ina mifugo mingi sana lakini haiongezi Pato la Taifa. Ni kweli Botswana tunavyosikia ng'ombe wana *market* lakini ni kwamba, wamejiandaa. Sisi huwezi tu ukasema ya kwamba kila mtu hapa awe na nyumba *self-container*, huwezi, kama yangu ni kibanda ndiyo uwezo wangu. Kwa hiyo, huwezi kuwaiga Botswana kwa sababu wamejiandaa mwaka mzima na wewe ulete Sheria ya Botswana useme ya kwamba, hii ndiyo Sheria tutakayoitumia, wao wamejiandaa.

Kwa mfano, tunaposema kuhusu malisho kuwa ng'ombe wasitembee kila mahali, nikitoa mfano wa kwenye Jimbo langu kuhusu malisho ni kwamba, Kata tatu zinatumia malisho sehemu moja yaani wanatengana tu kwa maboma lakini mchana wako katika malisho eneo moja ni kwamba zaidi ya Vijiji vinane viko pamoja. Sasa hii Sheria ukiwaambia hawa watu hawakuelewi kabisa kwa sababu mimi nilikuwa najaribu kutafuta namna ya kuwaeleza wananchi kuhusu huu Muswada lakini haingii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba unilinde hasa Mawaziri ukiwaangalia huku nyuma, kutujibu kabla ya mhusika hiyo nadhani siyo Sheria. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ningependa kusema tu kwamba, hili tutalipokea lakini lina matatizo makubwa na bahati nzuri siyo kwangu tu peke yangu ila hata kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, kama itaniumiza mimi na yeye itamwumiza kwa sababu tupo Wilaya moja, wote hatuna maji na pia wote tunahama.

Kwa hiyo, mimi nataka kuiambia Serikali kwamba, wafugaji wasinyanyaswe kwa ajili ya Muswada huu kwa sababu inawezekana kesho wataanza kukamatwa kwa sababu wanaswaga ng'ombe kwenda minadani, hawana magari, itakuwa ni ajira kwa baadhi ya watu, kesho wanaweza kuambiwa ya kwamba, kwa nini mmehama wakati hakuna maji, wamefuata maji au malisho ndiyo napenda kusema ya kwamba wafugaji wasinyanyaswe kwa ajili ya maandalizi ambayo Serikali haijaandaa kwa Muswada huu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ndiyo tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Nikumbushe ya kwamba, leo Bunge linarudia Saa 10.00 na siyo Saa 11.00 na tumebaki na wasemaji watatu waliojiandikisha, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe na Mheshimiwa Benedict Losurutia, ndiyo waliosalia.

Kwa hiyo, hadi hapo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi Saa 10.00 Jioni.

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kikao chetu kinaendelea. Labda kabla sijamwita mchangiaji wa kwanza mchana huu, inaoenakana baadhi yetu tumesahau Miswada nyumbani na tunaona aibu kuomba tupatiwe, lakini Miswada hii yote sita imo humu ndani, sasa kama unahitaji unawasiliana na hawa Makatibu tu, Miswada yote sita iko hapa mezani. Kwa hiyo, kwa wale ambao wana shida, wachukue ili tuweze kuchangia vizuri katika Miswada hii.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya awali kabisa mchana huu wa leo ili nami niweze kuchangia machache katika Muswada huu ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu, mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, ambapo wewe ni Mwenyekiti wetu, pamoja na wenzangu, nimeshiriki vizuri sana katika kuuchambua Muswada huu. Tangu asubuhi mpaka sasa yamesemwa mengi lakini nitoe machache pamoja na kukazia yale yaliyosemwa na wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijaendelea, niseme waziwazi kwamba, Muswada huu nauunga mkono mia kwa mia, sina matatizo makubwa, ni ushauri tu wa hapa na pale kutaka ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme kwamba, nakubaliana na mengi ambayo wenzangu wamesema leo asubuhi, wamesema vizuri sana, yako yale ambayo wameyasema tulikwishayajadili kwenye Kamati, lakini yako yale mengine ambayo ni ushauri mpya ambao hatukupata nafasi ya kuupata tukiwa kwenye Kamati. Lakini kwa vyovyote vile, pamoja na yote yaliyosemwa, kwanza kabisa, napenda niseme kwamba, sasa hivi Wizara imepata mwenyewe kwa sababu huko nyuma masuala ya mifugo hayakuwa yanapewa uzito unaostahili hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unakumbuka miaka yote huko nyuma tukizungumzia masuala ya mifugo ndani ya Bunge lako Tukufu, kusema kweli tulikuwa tunazungumza wakati wa kikao cha bajeti na kwenye vitabu vya Waziri aliyekuwa anahusika na masuala ya mifugo, kweli masuala ya mifugo yalikuwa yanapewa *paragraph* mbili au tatu, basi imeishia hapo na hata mtu wa kumkamata shati kwa matatizo ya mifugo alikuwa hayupo. Lakini angalau leo tuishukuru Serikali kwamba, imeunda Wizara hii na kutilia mkazo sana masuala ya mifugo na Miswada hii miwili huu tulioumaliza na huu ambao tunauzungumzia sasa kusema kweli ni hatua za mwanzo kabisa za kuimarisha eneo hili la mifugo na kulipa nguvu na hapo baadaye tunaamini kwamba, litapata tija ya kutosha na hatimaye kuweza kusafirisha mazao ya mifugo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa nimpongeze Waziri anayehusika, Naibu wake na wenzake, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, sasa mifugo inazungumzwa waziwazi, hadharani na Miswada hii kwa mara ya kwanza inakuja kwa ajili ya kusaidia eneo hili la mifugo. Kwa hiyo, nikubaliane kabisa kwamba, sasa masuala ya mifugo, yamepata mwenyewe, chini ya Ndugu yangu hodari, Edward Lowassa, hasa kwa kazi nzuri anayoifanya, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kuchangia, napenda nitoe maoni yangu kuwasaidia baadhi ya wenzangu waliotangulia kuchangia. Suala hili la mifugo kufugwa kiholela kusema kweli huu ndio mwanzo wa kulipiga vita kwa sababu huko tunakokwenda haitawezekana mtu aswage ng'ombe wake kutoka Kaskazini mpaka Kusini na dunia nzima haifugi kwa namna hiyo. Huko Botswana ambako tunatoa sana mifano ninaamini wameanzia mahali pazuri wakafikia hatua hii ndio maana mazao ya nyama na mazao mengine ya mifugo yao huwa yana bei nzuri sana katika soko la dunia. Huwezi ukapata soko zuri la kuuzia mazao ya mifugo kama mifugo yenyewe haiangaliwi na kutunzwa vizuri, haiwezekani. Kwa kweli tuwaandae watu wetu wafahamu, kule kwangu na mimi ninao nawaita wachungaji wenzangu, hawataki hapa lakini kwa kweli ni wachungaji wafugaji, ni kule ambako hakuna eneo la kuchunga jumla kwa hiyo unafuga kitu kinachoitwa *zero grazing,* hawa ndio wafugaji hawa wanaoswaga, ni wachungaji hawa rafiki zangu.

Kwa hiyo, tuwasaidie watu wetu wajue kwamba, huko tunakokwenda kusema kweli lazima kila mtu awe na eneo lake, alitunze, liwe na yale yote yanayohitajika kama ni mabwawa, malambo, madawa na majosho, huko ndiko tunakokwenda. Kwa hiyo, tuwaandae watu wetu waelewe kabisa kwamba, enzi hizi za kuchunga jumla muda wake

unakaribia kwisha, ni lazima sasa tuingie kwenye ufugaji wa kileo, ufugaji ambao utatupa maslahi na manufaa makubwa zaidi kwenye soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema wenzangu walisema mengi lakini napenda nikubali kwamba, yapo mambo ambayo pengine yatakuwa magumu kweli katika utekelezaji. Sasa yale ambayo yamesemwa yatakuwa magumu katika utekelezaji, naomba Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, ayaangalie upya. Moja la msingi kabisa ambalo limesemwa ni hili ambalo kwa kweli hatujajiandaa vya kutosha. Ninakubali kabisa kwamba, sheria hii tunayoiandaa sasa hivi ni mwanzo tu wa kujaribu kuzuia matatizo makubwa ambayo yanatumalizia mifugo kila siku, lakini yale mambo ambayo hatujayaangalia vizuri kwa kweli yaangaliwe. Kama mfugaji ana ng'ombe wake 100, 200, hana josho, hana maji, unatazamia vipi asitafute njia ya kwenda kupata maji mahali palipo na maji. Naomba hayo yaangaliwe.

Yale mengine walisema rafiki zangu ya mifugo kufika karibu na barabara kubwa, nadhani yanahusu usalama zaidi wa wenye mifugo wenyewe na pia usalama wa mali na vyombo vya usafiri na abiria. Namwomba Mheshimiwa Waziri, ayazingatie ili wakati anapojumuisha kusema kweli awape watu wetu matumaini na awaeleze wazi wazi kwamba, tunaanza tu kujiandaa kuboresha eneo hili la mifugo lakini mbele ya safari tutafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, pengine niulize tu sikumbuki sana kama tunayo sera ya mifugo, pengine Waziri, atatusaidia, lakini kama hatuna sera hivi tuna mipango gani ya muda mrefu ya kuboresha eneo hili ambalo ni muhimu sana kama inavyotolewa mifano mingi kwamba, baadhi ya wenzetu wanapata faida kubwa kabisa kutokana na mifugo yao, hivi tumejiandaa vipi? Halafu pengine tuelezwe kwa ufupi tu huko Botswana wanakosifiwa sana wamefanya nini, wameanzia wapi na sisi tunashindwa nini.

Nadhani jambo hili litatusaidia sasa, ni wakati ambao hatutakiwi tena tutembee, tunatakiwa tukimbie tumechelewa, raslimali tunazo tunatakiwa kuziandaa vizuri ili tupate faida, tumechelewa lakini baada ya kugundua kwamba tumechelewa naomba tukimbie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimfahamishe Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwamba,ukiacha maeneo ambayo yana mifugo mingi sana, ambako wana vituo vya dawa, maeneo mengi hakuna dawa, dawa hazifiki vijijini. Ukiona kwenye maduka yetu huko vijijini kuna dawa hizo huenda muda wake umekwisha. Dawa za mifugo hazifiki vijijini. Pengine hata mfano alioutoa asubuhi ni kwa sababu hakuna dawa za kuaminika na vituo maalum ndio maana mfugaji huyo ametapeliwa akapata madawa mabovu badala ya chanjo ikawa tiba na kupata hasara ya mifugo yake mingi kufa. Naomba msitosheke tu kwa maelekezo yaliyotolewa na Waraka wa Rais, tujue ni nani anafuatilia Waraka huo na umetekelezwa kiasi gani, nani anahimiza, nani anahakikisha kwamba maelekezo haya yamefika kwa watu kule ambako mifugo ipo. Sasa tukitosheka tu, kwa kweli hatutakwenda mbali na inawezekana tukamdhalilisha Rais wetu na si jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kasi ya kuenea na kusambaa kwa magonjwa haiendi sambamba na kasi ya dawa kufika huko. Ni vizuri tukalijua hilo na Wizara nasema kwa kweli itilie nguvu zaidi na kutafuta namna ya kuwasiliana na wale ambao wanatakiwa wapeleke dawa kule kwa wafugaji vijijini ili kukamilisha nia ya kupambana na magonjwa haya yanayoathiri mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme lingine kwamba, pamoja na kwamba kweli sasa tunajiandaa kuimarisha eneo hili la mifugo, elimu kwa wafugaji na wachungaji ni jambo la msingi kabisa. Watu wengi hawafahamu namna ya kufuga, watu wengi hawajui hata namna ya kuhudumia mifugo yao, hata wale ambao wanafuga kisasa hawajui wafuge vipi. Naomba wataalam wa Wizara hii, wawatembelee wafugaji hawa mara kwa mara na kuwapa ushauri. Kwa mfano, unafuga lakini hata kuandaa majani ili mifugo iweze kuyatumia baada ya mvua kukatika hatujui, hata chakula bora cha mifugo hiyo kichanganywe vipi hatujui, tunaomba msaada huo wa elimu ili kuboresha mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine limezungumzwa na wenzangu na mimi nalisema ni ughali wa dawa za mifugo, dawa hizi ni ghali kweli kweli, dawa ni ghali ajabu sijui inakuwa vipi pengine tuelezwe. Kama dawa za binadamu zinapata unafuu wa ushuru zinapoingia hizi hazipati au vipi? Kama bado nadhani ni muhimu Serikali ikaangalia upande huo kwa sababu ni lazima uwekeze ili uweze kupata faida kama huwekezi usitarajie kwamba utapata faida, dawa hizi ni ghali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda Waziri anielimishe na kulielimisha Bunge lako Tukufu ni kwamba, baadhi ya hawa vijana wataalam wa mifugo wako kule vijijini, kazi zao wanajitahidi kuzifanya lakini kwa sababu sasa dawa hizi hazipatikani na hazifiki vijijini, wao ndio wanakuwa *agents* wa dawa zile wananunua sijui kwa pesa zao, wanatuhudumia na mimi wamenihudumia sana, nashukuru, nawalipa lakini watu sasa hawaeliwi tofauti ya kazi zao halisi na shughuli hii wanayofanya. Pengine ni vizuri Wizara itoe ufafanuzi, mimi naelewa sasa unapoeleza wewe kila siku inawezekana isiaminike vizuri, lakini ikitoka kwenye kauli ya Waziri itakuwa kauli ya msaada sana na kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tunaomba Waganga wa Mifugo vijijini waongezwe na kupelekwa kule ambako hawatoshelezi kwa sababu naamini maeneo mengi hakuna watu hawa na kuwakosa ni matatizo. Leo asubuhi tumepitisha ile sheria nyingine inayowahusu wataalam hawa, namshukuru sana Waziri, naishukuru Wizara hii kwa kuwatambua wataalam wale wa chini katika vyeti vile ambavyo amevitaja. Huko nyuma ilikuwa vigumu sana kuwatumia hawa, maana kisheria hawajulikani lakini sasa hivi wanajulikana, ni vizuri tuweze kuwatumia na wapelekwe maeneo mengi ya wafugaji ili waweze kusaidia kwa utaalam wao na hasa msaada wa kujaribu kuelimisha watu ili kuepukana na magonjwa hayo ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishasema kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati iliyochambua Muswada huu, Muswada huu tuliuchambua vizuri sana lakini ulinipa nafasi hii nikafurahi kwamba nichangie yale machache ambayo nadhani nastahili kuyasema hapa na baada ya kusema hayo, kusema kweli naomba ufafanuzi tu kama tunayo sera na

sera hii ina programu gani ya utekelezaji na mawazo yetu ya kuendeleza *industry* hii ya mifugo yakoje huko baadaye ili tufanane na wenzetu kama hawa wa Botswana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nirudie tena kusema naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada wa Magonjwa ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wataalam wa Wizara yake, kwa kuja na Muswada huu ambao kama utatekelezwa, basi utaboresha sana sekta nzima ya mifugo. Sekta hii ni moja ya maeneo ambayo yanaweza kuiondoa Tanzania katika umaskini na inaweza kuiondoa Tanzania kwenye umaskini kwa kutumia utaalam ambao tayari upo, tunaujua na tunaweza kuutumia tukawaondoa wananchi wetu wengi sana kwenye umaskini na tukapandisha sana Pato la Taifa kwa kutumia sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kama tungekuwa na wafugaji wa kuzalisha maziwa milioni moja tu, ambapo kila mmoja awe na ng'ombe anayeweza kutoa lita 20 na tukaweka wastani wa wafugaji hawa kutoa lita 10 kwa siku, wangeweza kuzalisha shilingi trilioni 1.5 kwa mwaka. Sasa mapato hayo ni makubwa sana kwa sekta ambayo kwa kweli tuna ujuzi na utaalam wa kufanya mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilonalo ni utekelezaji. Kama tukitekeleza yale makubaliano tuliyokuwa tumefikia kwenye ule mkutano wa wadau kule Arusha mwaka 2001, basi mimi wala sidhani tungengoja mpaka 2025 kufikia viwango hivi ninavyovisema, tungefika mapema zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda niipongeze Wizara na wataalam, kwa kuleta Muswada huu. Lakini tuweze basi kuutekeleza na kwa kuutekeleza Muswada huu tutakuwa tumetekeleza upande mmoja wa kuweza kufuga vizuri. Kwa sababu kukabiliana na magonjwa ni sehemu moja na kuwapa mifugo chakula kinachofaa na kuwatunza vizuri ni upande mwingine, ambao huo ungeweza kufanywa kwa kutumia juhudi na utaalam tu wa ugani. Utaalamu wote huu tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondoa magonjwa kunaongeza ubora wa mifugo yetu na inaondoa hatari kwa wananchi kuambukizwa magonjwa na wanyama na pia ingetuwezesha kuuza mifugo nje ya nchi. Hapa tulipo sisi Watanzania tuko kwenye eneo zuri sana duniani. Ukifikiria wakati huu wa Ramadhani ukishaondoka basi tunaangalia mbele Hija, kule kwenye Hija watu wengi wanataka nyama wa kuchinja. Lakini sisi hatuwezi kupeleka mifugo yetu huko kwa sababu mifugo yetu ina magonjwa. Mifugo yenye mafua haiwezi kutoka nje ya nchi ikauzwa. Kwa hiyo, utekelezaji wa Muswada huu ni kitu muhimu sana, tusikiangalie tu kinadharia ndogo ndogo, ni kitu muhimu ambacho kinaweza kubadilisha hali yetu na hali ya wafugaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiondoa matatizo ambayo yameelezwa hapa na wasemaji wa mwanzo na mimi naona mantiki ya maelezo yaliyotolewa, ingekuwa vema sana kama tungeanzisha kupitia Muswada huu, maeneo ambayo hayana magonjwa. Maeneo ambayo tutaweza kuchukulia wanyama tukaanza kuwauzia hapo au *disease free areas*. Sasa Muswada huu ungeeleza uanzishwaji wa maeneo hayo halafu tukawa na mahali pa kuanzia. Kinyume cha hapo, tutakuwa tunachunga tu na kuchunga kama *tradition* hakuwezi kutuondoa kwenye umaskini. Ni lazima tuondoke kwenye kuchunga tuingie kwenye ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimwia Mwenyekiti, lingine nataka nitoe rai rasmi kabisa kwamba, ingekuwa vizuri Wilaya zote nchini zikawa na *Veterinary Officers* ili basi utekelezaji wa Muswada huu uwezekane. Kwa sababu mtu ambaye anajua kidogo magonjwa hawezi kutekeleza mahitaji ya Muswada huu. Muswada huu unataka utaalam na ingekuwa vizuri tukaanzia hapo kwamba, kila Wilaya iwe na Daktari wa Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Wilaya zile ambazo ziko mpakani kama Mwanga, miaka mingi hatuna *Veterinary Officer,* tuna Bwana mmoja anashika madaraka yote, yeye ni *Agriculture Production Officer,* yeye ni *Animal Production Officer*, yeye ni *Veterinary Officer,* mimi sijapata kuona, wala sijui mtu huyu anachojua vizuri ni kitu gani. Lakini ingekuwa vizuri katika Wilaya ambayo inapakana na nchi ya Kenya ambapo sasa ina Sotoka tukawa na *Veterinarian.* Pale Mwanga hatuna Daktari sasa Sotoka ikiingia pale tutafanyaje. Unafanya nini na ziko Wilaya nyingi za mpakani, pamoja na Wilaya yako Mheshimiwa Waziri? Alikuwa anasema kwa ukali kabisa hapa Ndugu yangu Laizer na mimi nimemwelewa kwamba, haiwezekani labda kwako kule una *Veterinary Officer,* lakini Mwanga hakuna na suala hili nimelisema, nime-*lobby,* lakini wapi. Sasa nataka kuomba rasmi kabisa kwamba, tukitoka hapa basi *Veterinary Officer* awekwe kule Mwanga ili Sotoka isije ikaingia ikatuharibia mifugo yote nchini kwetu na Sotoka ni kitu *serious. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la msingi zaidi kule kwenye Wilaya hakuna Wizara ya Mifugo. Sekta ya mifugo imechanganywachanganywa tu, ipo chini ya Wizara ya Kilimo. Sasa jamani kama tumekubali kuwa na Wizara ya Maji na Maendeleo na Mifugo, basi twende nayo mpaka kwenye kijiji maana inapofika kwenye Wilaya, amri za Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo zinaweza kuwa hazifiki na kama zinatungwa kwenye sheria nzuri namna hii, zinatakiwa ziende mpaka kule chini. Kwa hiyo, tungependa kabisa kimuundo kule kuwe na Afisa Mifugo wa Wilaya, tusiwe kama tulivyo sasa tumechanganya mifugo, kilimo, *veterinary.* Tunachanganya kama mtu unapika uji unaweka maziwa. Haiwezekani. Kwa hiyo, ili tuweze kutekeleza Muswada huu, ni lazima kimuundo tuanzie juu mpaka chini, lazima tuwe na Afisa Mifugo wa Wilaya na lazima tuwe na Mganga wa Mifugo wa Wilaya. Tukifanya hivyo, basi tutaweza kutekeleza Muswada huu, kinyume ilivyo sasa hakuna muundo wa kutekeleza Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu dawa za mifugo. Kule kwenye Wilaya ukienda kwenye maduka ambayo zinauzwa dawa za mifugo, dawa hizi kama walivyosema wenzangu, ni ghali sana lakini hiyo siyo pekee.

Gharama zake zinazidi kwa sababu ubora wake hauwezi kuthibitishwa. Tunanunua madawa kule kwenye maduka ya vijijini hata kule kwenye Mikoa mengi ni feki tu, yamewekwa vizuri lakini ubora, ile *content* ya *active ingredient,* ni kidogo sana na watu wananunua madawa haya wanawapa ng'ombe na ng'ombe wanaendelea kufa. Kwa hiyo, tuwe na utaratibu wa kuangalia ubora wa madawa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa tumeomba Kituo cha *TPRI* kule Arusha kipewe meno kidogo ya kuweza kwenda kukagua na kuangalia kama madawa yana ubora ambao unastahili ili yaweze kutumika katika kilimo na mifugo. Napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, suala hili liangaliwe kwa nguvu kabisa, madawa haya ni ghali sana lakini zaidi ya hapo ubora wake ni wa utatanishi. Kwa hiyo, tungeomba sana suala hili liangaliwe kwa undani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yameshaongelewa na wenzangu na napenda sasa nitamke rasmi kwamba, naunga mkono hoja hii na napenda iangaliwe kwa upana wake ili iweze kutufikisha katika azma yetu ya kuondoa umaskini kupitia kwenye sekta hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Niendelee tu kuishukuru sana na kuisifu Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Waziri, pamoja na Naibu wake na wataalam, kwa kuweza tena kuleta Muswada huu wa kudhibiti magonjwa ya wanyama au mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono Muswada huu vizuri sana. Muswada huu ni muhimu sana na ulikuwepo tangu zamani ila ulikuwa kwenye *archives* haukufanya kazi, ulikuwa *dormant* mpaka Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ikaenda kuuliza kwenye *archive* kwamba uko wapi? Kwa hiyo, tunashukuru sana. Enzi za Ukoloni Muswada huu umefanya kazi ndio ikaanza *stock routes, veterinary centers,* shughuli nyingi sana tukaja mahali kama historia inavyosema tuka-*cease* kwamba, Muswada huu hauna kazi. Sasa ndio maana hatua 200 kutoka barabara, hiyo enzi ya Ukoloni sio Muswada huu, mambo mengi hapa yalikuwepo sasa tumekuja inarudi tunaona sasa kuna mabadiliko na ndio imekuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, naomba tu Waziri katika kanuni zake, kuna mambo ambayo yapo katika Muswada huu, mimi narudia kusema kuna ufugaji wa ng'ombe za asili na ng'ombe wa kisasa na lazima tugawe huu ufugaji wa kisasa. Ukijaribu kuchanganya ufugaji wa asili unapingana kabisa na Muswada huu kwa sababu wao kuna mambo mengi sana ambayo hawajafanyiwa.

Mathalani ukitaka kusafirisha ng'ombe kuwapeleka katika ufugaji wa kisasa Ranchi ya Kongwa, lazima uwapakie kwenye malori uwapeleke Dar es Salaam, lakini ukitaka kusafirisha ng'ombe kutoka mnada wa Ngaruka kwenda Ngaranaiboru, hakuna lori kwa hiyo wao wataendelea kusafirisha hivyo mpaka watakapopata malori. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kitu kimoja tu, katika *centers (market),* kuna masoko kama tunapokwenda Weruweru, tunapokwenda katika minada mikubwa tunakuta wafanyabiashara wakubwa. Ukikuta wafanyabiashara wakubwa, hakuna mfanyabiashara siku hizi mkubwa anayetaka kuswaga ng'ombe, lazima anakuja na malori. Kwa hiyo, tunaomba twende taratibu ili hawa wafugaji wa asili tuweze kwenda nao pamoja.

Hilo tunaomba kidogo kwamba, kwa mazingira tuliyonayo, nadhani mpaka tubadilike lakini mwisho zaidi ni lazima tutafika mahali kutakuwa hakuna kuhamahama kwa mifugo, lazima tufike mahali hapo. Dawa yenyewe kwa sababu Waraka Na.1 wa Rais haujatekelezwa, mimi nasikitika sana, Na.2, Na.3, Na.4 zikoje? Mimi nina wasiwasi kabisa na ule ni muhimu sana kwa sasa yafanyike marekebisho kwa sababu asilimia 15 hatuna sasa katika Halmashauri, tumefuta kodi na kadhalika hata ile ya wanawake na vijana imekuwa matatizo kabisa, asilimia kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana suala la wafugaji kupata sehemu zao na wakulima kutenga maeneo, matumizi bora ya ardhi, ni muhimu sana katika suala hili, tukipuuzia tutapata matatizo na kila mtu, nashukuru sana sasa hivi tunabinafsisha ranchi na nadhani wafugaji watapata nafasi, tunamilikisha lazima twende kule ukitaka ufugaji mzuri uwe na eneo lako.

Tunaomba, tutapeleka *application,* ndio wakati wetu sisi Wabunge kupeleka *application* kule na watu wengine wote ambao wana nia ya ufugaji katika nchi hii, wapeleke maombi ili tupate ufugaji bora katika nchi hii.

Sasa sio mtu anapeleka akipata heka 2,000, 6,000 au 10,000 unaanza kusema amepataje, hapana, ndio namna ya ufugaji. Kwa hiyo, ukipata heka 10,000 usishangae maana yake heka 10,000 unaweza kufuga ng'ombe 400, 500, 600 na ng'ombe ni *petrol,* yaani kama unataka utajiri wa haraka nenda kwenye mifugo, utakunywa maziwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu suala la madawa, kwa kweli hili suala ni *very clear.* Majosho, sio suala unaona josho tu, kuchimba josho, kukarabati na kupaua haina shida, mimi ninayo mengi, suala ni dawa za josho. Sasa hivi *drum* moja la lita 200 ni shilingi kumi na moja milioni na kitu, lita moja ya *super deep* ni Sh. 58,000/=. Sasa usipoangalia hiyo tupate hela kidogo ya kusaidia hawa wafugaji, tumejaribu kuendesha *deep,* majosho hatuwezi kabisa. Suala la kuuza lita 200 kwa shilingi kumi na moja milioni utapata wapi. Kwa hiyo, kama *subsidies* zimetoka kwa mbolea na mambo mengine, angalieni kwenye majosho na sisi wafugaji tusaidiwe hata kama nusu basi iwe Sh.20,000/= kwa lita tunaweza kugharamia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hilo tu, kuna dawa nyingi za majosho, kuna *super deep, tactic, staledone, dominance, conflix*, sasa hujui imeletwa tena hii *conflix* hujui namna ya kuchanganya dawa zote zilizopo. Kwa hiyo, sasa wafugaji hatujui tuwaogeshe dawa ipi, ikitoka hii unaletewa hii, kwa hiyo, tunaomba nadhani katika sheria

tuliyopitisha asubuhi itatusaidia kwa hili kwa wataalam kuanza kuchunguza. Kwa hiyo, tunaomba sana halafu *veterinary centers,* hii mara kupeleka Temeke au wapi, hebu tujaribu, kila Wilaya kulikuwa na *Veterinary Center*, tulianzisha zipo lakini sasa hivi tumefanya nyumba za madaktari, hakuna kifaa chochote, lakini kila Wilaya kipo tumejenga, tuvifufue tena kuliko kukimbiza dawa mpaka Temeke kutoka Kiteto, tunaweza tukapima na sisi pale. Kwa hiyo, tujaribu kufufua ili tuweze kuendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu la mwisho kabisa ni hii alama. Nazungumza alama maana yake, Mheshimiwa Lekule asubuhi alizungumzia kwamba, alama kwetu ni muhimu sana. Juzi nilipokuwa nyumbani, ndama wangu mmoja alipotea, sikumweka alama, nilimnunua kwa mtu tu, lakini ana alama yake, sasa vijana wangu walikwenda kumtafuta wakamwona, walipomwona wakamwambia yule bwana ni ndama wetu, akawauliza kwa nini, mbona alama yenu siyo hii, hii ni ya boma fulani? Akawarusha hivi hivi, wakamwambia basi, wakaja kunieleza, nikaenda kumwangalia kweli ni ndama niliyemnunua kule, tulibishana na sisi tuna mambo ya kimila, kama mtu anataka kukurusha, hatwendi Mahakamani. Nilipofika pale nikamwambia lete sime hapa tukate sikio la ndama, damu ikidondoka tutajua ni ya nani. Akasema ahaa, basi kama hivyo hapana basi akanirudishia ndama wangu vizuri, nikaja kumuwekea alama. Sasa kwa mambo haya ya alama ni muhimu, wewe unaelewa kabisa nchi Oledimama ni ukoo wangu, mpaka huko Norok. Ng'ombe wa Oledimama na wangu alama ni sawasawa tu ya sikio hivi, sasa hawa wa Ngidong'i hawa akina Mheshimiwa Leizer mpaka Kiteto hata yeye mwenyewe si wako ni wa Mto wa Mbu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lazima twende kwenye siasa, twende taratibu, tuondoe alama ambazo kwa kweli hazifai kwa sababu kuna alama kweli ambazo zinaharibu ngozi, halafu kuna alama ambazo ziko *modern,* lakini lazima wananchi wapate elimu kwa sababu usipowapa elimu italeta vurugu ambayo ni kubwa sana, kwa hiyo, tunaomba sana suala la alama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, suala la wanyamapori limechelewa sana. Sasa tumeweka vizuizi kwa mifugo, wanyamapori wanapotoka kwenye *National Park* wanakuja kwenye maeneo yetu na kutuletea magonjwa, umeweka sheria ipi na fidia ya namna gani, kwa sababu wanaleta ile inayoitwa *catter fever* ugonjwa unapokuja kuzaliana? Wanaacha mifugo yetu inakufa, tukimwuliza Waziri wa Maliasili na Utalii, anaturuka. Sasa kwa sababu ni lazima kila mtu atunze mifugo yake, kama sisi tukiingia *National Park* tunalipa faini, wao wakitoka wapo huru, halafu wanatuletea maradhi, sasa lazima tu-*table* hiyo ili tuweze kupata fidia, kama umeweza kutoa fidia kwenye mambo mengine sasa wale wanyamapori wakileta magonjwa kwenye maeneo yetu basi tupate fidia, tunataka fidia sasa, la sivyo iwe na *control* kwani wanyamapori nao wana maradhi sawasawa na mifugo au kuzidi, lakini wao wamepewa madaraka makubwa zaidi, wanaweza kwenda popote na kuvuka barabara na kufanya chochote kuliko mifugo kuliko wanyama ambao tunawatawala sisi. Kwa hiyo, huwezi kusema kwamba, huu ni mwisho wa *National Park,* hapana, wao wanavuka lakini ng'ombe wakienda *National Park*, faini, yaani mambo mengi! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofika mambo ya maeneo, kwa mfano pale Simanjiro, kama wanyama wakienda kule wanalibatiza lile eneo kuwa ni *controlled area.* Tupo ndani huku lakini tunaambiwa hili ni *controlled area* ili yule mnyama alindwe au *open area*. Kwa hiyo, tunaomba sana katika suala hili, muweze sasa kukaa pamoja, Wizara mbili, muweze kufikiria kwamba sasa tumeshaweka hivi na mafaili yapo mengi sasa tutafanyaje na hao wa kwenu. Sijui Kusini simba wakila watu wanafidiwa au vipi, nasikia tu akina Mheshimiwa Akukweti, sijui kama wana fidiwa au wakishachukua nyama basi simba tu anakwenda kusubiri upande mwingine sina uhakika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunikaribisha nimalizie hoja yangu, lakini naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote wale waliochangia na wale waliokaa kimya, maana wote wameunga mkono Muswada wangu, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe waliochangia kwa kuzungumza ni Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Shaweji Abdallah, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Ole-Timan, Mheshimiwa Losurutia, Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Bendera, Mheshimiwa Mongella, Mheshimiwa Laizer, Mheshimiwa Kasaka, Mheshimiwa Kagonji na Mheshimiwa Maghembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mwanri, Mheshimiwa Semindu Pawa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zimetolewa nyingi sana, zipo hoja nitajibu, zipo hoja ambazo nitazichukua lakini nimezingatia na wataalam wa Wizara wamejaa pale tumezichukua tutazifanyia kazi Wizarani. Kwa hiyo, ukiona sijibu basi ujue zipo katika kapu la kushughulikiwa kule Wizarani. Lakini nilitaka nianze na hoja moja ya msingi kabisa kwamba, sisi kama viongozi, uelewa wetu katika sekta ya mifugo ni vizuri wote tukawa na uelewa unaofanana ili tuweze kuwaongoza wananchi wetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba, tunatekeleza maamuzi ya msingi ya Chama chetu. Tulisema katika Ilani ya Uchaguzi, ibara ya 17, tubadilishe ufugaji wetu kutoka ule wa jadi na kwenda kwenye ufugaji wa kisasa, unaozingatia ubora wa mifugo kuliko wingi. Huu ndiyo uamuzi wa msingi wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, kazi yangu ya msingi Mheshimiwa Ole-Timan, ni kutekeleza maelekezo haya na lazima tujue kwamba, dunia ya sasa ni soko moja la kibiashara, tunafuata *WTO,* tuna *OIE* kama unapokaa pale Sakala ama Olosokwan, unaona *CNN*, mwenzako aliyepo Marekani anaona *CNN* hiyo hiyo, ujue kwamba, soko la dunia vile vile lipo hivyo hivyo, kwa hiyo, mfugaji tunamsaidia afanane na soko la dunia na siyo arudi katika maisha ya Sakala au Olosokwan. Katika hilo ningekuomba tuelewane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatekeleza pia sera ya kilimo na mifugo ya mwaka 1997, ambayo msingi wake ndiyo sheria hii. Lakini kama alivyonisaidia Mheshimiwa Losurutia, namshukuru sana. Waheshimiwa Wabunge, sheria hii ni ya mwaka 1940 ilikuwepo, wakati wa ukoloni wakaitekeleza sana na baada ya uhuru tukaitekeleza, baadaye tukaiacha kwa sababu ambazo sijui ni za nini, kwa hiyo, si kwamba tumeanza jambo jipya, mengi ni mambo yale yale lakini kuna *running thread up* ambayo wamesema Waheshimiwa Wabunge wengi kama Mheshimiwa Kasaka, Mheshimiwa Bendera na Mheshimiwa Mongella, suala la usimamizi wa sheria zetu ndiyo tatizo hapa. Kwamba, sheria hii ilikuwepo ilikuwa haisimamiwi na ndiyo maana ufugaji wetu ukaenda holela. Nitafafanua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nipitie baadhi ya maeneo. Hili suala la alama, kwa hakika nadhani limekosewa kabisa kueleweka na waliolisemea sijui kama waliitazama ile sheria. Sheria inazungumza juu ya yule mtaalam akishakuja kwenye kundi akagundua kundi hili lina magonjwa anawaweka alama kwa madhumuni ya kumtambua yule mnyama ambaye ni mgonjwa. Hatufuti hata kidogo alama za jadi zitaendelea na ziendelee kudumu. Sasa rafiki yangu Lekule ameongea kwa masikitiko sana akasema inaweza kumkosesha kura 2005, mimi nadhani itakupa kura nyingi mwaka 2005 kuliko jambo lingine lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii, nimsifu sana Mheshimiwa Lekule Laizer, ana mifugo ya kutosha. Lakini siyo hiyo tu, yeye ana Chama cha Ushirika cha Mifugo alichoulizia hapa asubuhi, lakini kubwa zaidi sasa hivi zipo chanjo ambazo mkianza kuzitumia mifugo inadumu. Kwa mfano, chanjo ya ndigana, ukichanja chanjo ya ndigana una hakika asilimia 70 mpaka 80 ya ndama wako kubaki. Katika Jimbo lake amekuwa mfano, ningetumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namwomba akubali kwamba, mabadiliko kama hayo ndiyo lazima tuyapeleke kwa watu wetu ili watu wengi zaidi watumie chanjo, watu wengi zaidi wapate mifugo mingi na uchumi uweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kuchunga mita 200 kutoka barabara, hii ni sheria inayoitwa *Highway Ordinance* ya mwaka 1967, sisi tumeichukua mle tu lakini busara zake ni nini? Busara ni kwamba, nitaeleza baadaye kwa nini lazima usafirishe kwa lori, unasafirisha kwa lori usipoweka mita 200 wale ng'ombe wanaofuata majani mabichi pale watapata magonjwa ambayo wale ng'ombe kwenye lori wanayo. Kwa hiyo, sheria inakwambia sogeza ng'ombe wako mita 200 na *insurance* vile vile akigongwa ng'ombe katika barabara hawamlipi. Ukienda Mahakamani mwenye ng'ombe ndiye mwenye kosa na ng'ombe ndiye mwenye kosa si lori kwa sababu ipo *Highway Ordinance* inalinda hii. Katika maeneo mengine hata Wilaya ya Monduli ambapo barabara inapita kwenye eneo la mifugo, chini kuna daraja ambako mifugo inapita chini magari yanapita juu. Maeneo mengine kuna *bumps* zinawekwa, wanaambiwa kuna mifugo inapita, kwa hiyo unaweka *bump* unaelewa maeneo kama ni ya kuchungia kama jana alivyokuwa anasema Mheshimiwa Lekule, unaweka *bumps* akija mwenye lori anaona ni ng'ombe anasimama, mifugo yako inapita kwa utaratibu, lakini utaratibu huu jamani ndiyo utaratibu wa kisasa wa kufuga hatuwezi kuukataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zingine zimeweka uzio. Mheshimiwa Lekule hakuipenda sana Botswana, lakini Botswana tunaisema makusudi kwa sababu ina mifugo wachache sana kuliko sisi, sisi ni wa tatu Afrika, wao baada ya almasi, zao la pili linalofuata la kigeni ni la mifugo. Kwa bahati mbaya asilimia karibu 80 ya wanaosimamia mifugo ya Botswana ni Watanzania tuliowafundisha katika Vyuo Vikuu na waliofanya katika Wizara zetu, ndio wanaosimamia na wanasimamia sheria hizi hizi lakini kikamilifu, wanasimamia sheria kweli kweli. Siku za *weekend* ikifika Ijumaa, mtu anayefanya kazi Botswana, ikifika saa nane anaondoka, anakwenda wapi? Kwenye *cattle post.* Kila mfanyakazi wa Serikali ana ng'ombe kwa sababu hicho ndicho kipato cha hakika na kikubwa kuliko mshahara, lakini ni kwa sababu wamezingatia taratibu nzuri za kufuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utoaji taarifa saa ishirini na nne, Mheshimiwa Timan, ameuliza mtu kama yuko Ping'ing atatoaje taarifa? Sasa niwaambie ndugu zangu yeye anajua, Mheshimiwa Losurutia anajua, Mheshimiwa Lekule anajua, Mheshimiwa Kone anajua, Mheshimiwa Elisa Mollel anajua, hakuna mahali penye kupeleka taarifa haraka kama Umasaini bila simu, hakuna mahali taarifa inakwenda kama Umasaini. Kwa hiyo, jambo likitokea Kijiji A mara moja limefika Kijiji kingine na hasa kama ni taarifa za mifugo zinakwenda wala hawahitaji *Mobitel, it is faster,* lakini tunafanya kwa nia njema kwamba, taarifa ile ipatikane ili hatua zichukuliwe na ukiangalia ile sheria sehemu ya kumi na tano, ibara ya tano inatoa nafasi ya mfugaji aliye mbali kutoa taarifa tu kwa uongozi wa karibu, nia ni kutoa taarifa ili hatua zichukuliwe. Kwa hiyo, suala la Ping'ing ndugu yangu tafadhali halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *buffer zone*, Waheshimiwa Wabunge, tunaweka *buffer zone* ili kulinda eneo lisiingiliwe na maambukizi. Wakati wa kugawa *ranches,* moja ya *ranch* ambayo imeamuliwa na walianza wakati wa Mzee Malecela kuanzisha *ranch* ya Ruvu kuifanya ni *buffer zone* kwa ajili ya magonjwa kama kuna mifugo inayokuja kwenda bandarini unaimalizia pale kwanza unahakikisha unaitibu ndipo inakwenda bandarini. Kwa hiyo, ume-*create a buffer zone,* inafanyika mahali popote kwa madhumuni ya kutenga mifugo walio wagonjwa na wale ambao siyo wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu kwa wafugaji, nakubaliana mia kwa mia, nakubali kabisa kwamba, tusaidiane kuwaelimisha wafugaji wetu, lakini pamoja na elimu kusimamia sheria kwa sababu mambo haya haya tunayoyakataa yanafanywa Kenya nchi jirani kabisa, mtu yule anayetekeleza Kenya akija upande wa Wilaya ya Monduli hatekelezi, lakini Kenya anatekeleza. Kwa hiyo, naomba pamoja na elimu lakini tusimamie sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala ambalo limezungumzwa kwa kirefu sana juu ya madaraka ya Serikali za Mitaa na Wizara yetu. Mimi ningependa kusema kwamba, maboresho ya Halmashauri yanaendelea na suala la utumishi linaangaliwa. Nakubaliana kabisa na Profesa Maghembe na Mheshimiwa Kagonji walivyosema, lipo tatizo kule

lakini tatizo si la Halmashauri bali lina mambo mengi, nitatoa mfano mdogo. Kwenye Wilaya Afisa Mifugo anatumiwa zaidi kukusanya kodi kuliko kutibu mifugo na akienda kwenye zizi la mfugaji akitaka kujua idadi ya mifugo, mfugaji anakataa, anasema ahaa unataka kunitoza kodi. Kwa hiyo, yapo matatizo wanawajibika kwenye Wizara kwenye mambo ya *profession* lakini kwenye masuala ya utendaji wa siku kwa siku yupo kwa Halmashauri yake. Mara nyingine wameacha kuweka karantini, wanaambiwa ahaa, wakiweka karantini halafu mnada utakuwaje, tutatoa wapi hela. Kwa hiyo, nakubali lipo tatizo lakini tunaendelea na mazungumzo na TAMISEMI na wengine ili kuhakikisha kwamba tunaliondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira ya wataalam, Mheshimiwa Profesa Maghembe, yupo kwao zaidi, ndiyo wanaoajiri. Mheshimiwa Balozi Mongella, aliuliza dawa za asili, ni kweli zipo dawa za asili ambazo zinatibu mifugo, zinajulikana na zimewekwa chini ya usimamizi wa ile sheria mpya ya madawa ya *TFDA* na utafiti unaendelea *SUA, ADRI, TPRA* na katika taasisi nyingine kuhakikisha kwamba, dawa za mifugo zile za kienyeji zinatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo lililozungumzwa la kuhamahama. Namshukuru sana Mheshimiwa Losurutia. Waheshimiwa Wabunge hapa tukitoa *wrong signals* kwenye Bunge hili kwamba tunasema wahame hame tu, waendelee kutoka, utoke Loliondo mpaka Mtwara, utoke pale kwa Mheshimiwa Maghembe mpaka Rukwa, nchi hii itabaki na nini? Kutoka Maswa Usukumani kote mpaka Lindi, hii nchi ndiyo bado kweli ina maeneo, lakini kwa utaratibu huu tutaharibu nchi yetu yote, kwa hiyo ndiyo tunasema tafadhalini hapana kuhamahama, tukubaliane wafugaji wapewe maeneo ya kutosha kufugia. Mheshimiwa Lekule Laizer, unasema una Vijiji vinane vinachungia eneo moja, ndiyo tunataka hivyo, lakini tukishapanga maeneo, hili eneo ni kwa ajili ya mifugo libaki kwa ajili ya mifugo na wenye mifugo wasihame na wenye kilimo waheshimu wabaki kwenye maeneo yao. Lakini tukiruhusu Bungeni kwamba, tunakubaliana na kuhamahama nawaambia magonjwa ya mifugo yataendelea, mazingira yataharibiwa na kila siku migogoro kati ya wakulima na wafugaji itaendelea kwa sababu na wakulima nao hawakubali utaratibu wa kuvamia maeneo yao. Kwa hiyo, naomba tukubaliane kwamba utaratibu wa kuhamahama hapana, tuwajengee wafugaji mazingira mazuri katika maeneo waliyopo ili waendelee na ufugaji, ndiyo tunakubaliana na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kasaka alisema tuwawekee maji, ndiyo tunaweka maji, lakini kwa sasa pesa mnayonipa kwenye bajeti ndiyo naweza kuitumia, nimefanya nini? Bajeti iliyopita tumetoa shilingi milioni 540 tumejenga malambo 132, tayari tumejenga na tunapeleka maeneo yale ambayo wafugaji hawana maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile suala la majosho, kuna Mbunge hapa ameulizia hamuwatengenezei majosho, tumesema majosho ni sekta binafsi lakini hoja je, pale ambapo sekta binafsi haijajiandaa kabisa? Waheshimiwa Wabunge, tumepewa mwaka huu shilingi milioni 945 kwa majosho 196. Kwa hiyo, tunatekeleza mambo hayo. Halmashauri nazo zinatakiwa kuchangia katika hili, huu ndiyo uchumi mkubwa unaofaa kuchangia, lakini nakubaliana kwamba, kuna haja kwa kweli ya kuongeza kidogo fedha

kwa ajili ya majosho na nategemea Waziri wa Fedha, amesikia hoja tutakapozungumza atatukubalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la ukarabati wa miundombinu maeneo ya Kusini, ulisema kule kwamba, *TLMP* wanafanya Kaskazini. Ulikuwepo Waheshimiwa Wabunge Mradi wa *Tanzania Livestock Marketing Project (TLMP)* ambao uligharamiwa na *ADB*, lakini wakati ule wa majadiliano wakakubaliana awamu ya kwanza waanze Kaskazini mwa reli, awamu ya pili ndiyo Kusini mwa reli, Mkataba ulipokwisha wakasema hawana pesa tena tuendelee kwa nguvu zetu, lakini nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mwaka huu tumetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya *stock routes* katika Mikoa ya chini ya reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa Waraka wa Rais Na. 1 wa 2002, Mheshimiwa Bendera amelalamika sana kwamba, haujatekelezwa. Inawezekana haujatekelezwa Korogwe na yeye ni Mbunge wa Korogwe, nilitegemea atamwuliza Mwenyekiti wa Halmashauri na *DC* kwenye vikao kwa nini hatutekelezi Waraka wa Rais, kwa sababu Wabunge pia ni Wajumbe katika vikao hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mpaka sasa Halmashauri 70 zimefungua akaunti za Mfuko wa Kuendeleza Mifugo kutekeleza Waraka wa Rais Na. 1. Vile vile usafirishaji wa mifugo kwa malori unatekelezwa katika Mikoa ya Singida, Dodoma, Arusha, Manyara na Kilimanjaro na Waheshimiwa Wabunge, mliokuja kwa magari mmekutana na malori yanayobeba mifugo kutoka Dodoma kupeleka Dar es Salaam, ni utaratibu ambao umeanza, ni suala la kusimamia, lakini na mimi kama nilivyoahidi, tutafuatilia na viongozi wa Mkoa wa Tanga kumetokea nini wao hawajaanza kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei kubwa za madawa ya mifugo, Waheshimiwa Wabunge, tunakubaliana na ninyi mia kwa mia hata katika semina ya Arusha ya wadau, Mheshimiwa Rais, alielekeza kama tunaweza kutafuta utaratibu wowote wa kupunguza bei ya madawa ya mifugo. Lakini hatua za kwanza tulizochukua ni kwamba, tumeondoa kodi kama ilivyo kwenye magonjwa ya madawa ya binadamu katika madawa ya mifugo. Vile vile tumeiondoa na tunategemea kuendelea kutafuta *formula* lakini tujue kwamba, wanaotengeneza madawa haya ni *multinational* na wameamua kutengeneza huko kwao, hawataki kutengeneza viwanda kwetu na kwa hiyo bei inaendelea kuwa kubwa. Kama tukipata *formula* au kama kuna Mbunge mwenye *formula* ambayo anafikiri inaweza kutusaidia, tutakuwa tayari sana kupokea maoni yao. Lakini kwa dawa za kinga, niseme Wizara yangu ni moja ya Wizara ambayo inao wataalam waliobobea kweli kweli katika utafiti na mambo haya yanayofanana nayo. Hivi sasa wametengeneza kinga ya mdondo, ya kimeta na chambavu pale Temeke Dar es Salaam na wanaendelea na utafiti wa kuangalia uwezekano wa kutengeneza ile chanjo ya homa ya mapafu na homa ya miguu. Kwa hiyo, nategemea baada ya muda mfupi, *Inshallah*, tutafika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la ngozi, usimamizi wake unasimamiwa na Sheria Na. 704 ya mwaka 1962, yaani *Hides and Skins Trade Act*, lakini tuna tatizo la ngozi.

Kuna mkubwa mmoja ana kiwanda hapa cha ngozi, amepata watu wa kuingia naye ubia, wale watu wakazunguka nchini kidogo, baada ya muda wamemkatalia wakilalamikia *quality.* Ubora wa ngozi yetu bado una matatizo mengi sana.

Kwanza, kuna watu wanaopiga chapa kienyeji, wanapiga chapa kwenye nundu, sasa ngozi ukishaipiga chapa umeiharibu. Kuna wengine akiugua kidogo anapiga mstari hapa. Kuna hawa wanaosafirishwa sasa miba inachana ngozi yote ikifika siyo *quality* inayotakiwa. Ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge, mipango yote hii kwa pamoja inataka ubora na duniani inatakiwa ngozi bora. Lakini kama tulivyosema, tutaendelea kuwaelimisha na sisi tufike katika hatua hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa jambo moja la mwisho. Nakubaliana kabisa na Wabunge, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Getrude Mongella na Mheshimiwa Benedict Losurutia, kwamba tatizo ni usimamizi.

Tulikwenda Botswana baada ya kushangaa sana tukauliza, hebu tuelezeni siri ya mafanikio yenu ni nini? Wakatueleza *Stringent Veterinary Regulations*, wanazisimamia kwa ukali kiasi ambacho hakuna njia ya kufanya mchezo. Ng'ombe wa Botswana akiwa na kupe, mfugaji anatozwa faini, zinakaribia shilingi 100,000/= kwa kupe mmoja na Waheshimiwa Wabunge sheria hizi ndivyo zinapaswa kusimamiwa Kimataifa.

Nitawapeni mfano, mwaka 1984 Rais Mugabe, alikwenda nchi moja ya jirani ya Afrika Mashariki, akapewa ng'ombe, alipokwenda nyumbani akatuma ndege na wataalamu, wakawachukua ng'ombe hao wakawapeleka Harare, hawakutoka *Airport* ya Harare wote walichinjwa. Ni zawadi ndiyo, lakini waliona kwamba, wana magonjwa na wote walichinjwa. Tanzania tulitoa zawadi ng'ombe 108 kwa Msumbiji, wataalamu wakasema bwana kwa masharti yaliyoko hapa, ng'ombe hawa wa Tanzania *sorry,* ilitengenezwa *barbecue* moja kubwa ambapo walialikwa na Watanzania wengine wakashiriki, *barbecue* hiyo ya Kimataifa ng'ombe wote 108 walichinjwa kwa mpigo na wakaliwa wote hawakuwapeleka kuchanganya na mifugo yao. Hizo ndizo Stringent Government Regulations.

Nimetoka Rukwa mwezi uliopita, nilipokwenda pale mpakani wakaniambia mzee kuna biashara nzuri sana ya mnada, nikawauliza kwa nini hamuuzi ng'ombe mnauza nyama, wakaniambia, ng'ombe wa Tanzania wakiingia Zambia wanapigwa risasi, ndiyo, lete nyama yako lakini hapana kuleta magonjwa hapa.

Sasa na mimi nieleze mfano wa mwisho, nimesikia hao kondoo 52,000 wa Australia, walinunuliwa na mfanyabiashara mmoja wa Saudi Arabia, akapeleka kwenye soko lake la Saudi Arabia, soko liko salama kabisa, hakuna tatizo. Lakini walipokuwa wanawasafirisha wakagundua wana ugonjwa, sikumbuki jina vizuri. Walipokuwa kwenye *high seas,* Saudi Arabia ikakataa ikasema hawawataki wale kondoo kwa sababu ni wagonjwa.

Kwa sababu kule *Middle East* walikubaliana, akikataa mmoja na wengine wakatae, kwa hiyo, *Middle East* wote wakakataa. Tumekaa siku moja ananipigia simu Balozi wa Australia akiwa Nairobi, lakini ana *communicate* Tanzania akasema, nina jambo muhimu sana nataka tuzungumze. Akaniuliza umesikia habari ya hao kondoo? Nikasema nimesikia sana, akasema tunataka tuwapeni Tanzania bure, mna *capacity* ya kuwapokea na kuwatumia, nikasema hili ni jambo kubwa niletee kwa maandishi, akalileta kwa maandishi. Tukalichambua, tukalipeleka kwa viongozi wa juu, tukasema hapana bwana, ahsante sana, lakini *we are sorry*. Wakiingia kondoo 52,000 hapa kwanza *handling* yake ni matatizo, lakini huna hakika wana magonjwa gani ambayo yatakulazimisha kondoo wako wote nchini wamalizike kwa sababu ya bure, tukakataa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na bila kufuata utaratibu huo, tutaendelea nchi yetu kuwa mahali pa kuleta magonjwa na sisi tutaonekana Kimataifa hatukubaliki. Nitawape mfano wa mwisho, kuna biashara ya ndege hapa nchini ni kubwa kweli, tunapeleka ndege hai Ulaya, tunapeleka Marekani. Tumepata taarifa kutoka Marekani, miezi kama miwili iliyopita, wakatuambia ndege wenu wana ugonjwa wa mdondo, watalaamu wa kwetu wakasema, lakini mdondo mbona ni kwa ajili ya kuku tu. Wakawaambia zuieni ndege wenu wasije, tutakuja wenyewe, wamekuja. Kwanza, wameangalia mahali wanapokaa ndege kabla ya kusafirishwa, wakatazama sehemu nyingine zinaridhisha na sehemu nyingine haziridhishi. Lakini wakasema, bwana sikilizeni pamoja na kuja kwetu, ndege wa Tanzania hawaruhusiwi Marekani mpaka mmemaliza habari ya magonjwa yenu ya mdondo hata kwa ndege, kwa sababu hutaki kupokea kitu katika nchi yako ambacho kitakuharibia mifugo yako na soko lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Magonjwa ya Wanyama wa mwaka 2003 *(The Animal Diseases Bill, 2003)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu una vifungu zaidi ya 60 na mkiangalia muda wetu kwa leo tunatakiwa tumalize angalau saa 12.00 jioni, kwa sababu kuna wenzetu ambao wamefunga. Kwa hiyo, natoa ushauri kwamba, twende sehemu kwa sehemu, sijui hilo linakubalika? Ndiyo linakubalika, basi ahsante sana tuendelee.

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 5

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi kidogo au majibu ya Mheshimiwa Waziri. Wakati nilipozungumzia migogoro ya wakulima na wafugaji, Mheshimiwa Waziri, alikuwa ametuahidi kwamba, tungejengewa mabwawa, lakini alisema walipata fedha ambazo wamejenga katika sehemu nyingine, kule Wilayani Chunya hatujajengewa na mgogoro huo bado ni mkubwa katika Wilaya ya Chunya, anatuahidi nini kwa sasa hivi?

Kwa sababu alikuwa ametoa ahadi hiyo wakati ule na kwa kweli anapotamka Mheshimiwa Waziri, kwa uzito wake na viongozi waliokuwepo walilichukulia kwa uzito huo huo. Sasa tungependa angalau atuambie na sisi tutafikiriwa lini, baada ya kuwa amejenga katika sehemu nyingine huko?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba, liko tatizo katika Wilaya ya Chunya ambalo tunalifahamu na niliwahi kulielezea. Lakini ningependa kusisitiza maelezo yangu niliyotoa hapo kwamba, kwa kweli viongozi wa Wilaya na Mkoa wana kazi pia ya kuwaelimisha wananchi hao na kujaribu kuwasaidia kutatua matatizo yao. Pale panapowezekana, kama nilivyomwahidi Mheshimiwa Njelu Kasaka, tunatafuta fedha zinazowezekana kupatikana kusaidia kujenga mabwawa na majosho katika maeneo yale ambayo wale wafugaji watahamia, lakini jitihada kubwa tunazitegemea ziwe za Wilaya na Mkoa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 9

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Magonjwa ya Wanyama wa mwaka 2003 *(The Animal Diseases Bill, 2003)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Magonjwa ya Wanyama kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na mabadiliko yake. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa *The Animal Diseases Bill,* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada tumeshaumaliza, sasa nina matangazo mawili. Moja, ni lile ambalo lilitangazwa wakati wengine hawapo kwamba, iwezekana tulipochukua Miswada tukaenda nyumbani tumeisahau. Ile Miswada yote ambayo tumeisahau iko hapa, wale wenye shida wamwone Katibu Mezani ama wawatume vijana wetu wawachukulie.

Waheshimiwa Wabunge, kesho tutakuwa na Miswada miwili, *The Public Service (Negotiating Machinery) Bill, 2003* na *The Seeds Bill,2003.* Hiyo Miswada miwili kama huna unaweza kuja kuchukua hapa.

Sasa baada ya hayo na kwa sababu shughuli ambazo zilipangwa leo zimekwisha, basi naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.18 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 5 Novemba, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*